

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nne - 29 Januari, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 39

**Watumishi Hewa Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2006/2007 Serikali ilipofanya uchunguzi wa ajira za Watumishi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı iligundua kuwepo kwa Watumishi hewa zaidi ya elfu moja (1,000) ambao walisababisha hasara ya mabilioni ya fedha za Serikali; na kwa kuwa, mwaka 2008/2009 uchunguzi huo huo ulifanywa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kugundua kuwepo watumishi hewa zaidi ya elfu moja (1,000) pia; na kwa kuwa, ajira Serikalini hutawaliwa na kuongozwa na Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali za ajira:-

(a) Je, ajira ya watumishi hewa inasababishwa na nini?

(b) Je, katika kipindi cha miaka minne (mwaka 2006 hadi 2009) Serikali imepoteza fedha kiasi gani kwa kulipa watumishi hewa na ni kutoka Wizara na Taasisi zipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI  
WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Misanga - Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika utafiti uliofanyika ilionekana kuwa, watumishi hewa husababishwa na watumishi wameajiriwa na Serikali kihalali ambao utumishi wao umekoma kutokana na kustaafu kazi, kufariki, kuacha kazi, kufukuzwa kazi na hivyo kuendelea kulipwa mishahara isiyo halali kutokana na waajiri husika kutochukua hatua za kuwaondoa kwenye *payroll* na kusababisha kuwepo kwa malipo hewa ya mishahara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2009 Ofisi yangu ilifanya uhakiki wa Rasilimali watu katika shule za Sekondari Vyuo vya Elimu, Hospitali za Serikali, Vituo vya Afya, Zahanati, Vyuo vya Afya pamoja na Hospitali binafsi na Hospitali za Mashirika ya Dini zenye watumishi wanaolipwa mshahara na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uhakika huo ilibainika kuwa Serikali ilipoteza kiasi cha Tshs.7,568,625,519 kwa kulipa watumishi hewa 2,924. Waajiri waliobainika kuwa na malipo mengi hewa ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo hili ninachukua fursa hii kuwataka waajiri wote kuhakikisha hatua zimechukuliwa dhidi ya watumishi wanaoshindwa kutekeleza dhamana zao za kuwaondoa kutoka kwenye *payroll* watumishi ambao utumishi wao umekoma.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hiyo namshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa majibu mazuri. Hata hivyo nauliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hawa watu watumishi hewa ambao wameonekana au wanajulikana waliowekwa hapa ni 2924 ni wengi sana na kwa kuwa fedha ambazo zimepokea ni shilingi bilioni 7.5 ni fedha nyingi sana fedha ambazo zingeweza kusaidia kutatua baadhi ya matatizo ya madai ya walimu na watumishi wengine ambao siku zote hapa tunawalamikia.

Je, Serikali iliachukulia hatua gani hao watumishi ambao wamesababisha haya malipo hewa yapatayo kiasi cha shilingi bilioni 7 na milioni 500?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hatua ambayo tumechukua ni kukabidhi majina ya wahusika wote katika vyombo vya ulinzi na usalama ili waweze kufanya uchunguzi kujua hizo pesa ni akina nani ambao hasa wamehusika kuzichukua. Kwa sababu baadhi yao wamefariki na wengine wamestaafu na baadhi ya maeneo hizo pesa zilikuwa zikirudishwa lakini zimekuwa zikipotea katikati kwa hiyo hadi sasa hivi vyombo vya ulinzi na usalama vinafanyia kazi suala hilo.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili suala anasema Mheshimiwa Waziri kwamba limepewa vyombo vya ulizi na usalama kuchunguza. Je, watachakua muda gani kuweza kupata matokea na Serikali itachukua hatua gani baada ya kujua kwamba nani hasa wanahusika? Ahsante. (*Makofit*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watumishi hewa wa sekta ya elimu sasa hivi tumeshaanza kupata taarifa za awali na hivyo kuanza kuweka taratibu za kuchukua hatua. Kwa upande wa wenzetu wa Wizara ya Afya kwa sababu uhakiki tumeumaliza mwaka jana na wao tuliwapa zile taarifa ili na wenyewe kwanza wajiridhishe baada ya hapo ndio tunazikabidhi vyombo vya ulinzi na usalama.

Kwa hiyo, kwa upande wa sekta ya elimu muda si mrefu tutaanza kupeleka katika mahakama na wale wanaopaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na wenyewe tutaanza. Lakini kusema *exactly* ni lini hilo siwezi kumdanganya Mheshimiwa Mbunge.

Na. 40

### **Kuporomoka kwa Utawala Bora Nchini**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miezi hii ya karibuni Taifa limeshuhudia mambo mengi mabaya katika jamii kwa mfano mikataba mibovu, wizi na ubadhifuru wa kiwango cha hatari, migomo mbalimbali na matukio ya hapa na pale na wananchi kujichukulia sheria mikononi. Na kwa kuwa kuna mifano dhahiri ya kuzidi kwa mauaji, vitendo vya ujambazi na kuongezeka kwa kero za wananchi kila pembe ya nchi.

(a) Je, Serikali haioni kwamba mambo haya yanaashiria kuporomoka kwa utawala bora katika taifa letu?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kwa kuchelewesha au kutochukua maamuzi sahihi kwa wakati kunaongeza matatizo na kuzidi kusababisha kupungua kusadikika kwa Serikali (*credibility*)?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba katika kipindi cha miaka michache iliyopita kumekuwa na matukio mengi ya uvunjaji wa sheria na taratibu zilizowekwa, matukio ya ujambazi na migomo inayochochewa na vikundi mbalimbali katika jamii. Vitendo vya wizi, ujambazi na vitendo vingine viovu ni makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi hutendwa na watu wachache wanaokiuka misingi ya maadili na sheria. Huu ni uhalifu kama uhalifu mwingine wowote. Serikali itaendelea kupambana nao kwa nguvu zake zote. Sababu ya hali hii inaweza kuwa mojawapo ya yafuatayo:-

- Athari za utandawazi zinazosababisha watu kuiga tabia na vitendo vya watu wa mataifa mengine.
- Uchu, tamaa na pupa ya utajiri wa haraka.

Aidha, kuhusu mikataba mibovu na ubadhirifu wa mali ya umma, Serikali na vyombo vyake vinaendelea kuchunguza, kufutilia na kuchukua hatua zinazostahili, kwa kuwafikisha mahakamani wale wote watakaobainika kuhusika na njia moja au nyingine na ubadhirifu wa mali ya umma au kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora hapa nchini utaendelea kuimariswa kwa Serikali kuendelea kutekeleza programu muhimu za Utawala Bora kama vile Maboresho katika uUumishi wa Umma, Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za umma, Maboresho katika Serikali za Mitaa na Maboresho katika sekta ya sheria.

Mheshimiwa Spika, juhudi za pamoja katika jamii yetu zinahitajika katika kupiga vita tabia na vitendo viovu katika jamii yetu. Waheshimiwa Wabunge wanayo nafasi muhimu ya kusaidia kwa kuwaelimisha wananchi wao kuondokana na hali hii kwa vile athari zake ni kubwa na mbaya katika maendeleo ya jamii.

(b)Mheshimiwa Spika, si kweli Serikali huchelewesha maamuzi au haitoi maamuzi sahihi na kwa wakati. Serikali ipo makini kuhakikisha kuwa uamuzi wowote unaotolewa na Serikali lazima uwe ni uamuzi ulio sahihi. Maamuzi ya Serikali hayawezi kufanywa bila kufanyiwa kazi na bila kuzingatia taarifa zilizopo mikononi mwa Serikali. Wakati mwingine inabidi utafiti au uchunguzi wa kina ufanyike kabla ya uamuzi kutolewa. Aidha, ukusanyaji taarifa, uchunguzi au utafiti wakati mwingine unahitaji muda wa kutosha ili kazi ifanyike kwa makini na kuweza kupata taarifa za uhakika na zenyte kutosheleza kabla ya uamuzi kufikiwa.

Lengo la kufanya hivyo si kuchelewesha uamuzi bali ni kuhakikisha kuwa uamuzi unaotolewa na Serikali unakuwa ni sahihi, unaozingatia sheria, haki na maslahi ya taifa.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nashukuru majibu hayo japo kwa kiwango kikubwa nayaona ni ya nadharia kuliko vitendo. Si suala la kujadiliana lakini ningependa kutoa wazo langu kwamba pengine wakati umefika kwa sababu majibu haya yanakubali hoja yangu kwamba kweli kuna matatizo pengine njia bora ni kutazama uwezekano wa kutazama suala hili kwa makini zaidi pengine tuwe na tume ya kitaifa itakayo zamia suala hili zima la maadili linaloongeza maovu tuwe na wataalam wa saikolojia na wataalam wengine waweze kutuelekeza nchi iende wapi?

Pili zamani tulikuwa na tabia ya viongozi kukemea nchi na watu wakasikia kama kuna tatizo linalopotosha Utawala Bora, sasa hii naona hakuna. Je, Waziri anaweza akatupa maelezo kwanini isifanyike sasa ili kusudi tuepushe yale mambo ambayo yanavuruga nchi kiasi kwamba sasa hivi kila mtu ukimuuliza anasema nchi inaporomoka? Ahsante sana?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante maswali ya nyongeza yamekuwa marefu hayo. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, wewe jibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ametoa ushauri akiwa kama mstaafu katika Serikali. Kwa hiyo, anaelewa vizuri mambo ya *governance* tunapokea vizuri ushauri wake na utaangaliwa kama unafaa lakini naamini kuna vyombo vingi ambavyo vinahusiana na masuala ya maadili, tunapokea ushauri wake tukizingatia uzoefu wake katika Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Galinoma anazungumzia kwamba Serikali haikemei, mimi ningependa kutofautiana naye kwa sababu mambo mengi ambayo yamekuwa yakiendelea ndani ya Serikali yetu yanaashiria kukemea na kwamba vyombo vyote sasa hivi vinafanya kazi kwa uadilifu sana na kwa juhudu kubwa ukiangalia Jeshi la Polisi limejipanga vizuri PCCB imejipenga vizuri Serikali imeiwezesha sasa hivi *PCCB* ina ofisi katika kila wilaya na kadhalika. Lakini tukubaliane kwamba tunapozungumzia kukemea tunafuata pia utaratibu wa sheria uliopo pamoa na Katiba inavyotuelekeza. Kwa hiyo, masuala ya kukemea ni kweli sisi kama Wabunge tunastahili pia tukemee lakini tunaendesha utawala wa sheria. Kwa hiyo, kutokana na Utawala wa Sheria kila mmoja anatakiwa atekelze wajibu wake kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoa na majibu ya Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kuwa Serikali iko makini sana katika kukemea mambo kama haya sasa kama hivyo ndivyo kwanini katika miaka ya hivi karibuni Shirika kama la Reli limeachiwa *Rites* wameliumiza, *TANESCO* wameachiwa *Net Group*, *ATCL* limeachiwa *South Africa Air Ways* wameumiza. Kama Serikali inafanya uchunguzi katika mambo kama haya inakuwaje mambo haya yanatokea na kuliumiza sana Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Yaani kama hayo inatakiwa ikemee kweli? Haya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu kwamba mambo ambayo yametokea hasa katika mikataba ni masuala ambayo yameletwa pamoa katika utaratibu wa mabadiliko ya kisera ambayo tunayo.

Kwa hiyo, wakati wa kuingia katika mikataba hii uwezo wetu wote tunakubali wakati wakuingia mikataba kulikuwa na matatizo na Serikali imeahidi kuipitia mikataba hii na ndio maana yametokea matatizo haya. Sisi wote Wabunge tumekubali na tumekiri

kwamba ipo haja ya kuwapa uwezo mkubwa zaidi watendaji wetu waelewe jinsi ya kuingia katika mikataba hii.

Na. 41

**Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Kahawa**

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni nia ya Serikali kuwa ifikapo mwaka 2010 nchi iweze kuzalisha si chini ya tani 120,000 za kahawa kwa mwaka.

- (a) Je, ni mikakati gani inayoendelea ya kuongeza miche bora ya kahawa?
- (b) Je, ni mikakati gani iliyopo ya kuongeza watalaam wa kilimo (*extension officiers*)?
- (c) Je, Serikali inaweka mikakati gani kushawishi uanzishwaji wa *central pulparyies*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na wadau wa zao la kahawa nchini inatekeleza mpango wa kuendeleza zao la kahawa kama sehemu ya utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (*ASDP*). Kupitia mpango huo, Serikali inashirikiana na Halmashauri za Wilaya katika maeneo yote yanayozalisha kahawa nchini, kuzalisha miche bora ya kahawa yenye ukinzani dhidi ya magonjwa ya kawa aina ya chule buni na kutu ya majani. Ili kuhakikisha uzalishaji wa miche hiyo kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwenye taasisi ya utafiti wa kahawa (*TACRI*) kwa ajili ya kuiwezesha ishirikiane na Halmashauri zinazozalisha zao la kahawa kuzalisha kwa wingi miche bora ya kahawa na kuwauzia wakulima kwa bei nafuu. Hadi kufkikia mwaka 2008/2009 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 1.1 ambazo zilitumika kuzalisha jumla ya miche milioni 15 ambayo imesambazwa kwa wakulima. Aidha, katika msimu huu wa 2009/2010 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya kahawa milioni 15.

(b) Kupitia program ya kuendeleza sekta ya Kilimo (*ASDP*) kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali inatekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani nchini. Lengo la mpango huu ni kuajiri watalaam wa ugani 11,703 ili kuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na mtaalam mmoja wa ugani wa kilimo katika ngazi zote mpaka kwenye

tarafa. Hivi sasa wapo jumla ya watalaan 4,400 na watalaan wengine 3,000 wapo katika ngazi mbalimbali za mafunzo katika vyuo vya mafunzo katika ngazi ya Stashahada na Shahada. Baadhi ya wataalam hao wamepangia kufanya kazi katika maeneo yanayozalisha kahawa.

(c) Kuanzia miaka ya 1990 Serikali ikishirikiana na wadau wa kahawa nchini hususan Halmashauri ya Wilaya, vyama vya ushirika pamoja na vikundi vya wakulima na sekta binafsi, imekuwa ikihimiza ujenzi na matumizi ya vituo vya kubangulia kahawa.

Lengo kuu la ujenzi na matumizi ya vituo hivyo ni kuongeza ubora wa kahawa inayozalishwa ili kupata bei bora katika soko la dunia hivyo kumwongezea mkulima kipato. Hadi msimu huu wa 2009/2010 jumla ya vituo vya kubangulia kahawa 250 vimejengwa nchini kwa matumizi ya wakulima wadogo wadogo ikilinganishwa na vituo 40 vilivyokuwepo mwanzoni mwa mwaka 2000. Ujenzi wa vituo hivyo unaendelea kwa kuwa wananchi wamehamasika kuvitumia baada ya kuona faida na mapato ya matumizi ya vituo hivyo.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuwapongeza sana wale wananchi wa Wilaya ya Hai ambao wameitikia wito wa kuanzisha hizi bustani za miche bora ya kahawa na pia taasisi yetu ya *TACRI*. Kwa kuwa utaratibu wa taasisi yetu ya *TACRI* ya kuwasaidia walimu wakulima wenzao imeonyesha jitihada kubwa na mafanikio mazuri sana kwa mfano kumtumia Ndugu Gerald Mussa, ambaye amekuwa akisaidia zaidi ya Kata moja.

(a)Je, sasa Serikali itaweza kusaidia taasisi hii ya *TACRI* ili kuwapatia vyombo vya usafiri hawa wakulima ambao wameshakuwa walimu kwenda kuwafundisha wenzao katika kulima zao la kahawa?

(b)Nakubaliana na Serikali katika mpango wake mzima mzima wa kuwa na mtaalam wa ugani katika kila kijiji.

Je, sasa Serikali ina mipango/mikakati gani ya kuhakikisha hawa wataalam wa ugani katika kijiji wanaishi katika kijiji husika badala ya kukaa vijiji vilivyoko mbali na kile kijiji alichopangiwa?

**NAIBU WA WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kuwa zao la kahawa lina faida kubwa kwenye Halmashauri ambazo zinahusika, ninashauri Halmashauri hizi ziweze kutumia fedha za *DADPs* ili waweze kuwapatia usafiri walimu hawa katika maeneo hayo ya bustani za miche ya kahawa. Kwa sasa hivi hela tunayotoa kule *TACRI* ni kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya kahawa.

Swali lake la pili kwamba watalaan wa ugani wawewe kukaa maeneo hayo ndiyo lengo letu hasa kwa watalaan wa ugani wale wanaopangiwa kwenye vijiji na kwenye Kata wakae kwenye maeneo yale na wawezeshwe kwa kutumia fedha za *DADPs* kujenga nyumba pamoja na kupatiwa usafiri ili wawe na mazingira mazuri ya kufanya kazi.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu uzalishaji kufikia tani laki moja na ishirini na kwa vile ili tuweze kufikia hapo inatupasa pia kutunza ile miche ambayo inazaa sasa na kwa vile katika Kata za Mkumbi, Ukata, Linda, Kitula, Litembo kule Mbanga kahawa hiyo imeingiliwa na wadudu na tatizo hili linaendelea kusambaa katika Kata zingine. Serikali inachukua hatua gani za haraka kusaidia na Halmashauri ya Wilaya ili kumaliza tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia kwamba nitatuma wataalam wa kwenda wilayani kwake kwa kusaidiana na viongozi wa Halmashauri ili waweze kufanya utafiti na kujua wadudu hao wanaweza kuangamizwa namna gani.

**MHE. BASILI PESAMBILI MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba hivyo vyanzo vya fedha za kuhudumia zao hili *DADPs* kama alivyotaja na vyanzo vingine vya kiserikali ni vidogo mno kuweza kufikia malengo ya hizo tani 120, 000. Kwa hiyo inahitajika programu maalum operesheni maalum hasa ya kuongeza miche na mashine hizo ndogo ndogo za kukoboa kahawa ngazi ya vijiji. Je, anakubali kwamba ni fedha maalum zinahitaji kwa kazi hizo mbili ili kuweza kuongeza uzalishaji na mapato kwa mkulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na yeYe kwamba fedha zinazotengwa ni kidogo lakini zinatengwa kutokana uwezo wa Bajeti ya Serikali na nipende kumjulisha kwamba Serikali inahudumia mazao mengi yakiwemo mazao ya chai pia tunapeleka miche, tunahudumia mazao ya korosho pamoja na pamba pamoja na mazao ya chakula kama mahindi. Kwa hiyo, uwezo wa Serikali pale tunapokuwa na uwezo zaidi tunawenza tukaongeza fedha kwa ajili ya miche na kwa ajili ya mashine hizo kwa ajili ya kubangulia kahawa.

Nadhani tunakubaliana kwamba tangu tuanze kutoa miche hii miaka mitatu iliyopita ilikuwa ni michache kuliko sasa hivi. Kwa hiyo, tutaendelea kuongeza kutokana na uwezo wa Serikali.

Na. 42

### **Kuendeleza Kilimo cha Chai Ludewa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ludewa inachipukia katika kilimo cha chai:-

- (a) Je, kwa nini wilaya hiyo haikupewa chochote katika mgao wa fedha za *DADPs* kwa mwaka 2007/2008 - 2008/2009?

- (b) Je, kuna mpango gani kabambe wa kuendeleza zao hilo wilayani Ludewa ikiwa ni pamoja na kuwekewa kiwanda cha chai hivi karibuni?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Raphaele Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara za sekta ya Kilimo kupitia Mipango ya Maendelo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans (DADPs)*) zilianza kutekeleza sera na kupeleka madaraka karibu na wananchi mwaka 2006/2007. Timu ya Taifa ya wawezeshaji imekuwa ikiwezesha timu za uwezeshaji za Wilaya na Kata namna ya kuwezesha walengwa kupitia mpango shirikishi kuibua miradi kulingana na fursa za uchumi na vikwazo vilivyopo kijijini. Kutokana na utaratibu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009, ilitengewa jumla ya shilingi 45,613,693 kwa ajili ya kuendeleza zao la chai kupitia ruzuku za *DADPs*. Aidha, katika mwaka 2009/2010, wilaya ya Ludewa imetenga shilingi 22,304,176 za *DADPs* kwa ajili ya kuendeleza zao hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kiwanda cha chai katika kuendeleza kilimo cha chai. Ili kuendesha kiwanda cha chai kwa faida. Zinahitajika hekta 500 zilizopandwa chai.

Tathimini iliyofanywa na Bodi ya Chai Tanzania ilibaini kuwa mashamba ya chai ya wakulima wadogo Ludewa yana hekta 13 tu. Hata hivyo, kwa sasa soko la majani mabichi yanayozalisha siyo tatizo kwani kiwanda cha chai cha Luponde kinapokea na kusindika majani yao.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inaendelea kuviwezesha vikundi vya wakulima kwa kuvipatia ruzuku ya miche bora ya chai ili viweze kupanua mashamba hayo. Lengo ni kuzalisha angalau miche 6,000,000 ifikapo mwaka 2013, kiasi ambacho kitawezesha kuwa na hekta 500 zilizopandwa chai ifikapo mwaka huo. Tangu kuanza kwa mpango wa kuwezesha vikundi vya wakulima kuzalisha miche bora ya chai, miche 1,970,000 imezalishwa Ludewa.

Aidha, kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kati ya mwaka 2007/2008 na mwaka 2008/2009 vikundi vya wakulima katika vijiji vya Mfalasi, Madilu, Manga, Mangalanyene, Ilawa, Luvuyo na Madope vilizalisha miche 752,000 kwa ajili ya kuendeleza zao la chai Wilayani Ludewa.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri na nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wangu kwa kuweka msisitizo mkubwa katika zao la chai. Sasa maswali mawili mafupi ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa uzoefu wa Wanaluudewa katika kilimo cha chai ni mdogo ndiyo kwanza wanaanza, Wizara au Serikali itawasaidiaje wananchi wa Ludewa kupata uzoefu au elimu ya nadharia na vitendo ili waweze kwenda na wao na kasi inayotakiwa katika kilimo cha chai?

(b) Uzoefu wangu kuhusu viwanda nikijifunza kutoka Kilolo na Wialaya ya karibu Njombe ambako wananchi wa Lupembe ambao kiwanda chao hakifanyi kazi majani ya wananchi yanamwagwa ina maana kwamba kuna umuhimu wa kuwa na kiwanda chetu sisi wenyewe na kwa kuwa mchakato wa kupata kiwanda inachukua muda mrefu sana, Mheshimiwa Waziri ni utaratibu upi mtautumia Serikali kuhakikisha kwamba sasa mnaanza kushirikiana na wananchi kwenda kuibua, kutafuta maeneo yanayoyofaa kuwekwa kiwanda kwa kuzingatia kwamba lazima kuwe na msitu utakaopandwa kwa ajili ya kuni na kwa ajili ya kiwanda kitakacho jengwa?

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya Profesa Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza linahusu elimu. Kama nilivyozungumza kwamba sasa tuko kwenye programu ya kuzalisha maofisa ugani ambao watakwendwa vijijini. Lakini napenda kuiomba Halmashauri ya Ludewa kwa kutumia fedha hizo hizo ambazo tunazitoa kwa ajili ya kuendeleza yaani kwa maana ya DADPS waweze kuanzisha mashamba darasa kwa kutumia wataalam waliopo waanzishe mashamba darasa ya chai ili waweze kuwafundisha vizuri wakulima wale jinsi bora ya kulima chai katika eneo hilo ili hatimaye waweze kuwa na mashamba makubwa na yenye chai yenye ubora unaotakiwa.

(b) Kama nilivyosema hapo awali. Kujenga kiwanda kinahitaji hekta mia tano sasa hivi Ludewa wana heka kumi na tano, kwa hiyo kitu cha kwanza tuongeze uzalishaji wa zao hili ili tuweze kuwa na uwezo wa kujenga kiwanda, kwa sababu ukijenga kiwanda wakati uzalishaji ni mdogo ni hasara.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa leo katika soko la ulmwengu, mazao yote ambayo ni *organic*, ambayo yanatumia mbolea asilia yana bei kubwa kuliko mazao yanayotumia mbolea ya kutengenezwa viwandani. Je, Waziri anaweza kuniambia wana mpango gani wa kuongeza ukuzaji wa Kilimo cha kahawa na kilimo cha chai kwa kutumia mbolea asilia ili nchi hii iweze kufaidika zaidi kwa bei ya bidhaa na vitu vilivylimwa kwa mbolea asilia?

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nina heshima ya kujibu swali la Mheshimiwa Malecela, kama ifuatavyo:-

Kwanza nikubaliane na yeze kabisa kwamba mazao ambayo ni *organic* yana bei nzuri duniani kuliko yale ambayo yamezalishwa kwa mbolea yani *chemical fertilisers*. Kwa hiyo, ningeweza kukubalina naye kwamba wazo lake ni zuri na kwamba Serikali tuna hamasisha utumiaji wa mbolea hii. Lakini mipango inaendelea kufanywa kutokana na uwezo wa kiserikali wa Bajeti kuhusiana na uzalishaji wa mbolea na ukusanyaji wa mboji na utengenezaji, lakini japo niseme kwamba, mbolea hii ya *organic, nutrients* au viini/madini yaliyoko pale ni madogo sana ukilinganisha na mbolea hii inayotengenezwa na viwanda, ndio maana mara nyingi wananchi wanatumia maeneo mengi hata ukizungumzia uzalishaji wa chakula, tunatumia mbolea ile ya viwandani kwa sababu madini yake ni mengi na uzalishaji wake ni mkubwa zaidi kuliko ile ya *organic*.tutaendelea kufuata ushauri wake Mheshimiwa Malecela na tuangalie kwamba tunaweza tukafikia wapi.

Na. 43

### **Serikali Kutoa Mafunzo ya *Epicor Package* kwa Wahasibu**

**MHE. MGANA IZUMBE MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha utaratibu kwa Wizara na Halmashauri zote kutumia Mfumo wa Kihasibu uitwao *Integrated Financial Management Systems (IFMS)* na kwa kuwa jukumu la Wizara ya Fedha na Uchumi kuhakikisha kuwa inatoa mafunzo ya *Epicor Package* kwa wahasibu wote:-

Je, ni Wizara ya Fedha na Uchumi inatoa mafunzo hayo kwa Wahasibu wa Halmashauri zote ambazo hazijaanza kutumia mfumo huo kwa sababu ya kukosa wataalam?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi ,naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya fedha na Uchumi inaendesha na kusimamia mfumo wa kimtandao wa kifedha na kihasibu wa kupokea fedha na kufanya malipo ya Serikali (*Intergrated Financial Management System*).

Mfumo huu hutumika pia kuandaa malipo, kutunza kumbukumbu za fedha za Serikali na kuandaa na kutoa taarifa za fedha za mwaka na taarifa nyingine mbalimbali. Mtandao huu hutumia mfumo wa *computer uitwao Epicor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza wajibu huu Wizara ya fedha na Uchumi imekuwa ikiendesha na kugharamia mafunzo Serikalini kwa wahasibu, wakaguzi

wa ndani na wakaguzi kutoka ofisi ya mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili kuwezesha kuendesha na kusimamia mfumo huu wa kifedha na kihasibu kwa ufanisi. Mpaka sasa wanaotumia mtandao huo ni pamoja na Wizara zote za Serikali, Sekretariati zote za Mkoa, Hazina Ndogo zote na Idara za Serikali zinazojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Halmashauri 86 zimekwisha unganishwa kwenye mtandao wa mfumo huu baada ya mafunzo kwa wataalamu husika wa Halmashauri. Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuunganisha Halmashauri zote nchini kwenye mtandao, Halmashauri 36 zilizobaki zitawekwa kwenye mfumo wa mtandao huu wa kifedha na kihasibu mapema iwezekanavyo baada ya mafunzo kwa wahasibu na wataalam wengine wa Halmashauri hizi, kumalizika kufanyika kwa tathmini na matayarisho mengine husika kukamilika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Nimeridhika na majibu ya Serikali, lakini je, anavyosema ni mapema iwezekanavyo zile fedha zipo kwenye Bajeti hii?

(b) Kwa kuwa huu mfumo wa *Epicor* ni mzuri sana na umefaidisha Wilaya yangu ya Iramba na bado hizi Halmashauri zingine zinapata hoja kutoka kwa CAG, Serikali iko tayari kuharakisha kuwasomesha hawa na baada ya kuwasomesha wasiwe wanawahamisha kabla hawajatoa huduma kwenye Wilaya walikotoka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Maswali ya Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, kama ifuatavyo:-

(a) Ndiyo, fedha zimetengwa kwa ajili ya kazi hii, lakini naomba nitadhazarishe kwamba Halmashauri zilizobakia kama nilivyosema ni 36 na haiwezekani zote zikakamilika ndani ya mwaka mmoja. Tunatarajia sasa kwamba kazi hii kumalizika itachukua kati ya miaka mitatu na minne na baada hapo tutakuwa sasa tumeshakamilisha kuunganisha Halmashauri zote nchini 132 kwenye mtandao huu.

Ni kweli mara nydingine wahasibu baada ya kuwasomesha na kuwapitisha kwenye mafunzo wanahamishwa lakini ni chini ya utaratibu tu wa kawaida tu wa utumishi, tutakachofanya ni kwamba tutajitahidi iwezekanavyo pale ambako tumeshampa mafunzo mhasibu basi anabakia pale mpaka tumalize programu hii basi tatizo hili halitakuwepo tena.

Na. 44

**Haki za Watoto Wanaozaliwa Nje ya Ndoa Kisheria**

**MHE.DIANA M. CHILOLO(K.n.y. MHE. DR. GETRUDE RWAKATARE)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kuwa rafiki wa nje ya ndoa mke/mume wa siri; na kwa kuwa wengine huzaa hata watoto ila hawatambuliki kisheria:-

Je, ni zipi haki za watoto hao pale baba zao wanapofariki?  
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum. Kabla ya kujibu swalii kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kisheria sio sahihi kusema rafiki wa nje ya ndoa ni mume au mke wa siri. Maneno mke au mume hutumika pale ambapo uhusiano wa wawili hao unatambulika na sheria husika kama ndoa ama ya kimila, kidini au kiserikali. Pia tunazo sheria kadhaa mahususi kwa mfano sheria ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa, sura ya 278 yaani *The Afiliation Ordinance Chapter 278* ya sheria zetu zinazo shughulikia matunzo ya watoto kama hawa ingawa kwa masharti kadhaa. Hata hivyo sheria hii itakoma kutumika mara sheria ya mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 iliyopitishwa na Bunge hili itakapoanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa watoto wanaozaliwa nje ya ndoa wanapata matatizo mengi hususan yale yanayohusiana na urithi. Matatizo haya husababishwa na sababu kadhaa zikiwemo za kidini na pia baadhi ya mila na desturi mbalimbali zilizopo katika jamii zetu ambazo huwatenga watoto hawa na kuwaacha wakiwa hawana haki yejote ya kuwarithi wazazi wao wanapofariki. Changamoto hii ni mionganii mwa hoja ambazo zimeifanya Serikali itake kutunga sheria ya mirathi ambayo itashughulikia, pamoja na masuala mengine, watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Hata hivyo kutohana na unyeti wa masuala ya ndoa na mirathi, hasa ukizingatia kwamba masuala haya yanagusa hisia za wananchi katika imani, mila na desturi zao Serikali imepanga kukusanya kwanza maoni ya wananchi ili hatimaye kupata sheria bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa busara zao wananchi watatoa maoni mazuri juu ya ndoa na mirathi yatakayowezesha kutatua tatizo hili la watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Kwa sasa sheria ya mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ambayo tulishapitisha katika Bunge hili Tukufu mwezi Novemba, 2009 (mwaka jana) ni chanzo cha kutambua haki za watoto wakiwemo hawa waliozaliwa nje ya ndoa. Pamoja na mambo mengine, sheria hii mpya imepiga marufuku ubaguzi dhidi ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare, kama ifuatavyo:-

Kimsingi hakuna sheria mahususi inayotoa haki kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa pindi baba zao wanapofariki, ila zipo baadhi ya mila na desturi huruhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kurithi pale watoto hao wanapokuwa wametambulishwa rasmi katika familia na wazazi wao kabla hawajafariki dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hususan Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare, wakati wa kutoa maoni utakapowadia tushiriki kikamilifu ili kuziboresha sheria hizi za ndoa na mirathi ili ziweze kukidhi mahitaji yetu ya sasa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu yake mazuri nina swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa wako akina mama ambao wamezaa nje ya ndoa, wanashindwa hata kuwataja wanaume waliozaa nao ili angalau hata ile sheria ya kimila iweze kuchukua nafasi yake, hatimaye watoto hao, hao wazazi wanapofariki, inashindikana kabisa kupata msaada wowote. Ama wakati mwagine kuogopa kwa kukatazwa na mwanaume huyo kwa kuwa tu anaona aibu kwa jamii kwamba amezaa na fulani. Je, Serikali itasaidia vipi akina mama hawa ili wapate ujasiri wa kueleza ukweli ili watoto hawa waweze kupata msaada kutokana na sheria hii mpya ambayo tayari tunategemea itatumika mapema na katika sheria za mila pia?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali rahisi la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni wajibu wa binaadamu wote, wanawake kwa wanaume kufahamu athari zinazotokana na matendo yao ya zinaa. Na ni wajibu wa sisi Watanzania kuwaelimisha wasichana na watoto wetu wa kiume kuwa Watanzania wanaotii sheria na maadili ya Kitanzania. Kwa wale ambao wanaficha watu waliowapa ujauzito, sasa nafikiri sasa Serikali ifanye nini hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwaomba Watanzania, hasa vijana wa kike na wa kiume kujua wajibu wao katika jamii. (*Makofi*)

Na. 45

**Washitakiwa Kucheleweshewa Nakala za Hukumu  
Wanapotaka Kukata Rufaa**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA (K.n.y. MHE. RAMADHANI A. MANENO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo wananchi waliofungwa ambao wengi wao wamedhamiria kukata rufaa na kwa kuwa, lipo tatizo sugu la kutopatikana kwa nakala za hukumu na mahakama husingizia ukosefu wa vitendea kazi:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba mtu akiwa gerezani hukosa haki yake ya msingi?
- (b) Je, Serikali inawajibika vipi kwa watu wanaopata nakala za hukumu zao tayari wameshamaliza kutumikia vifungo vyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) aijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri ya Katiba na Sheria, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ramadhani Maneno kama ifuatavyo. Kabla sijajibu swalii hilo naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mahakama haisingizii ukosefu wa vitendea kazi kuwa ni sababu ya kuchelewesha utoaji wa nakala za hukumu. Ukweli ni kwamba Mahakama zetu nyingi zinakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi na watumishi hasa wapiga chapa, hali inayoathiri utendaji kazi ikiwemo utoaji wa nakala za hukumu kwa wakati.

Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya watumishi na vitendea kazi kwa kadri uwezo wa fedha unavyoruhusu na kama ambavyo Bunge hili linatoa fedha kwa Mahakama.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliopita 2008/2009 jumla ya Makatibu Mahususi 19 ambao hupiga chapa walajiriwa na kusambazwa sehemu mbalimbali. Aidha, jumla ya Makatibu Mahususi wengine 25 wamepatikana baada ya usaili na taratibu za kuwasambaza sehemu mbalimbali zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Ramadhani Maneno, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua kuwa mtu akiwa gerezani bila sababu ya msingi anakosa haki yake. Iteleweke pia kwamba Serikali haikusudii kumnyima haki raia wake ye yote kwa hali yoyote ile. Ila kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje ya uwezo wa Serikali zikiwemo nilizotaja hapo juu hali hii kutokea.

(b) Sio lengo la Serikali kuchelewesha utoaji wa nakala za hukumu ili wakate rufaa, hata hivyo, itakuwa sio busara kwa Serikali kuwajibika pale mtu anapomaliza muda wake wa adhabu bila kupata nakala ya hukumu. Hata hivyo mtu huyo atakuwa amepelekwa gerazani kwa amri halali ya Mahakama. Aidha mtu aliemaliza kifungo chake anawenza bado kuendelea na rufaa yake ili kusafisha jina lake kama ataona inafaa.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Jaji Werema kwa majibu yake mazuri, lakini ningependa kujua ni raia wangapi wa Tanzania mpaka sasa wamepatwa na mikasa hii kwa kucheleweshewa haki zao?

**NAIBU SPIKA:** Unategemea kupata hesabu kabisa? Mheshimiwa AG, labda hesabu unayo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa sina takwimu za hakika, lakini nafahamu kwamba wapo baadhi ya Watanzania wenzetu ambao rufaa zao zinaitwa wakati wamekwisha tumikia muda wake wa kifungo umekwisha. Isipokuwa kama mtu alie tumikia kifungo anaona kwamba alionewa, kama nilivyosema anaweza kuendelea na rufaa. Sasa yako mambo mawili yanaweza kutokea. Inawezekana kile kifungu alichopewa pengine kilikuwa tahafif, kilikuwa kidogo na Mahakama ya juu ina uwezo wa kuongeza kifungo hicho. Kwa hiyo, anaweza kuongezewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama alionewa anayo mamlaka, anayo haki ya kuanzisha kesi ya madai kwa yule mtu ambaye alisababisha yeze kushitakiwa.

Kama huyo mtu alifanya hivyo kwa makusudi, kwa kumkomoa. Lakini pia ni lazima ahakikishe/ asibitishe kwamba huyo mtu alifanya hivyo kwa ajili ya kumkomoa, la sivyo *public interest* ni kuzuia kosa la jinai.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kutokujua sheria hakumzuii alietenda kosa kutiwa hatiani na kwa kuwa wako watu ambao wametiwa hatiana baadaye wakakata rufaa na wakaonekana hawana hatia wakafutiwa kesi.

Lakini mtu yule ameshatumikia kifungo pengine mwaka mmoja na kitu na kwa kuwa baada ya adhabu aliyoipata anashindwa yeze kufungua kesi kwa kuwa kaonewa. Je, Serikali inasema nini katika watu kama hawa ambao wameonewa na hawana fidia wanayoipata?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifutavyo:-

Nafikiri tunaweka wajibu mwangi sana Serikalini. Hakuna haki bila waajibu na nadhani huyo mtu ambaye amepata hiyo athari anaweza kuchukua hatua nyingine kwa

kutaka hizo haki zake kwa njia ya madai na Serikali haina ambacho inaweza kufanya kwa sababu Serikali ina tekeleza sheria zilizopo. Labda kama Bunge hili litatunga sheria kwa ajili hiyo, lakini mpaka sasa hakuna sheria ya kulipa hizo athari.

Na. 46

### **Kukuza Michezo ya Riadha Kwa Vijana**

**MHE. MAULIDAH A. KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali haitilii maanani sana mchezo wa riadha (kukimbia) kama inavyofanya kwenye mchezo wa mpira wa miguu, na kwa kuwa Tanzania ina hazina kubwa ya vijana wanaoweza kuitangaza nchi kuititia riadha.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukuza vijana wadogo mashulenii hususan Mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma, Singida na mingine kwa kuanzia ili waweze kuitangaza nchi yetu kama wenzetu wa Kenya?

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mbunge wa Viti Maalum, kamaifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba sio kweli kuwa Serikali haitilii maanani sana mchezo wa riadha kama ilivyo kwa mpira wa miguu. Serikali inatambua na kuthamini michezo yote ukiwemo mchezo wa riadha.

Mikakati ya Wizara ni pamoja na kuwa na mpango endelevu wa maendeleo ya mchezo wa riadha. Tayari chama cha riadha nchini kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki hapa nchini wameandaa mpango mkakati wa kuendeleza mchezo wa riadha kwa kuzingatia mahitaji yote yanayoweza kuendeleza mchezo huo ikiwa ni pamoja na kuwa na makocha bora, mafunzo kwa makocha wazalendo, viwanja vyenye viwango vya kimataifa, vifaa na kuandaa mashindano mbalimbali ndani ya nchi yetu.

Kurejeshwa kwa mashindano ya shule za Msingi, Sekondari na Vyuo na ujio wa walimu wawili wa michezo wa riadha kutoka Cuba ambao ni Andres Baro Curtis na Jorge Luis Bravo Rojas kutaimarisha na kuendeleza mchezo wa riadha hapa nchini.

Walimu hawa wameanza kutembelea mikoa mbalimbali nchini na kufanya mazungumzo na viongozi wa mchezo wa riadha kuona jinsi watakavyoshirikiana nao katika kuibua vipaji na kuviendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi juni mwaka 2007, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumanu imemleta mtaalam wa mchezo wa riadha Bwana Peter Thumm Hans ambaye jukumu lake kubwa ni kuandaa na kuendeleza programu mbalimbali za mafunzo na utambuzi wa vipaji vya mchezo wa riadha.

Tangu awasili tayari ameendeha mafunzo na walimu wa shule za msingi, sekondari na madaktari wa michezo katika mikoa ya Morogoro, Arusha, Mbeya, Songea, Dar es Salaam na Unguja na anaendelea na Mikoa mingine. Jumla ya washiriki 359 wamepata mafunzo hayo kama ifuatavyo:-

- o Morogoro washiriki 36;
- o Arusha washiriki 18;
- o Mbeya washiriki 28;
- o Songea washiriki 30; na
- o Unguja washiriki 70 (Awamu 2).

Aidha, chama cha riadha nchini kinaandaa mashindano mbalimbali ya KItaifa kwa mchezo wa riadha kwa lengo la kuibua vipaji vipyta na pia kuendeleza mchezo wa riadha.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambapo pia naomba vitendo viendane na majibu yenye. Nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali yenye imekubali kwamba inatoa mafunzo kwa makocha wetu wazalendo. Je imejizatiti kisawasawa ili tutokane na hawa walimu wageni ambao tunawalipa hela nyingi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwamba hatuzungumzii nadharia, nazungumzia vitendo na mafunzo yanafanyika, maana yake namhakikishia kwamba hatuzungumzi nadharia. Tunazungumzia vitendo, maana yake namhakikishia kabisa *with program* ambayo imeandaliwa, ni program ambayo inafanyika na nimeshatoa mfano kwamba makocha hawa waliokuja licha ya kufundisha wachezaji lakini pia wanaandaa kufundisha makocha wazalendo ili waweze kupata uwezo wa kufundisha vizuri riadha. Lakini kubwa zaidi pia na sisi tunapeleka makocha kwenye vyuo vyetu kama Lapisu Ujerumanu na maeneo mengine Hungary ili wazalendo nao waweze kupata mafunzo ya kufundisha riadha katika nchi yetu.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda tu nimwulize. Je, Serikali haioni kwamba kwa kuweka utaratibu wa kuwashindanisha vijana wenyе vipaji katika kila Mkoa kama inavyotokea katika nchi zilizoendelea kwa mfano *American Idol* au *Ex-Factor* ya Uingereza au kama *Maisha Plus* yanavyoshindanisha wasanii na kuwaweka katika kambi moja ili kuweza kupata wale wenyе vijapaji na kuinua vipaji vyao? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtoe wasiwasi nimeshamjibu kwenye swalı la msingi kwamba Chama cha Riadha Tanzania kina kalenda. Katika kalenda hiyo kuna mashindano mbalimbali yanayofanyika kila mwaka, tena kwa umri tofauti, kuna *youth* kuna *junior* kuna *senior*. Kwa hiyo asiwe na wasiwasi, mashindano hayo ya Chama cha Riada kinashindanisha ili kuweza kutambua vipaji vyenye umri tofauti tofauti ili angalau wakimbie kwa mbio inayohusikana na umri wake. Chama cha Riadha kinafanya hivyo na sisi Serikali tunasimamia kwa karibu.

Na. 47

### **Kujenga Vyuo vya Michezo na Kuendeleza Vijana kimichezo**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo vijana wengi hapa nchini wenyе vipaji vya michezo mbalimbali; na kwa kuwa kituo cha michezo cha Malya hakitoshelezi mahitaji ya nchi nzima:-

- Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, kati na muda mrefu wa kujenga vyuo vya michezo?
- Je, Serikai ina “*data bank*” ya vijana nchini wenyе vipaji vya michezo?

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikalai inayo mipango mbalimbali itakayowezesha kuibua na kuendeleza vipaji vya wanamichezo mbalimbali hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuwa na vyuo bora vya michezo vitakavyotosheleza mahitaji yanayolingana na michezo mbalimbali ambayo inachezwa hapa nchini.

Katika mipango ya muda mfupi, Serikali inaendelea kuboresha vituo vya michezo vya Songea na Arusha ili viwe na uwezo wa kutoa kozi fupi kwa michezo

mbalimbali. Aidha, Serikali pia inaendelea kuhamasisha wadau mbalimbali wa michezo ili waweze kuanzisha vyuo au mafunzo katika kuendeleza taaluma za fani ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya muda wa kati na mrefu Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo cha Malya ili kiweze kuhudumia wanachuo wengi zaidi kwa pamoja. Aidha Serikali inakusudia kukifanya chuo hicho kiwe kinatoa mafunzo ya shahada. Sasa hivi kinatoa stashahada. Taratibu za kutoa mafunzo katika ngazi hiyo zinafanywa kwa kushirikiana na *NECTA*. Vile vile, Serikali inakusudia kujenga vyuo vingine vya michezo kikanda hapa nchini kutegemea na Bajeti yake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo “*data bank*” ya vijana wenye vipaji katika michezo mbalimbali hapa nchini. Kila chama cha michezo husika kitaifa inayo “*data bank*” yake. Hapa nikimaanisha, kwa mfano mpira wa miguu, riadha, *basketball*, *netball* na kadhalika, wanazo “*data bank*” za vijana na vipaji mbalimbali.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nilitaka nifahamu kwamba kwa kuwa suala la michezo ni suala mtambuka *cross cutting*, kwa maana kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo inatakiwa kushirikiana pamoja na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Elimu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi, sasa nilitaka nifahamu. Je, Wizara hii imejipangaje kushirikiana na Wizara zingine kuhakikisha kwamba michezo inaboreshw na inakua?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amejibu kwamba Serikali inayo *data bank* ya wachezaji wetu tulionao. Lakini kwa masikitiko hakuweza kutaja wachezaji wetu wako wapi. Ningependa alieleze Bunge hili Tukufu wachezaji wetu wako wapi, wa michezo gani ili pale tunapohitaji katika timu zetu za Taifa tuweze kuwaita watumikie taifa letu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Blandes kwa maswali yake. Nampongeza kwa sababu ni maswali mazuri hasa kwa kutambua kwamba michezo ni mtambuka na Wizara zote zinahusika, hasa hizo Wizara ambazo amezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu mimi ni Wizara ambayo ni ya kitaalam zaidi maana sisi ndiyo tunatoa makocha. Lakini michezo iko kwenye Wizara ya Elimu ambako ndiko kwenye watu, kuna watoto, michezo iko kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, ndiyo kuna Polisi, kuna Magereza, Uhamiaji. Michezo iko majeshini, kuna wanajeshi, kuna wanajeshi na TAMISEMI kwenye vijiji, Kata na kuendelea.

Kwa hiyo, napenda kumpongeza sana kwa kulitambua hilo. Sisi kama Wizara ni hivi karibuni tu Waziri wangu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, tayari

wameshaandaa utaratibu wa kukutana Wizara hizi tano ili angalau turudishe historia huko tulikotoka kwamba Wizara hizi zikijikita vizuri tunaweza kufanya maajabu katika nchi yetu kwa sababu ndiyo zenye watu.

Kwa hiyo, tunaendelea kuweka mikakati na mipango ili turudishe heshima ya majeshi, michezo ya polisi, michezo ya shule ili tuweze kufanya vizuri zaidi. (*Makofî*)

Suala la pili, sikutaka kuelezea vipaji kwa sababu kila chama husika kina *data base* yake. Lakini kwa faida ya Bunge nataka nieleze tu kwamba mashindano kwa mfano ya *Kopa Cocacola* yaliyochezwa mwaka uliopita yameweza kushirikisha vijana 600 na katika 600 hao wale 20 *best* walichaguliwa wengine wamekwenda Brazil, lakini juzi wenyewe mmesikia kwenye redio kuna vijana wetu hapa kutoka Tanzania Bara na Zanzibar 6 wanakwenda Spain na wametupigia simu tu. Lakini TFF kwa sababu wana *data base* nzuri wakatoa majina ya hawa vijana wafuatao:-

Kuna Omega Sunday - Same, Issa Ramadhani Issa kutoka Zanzibar, Michael Victor, Thomas Emmanuel, Awadhi Juma na Makame. Hawa wamekwenda Spain kwenda kwenye vilabu ili waweze kupata uzoefu na baadaye watumike vizuri kwenye Taifa letu.

Kwenye riadha huko msururu wa vijana 22 ambao wako nje nao wamekwenda kujifunza. Kwa sababu orodha ni ndefu lakini nitampatia Mheshimiwa Blandes na kwa faida ya Wabunge wengine nitawapatia. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, majibu yalikuwa marefa siwezi kuchukua wengine. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Atauliza swali Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Na. 48

### **Ahadi ya Kuwapatia Wananchi Mashamba/Makazi**

**MHE. HERBET J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa ahadi kwa Benki ya Dunia kuwa itawapatia mashamba/makazi mapya wananchi wanaohamishwa kutoka hifadhi ya Msitu wa Derema, Amani na kwamba malipo ya fidia hiyo sasa yamekamilika.

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa, ikiwa Serikali inatambua suala hilo kupitia Ofisi ya Mkuu

(b) Kwa kuwa mwaka 2007 Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza lilipitisha mapendekezo ya kufuta Hati za mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa. Je, kwa nini pendekezo la dharura la kumega ekari 1200 kutoka shamba la mkonge Kibaranga lisitekelezwe ili kutoa makazi kwa wananchi hao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swalii la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) Kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali Wilayani Muheza iliahidi kutoa eneo mbadala kwa wananchi 1,128 waliohamishwa katika eneo la Derema ili kupisha hifadhi ya msitu kwenye ushoruba wa Derema.

Ahadi hii itakamilishwa mara tu baada ya taratibu za ubatilisho wa shamba la Kibaranga lenye Hati Na. 4656 na ukubwa wa hekta 5,730 kukamilika. Wizara yangu tayari imeshawasilisha ombi la kufuta miliki ya shamba hilo kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, umegaji wa ardhi katika eneo lolote lililopimwa hufanyika kulingana na Sheria na Kanuni. Hivyo ugawaji wa ekari 1,200 kwa wananchi wanaohamishwa kutoka kwenye hifadhi ya msitu wa Derema utafanywa mara tu baada ya ubatilisho wa miliki ya shamba la Kibaranga, ambao unatarajiwa kukamilika wakati wowote kuanzia sasa. Wizara yangu itakamilisha kwa haraka hatua zitakazofuata baada ya Mheshimiwa Rais kutoa kibali cha ubatilisho huo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Lakini vile vile nimpongeze sana kwa jitihada ambazo amefanya yeye mwenyewe amefika katika eneo ninalozungumzia na amezungumza na wananchi na amewezesha hali hii kufikia hapo ilipofikia. Sasa swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Kampuni ya *Katani Limited* wamefanya kazi mzuri ya kuwezesha kuzalisha umeme na gesi kutokana na usindikaji wa katani. Lakini vile vile wapo wananchi ambao sasa watapata ardhi na hawa wawekezaji ambao sisi tunawaona ni makini katika Wilaya yetu ya Muheza nao tunadhani watapata nafasi ya kupata ardhi. Je, hawa wananchi pamoja na wawekezaji hao watapata fursa sasa ya kuweza kupata Hati miliki katika maeneo watakayogawiwa ili waweze kupata mikopo ya kuendeleza kilimo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napokea shukrani zake ni kweli nilifika nikiongozana naye kukagua maeneo haya na vile vile na mimi nakupongeza kwa jitihada anazofanya ili tukamilishe jambo hili kwa manufaa ya wananchi. Sasa ameuliza kuhusu suala la kumilikisha wananchi. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwamba mara baada ya

Mheshimiwa Rais kukubali miliki ya zamani ibatilishwe. Tutakapoanza kugawa shamba hilo kwa wamiliki wapya basi ugawaji huo hautakamilika mpaka tumewapa na Hati Miliki. Kwa hiyo, hilo linakuja Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana.

Na. 49

**Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Kupandisha  
Kodi Bila Kuzingatia Kipato cha Mtanzania**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa tunalo Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) nchini ambalo limekuwa ni msaada mkubwa sana kwa Watanzania, lakini Shirika hilo limepandisha kodi zaidi ya 100%.

- (a) Je, katika kuongeza kodi hiyo Shirika lilizingatia kuongezeka kwa kipato cha Mtanzania au mshahara?
- (b) Kwa kuwa ongezeko hili la kodi halifanani na ongezeko la mshahara. Je, Serikali inatoa maoni gani juu ya ongezeko hilo?
- (c) Je, wadau wanaoishi katika nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa walishirikishwa katika mjadala wa ongezeko hilo, kama ndio; ni wakati gani walishirikishwa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambalo linamiliwi na Serikali lilianzishwa mwaka 1962 kwa madhumuni ya kujenga nyumba kwa ajili ya Watanzania wa kipato cha chini na kat. Miaka ya nyuma Shirika lilikuwa linapata ruzuku kutoka katika Bajeti ya Serikali ili kutekeleza majukumu yake. Katika miaka ya hivi karibuni Serikali imesitisha ruzuku na Shirika limeambiwa lijiendeshe lenyewe kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Shirika lijiendeshe kibiashara halina budi kupandisha kodi ya pango la nyumba mara kwa mara. Mwezi Agosti, mwaka jana Shirika lilipandisha kodi ya nyumba za makazi kwa asilimia 60. Kifungu cha 78 cha Sheria ya Ardhi na Kifungu namba 11 cha Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa vimeweka vigezo vya kuzingatiwa kabla ya kupandishwa kodi. Mamlaka ya kupandisha

kodi kwa mujibu wa sheria hii ni mmiliki wa nyumba na sheria haimlazimishi ashauriane na wapangaji wake anapoamua kupandisha kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kodi za Shirika la Nyumba kupanda kwa asilimia 60 bado viwango vya kodi hizo ni asilimia 45 tu ya viwango katika soko. Wananchi wanaonufaika na hali hii ya unafuu wa kodi ni asilimia 0.6 tu ya Watanzania wote. Kutokana na udogo wa kodi, Shirika halipati mapato ya kutosha kukarabati nyumba zake zilizopo wala kujenga nyingine nyingi ili Watanzania wengi zaidi wawzeze wakanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mazingira haya, Serikali imeamua kulifanya mabadiliko makubwa Shirika hilo. Katika mabadiliko hayo, Shirika litaacha jukumu la kupandisha nyumba na kukusanya kodi kama jukumu kuu na badala yake litaelekeza nguvu zake katika ujenzi wa nyumba katika mikoa yote na kuziwa kwa mikopo kwa Watanzania, hasa wa kipato cha chini na kati ambaa ndio walengwa hasa wa Shirika hili. Hatua hii ina lengo la kuwanufaisha Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaanza kuchukua hatua za kuliboresha Shirika la Nyumba ili lifanye mambo mazuri na makubwa kwa wananchi, tunaomba wananchi wawe na subira, watumaini, na watunge mkono. (*Makofi*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa Wizara yake ni Wizara ambayo inahakikisha kuwa na makazi salama katika miji mfano Dar es Salaam na kwa kuwa amekiri kuwa wananchi wengi wa kipato cha chini hawajawenza kwa sasa kupata hizo nyumba ni asilimia 0.6 kutokana na hali halisi na hivyo kuwafanya kujenga katika maeneo hatarishi kwenye mabonde kwa mfano ya Mto Msimbazi na hivi kufanya wakati wa mvua kuwa na mafuriko makubwa katika barabara zetu na kuziba mifereji. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha inatatatua tatizo hilo kabla ya mafuriko hayajawenza kutokea kwa bahati mbaya na kuleta athari kama ilivyo katika maeneo ya Kilosa na maeneo mengine?

Pili, kwa kuwa Shirika la Nyumba lilianzisha makazi kwa njia ya mkopo katika eneo la Boko, eneo ambalo pia lina machimbo ya m awe. Je, kuna utafiti wowote ulifanyika kwamba nyumba hizo hazitakuwa katika athari kutokana na ubomoaji unaofanyika katika maeneo hayo kwa kutumia baruti na mambo mengine?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDEDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, jukumu la kuhakikisha kwamba wananchi wanapata viwanja katika maeneo salama kwa Wizara yangu sisi tunaweka Sheria na miongozo, Sheria ya Mipango Miji. Wanaotekeleza sheria ile wenye jukumu la kupima viwanja na kuvigawa viwanja kwa wananchi ni Halmashauri ya Miji, Manuspaa na Majiji na miji yote hao ndiyo wenye jukumu hilo.

Wizara yangu vile vile inawawezesha kwa kuwapa mikopo ili wafanye kazi ya kupima katika maeneo salama. Manuspaa za Dar es Salaam kwa mfano kwa pamoja, kuanzia mwaka jana tumewapa mikopo ya shilingi bilioni 1.4 wapime viwanja katika

maeneo salama wawagawie wananchi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wako wafuati

Swali la pili, ni kweli *National Housing* walijenga nyumba nadhani 200 kule Boko na wameshaziuza. Ni kweli vile vile hapo jirani na *Estate* ile ya *National Housing* kuna machimbo ya madini lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini wale watu wanaochimba pale walishazuiliwa ili wasiendelee kuharibu mazingira na kuhatarisha hizo nyumba pale mahali zilipo. (*Makofi*)

Na. 50

### **Mpango wa kujenga Upya bandari ya Tanga**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa Bandari ya Tanga ikiimarishwa na kujengwa upya itaiwezesha Tanzania kushindana kwa nguvu dhidi ya Bandari ya Mombasa na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu

Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kujenga upya bandari ya Tanga?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mhesimiwa Lazaro Samwel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Tanga haina uwezo wa kuhudumia meli kubwa kutoana na kina cha maji kwenye gati kuwa kifupi. Kina cha maji kilichopo sasa ni meta 6 wakati wa maji kujaa na meta 3 wakati wa maji kupwa wakati kina kinachotakiwa kuwezesha meli kubwa kutia nanga kwenye gati ni wastani wa meta 12. Gharama ya kuongeza kina inakadirwa kuwa kubwa ikilinganishwa na faida itakayopatikana kutokana na ufinyu wa eneo la kufanya kazi (*back –up area*) mahali bandari ya sasa ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na sababu hiyo, katika utafiti wenye lengo la kubaini mahitaji ya muda mrefu na mikakati ya kuziendezea bandari nchini ama (*Port Master Plan 2009/2010 – 2029/2030*), kwa upande wa bandari ya Tanga imependekezwa kujengwa bandari mpya (*deep seawater port*) katika eneo la *Mwambani Bay*. (*Makofi*)

Mamlaka ya Bandari imekwisha nunua eneo la ekari 92 na ekari nyingine 82 zitanunuliwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2009/2010. Lengo ni kutekeleza mradi huu kwa kushirikisha sekta binafsi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amelijibu swali langu kwa ufasaha na namshukuru kwa sana. Nina ombi moja tu,

kwa sababu ni muhimu tujenge bandari ya Tanga. Ningombaa Serikali ifikirie uwezekano wa kuanzisha *inter ministerial task force* kwa ajili ya ku-source hizo *investment*, ili hiyo kazi ianze, bandari hii itatusaidia?

**WAZIRI WA MIUNDOOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri nimeupokea na tutaufanya kazi.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ningependa kufahamu kutoka Serikalini pamoja na ujenzi wa bandari ya Tanga kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali ina mpango wowote wa kujenga reli ya kutoka Tanga-Arusha mpaka Musoma ili iweze kutumika kwa ajili ya kubeba bidhaa za Uganda na kuifanya bandari ya Tanga sasa iweze kufanya kazi kubwa zaidi kuliko kutegemea bidhaa za Tanzania? (*Makofii*)

**WAZIRI WA MIUNDOOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ina mpango huo na tumeshaanza kuufanya kazi na tunafanya kazi pamoja na Serikali ya Uganda na hivi karibuni tutakuwa na mjadala maalum pamoja na Serikali ya Uganda.

Na. 51

#### **Ahadi ya kujenga barabara toka Nangurukuru – Liwale**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara yenyewe urefu wa km 231 toka Nangurukuru kwenda Liwale kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka kama kichocheo cha maendeleo ya wananchi wa Liwale.

- (a) Je, Serikali inafahamu kwamba, hadi sasa juhudii zake hazijazaa matunda kwa vile barabara hiyo hufungwa nyakati za masika na ni lini ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais itakamilika?
- (b) Je, Serikali inaweza kuainisha sehemu korofii/sugu kwenye barabara hiyo ambazo zinasababisha barabara hiyo kutumika nyakati za masika na inajiandaa vipi kukabiliana na hali hiyo?
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika Awamu ya Nne kwa maboresho ya barabara hiyo ambayo imekuwa ni kero kubwa na ya muda mrefu kwa wananchi wa Liwale na Kilwa Kaskazini?

## **WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chache Kigwailo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa umakini kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali haijakamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kukarabati barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 231) kwa kiwango cha changarawe ili iweze kipitika kipindi chote cha mwaka. Serikali imejipanga kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kuanza kutengeneza sehemu korofii katika barabara hii.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kuptitia Wakala wa Barabara – *TANROADS* tayari imeainisha maeneo korofii katika barabara hii kama ifuatavyo:-

Naking'ombe – Mbwindi      km 05;  
Mbwindi – Zinga               km 04;  
Zinga – Kimambi               km 10; na  
Kimambi – Kichonda           km 10.

Katika kukabiliana na hali mbaya ya maeneo hayo Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuyafanya matengenezo maeneo hayo.

- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani kiasi cha shilingi bilioni 1.77 zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya aina mbalimbali katika barabara hii.

Aidha, jumla ya shilingi milioni 756.33 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya sehemu korofii, matengenezo ya kawaida na ujenzi wa daraja la Miguruwe katika mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Nashukuru kwa majibu mazuri, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Wizara ya Liwale kwa kutumia barabara alikiri kwamba barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi wa Liwale kuwaletaa maendeleo yao na pia kwa wananchi wa Kilwa Kaskazini pamoja Nachingwea kwa kuwa ni fupi mno na hapo hapo aliwaahidi watu wa *TANROAD* kwamba atawasaidia kufuatilia bilioni 1.9 ambayo inahitajika kukamilisha kwa sehemu korofii ili iweze kutumika kipindi chote cha mwaka.

Je, hatua ipi imefikiwa hadi hivi sasa kwa maombi hayo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu vilivyo?

La pili, kutokana na hali ilivyo sasa hivi haipitiki maeneo korofii na wananchi wa Liwale wanataka kuendelea kutumia. Na hivi sasa magari yanakwama sana.

Je, Serikali na Waziri kwa vile uko makini unaweza kukubaliana na mimi sasa chukua hatua za mpito kwa kutumia makandarasi waliopo katika maeneo yale ili wawze kurahisisha usafiri ili wananchi wale wa Liwale pamoja na wafanyabiashara waendelee kutumia kwa kipindi hiki. Naomba Mheshimiwa Waziri hili liwe lako?

**NAIBU SPIKA:** Haya baada ya kujibu itakuwa kimeelewaka. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama nilivyo sema katika majibu ya msingi ni kwamba mwaka huu wa fedha tumeitengea hiyo barabara shilingi milioni 756,000 kwa hiyo katika zile milioni elfu moja na mia tisa alizozitaja Mheshimiwa ni kwamba karibu nusu ya fedha hizo ziko katika Bajeti tayari.

Kwa hizi ambazo haziko kwenye Bajeti bado tuna changamoto ya kuweza kuzipata kutoka nje ya Bajeti kazi ambayo siyo rahisi sana kipindi hiki hasa kwa kuzingatia kwamba pia tumepata maafa katika sehemu mbalimbali ambayo yatahitaji jumla ya shilingi bilioni 13 nje ya Bajeti. Kwa hiyo tutajitahidi kadri tutakavyoweza. Siwezi kutoa ahadi mahsus kwa Mheshimiwa Mbunge lakini tutajitahidi kwa kadiri tutakavyoweza kuhakikisha kwamba tunapata pesa zaidi kwa ajili ya kuhudumia barabara hii. (*Makofî*)

Hatua za dharura, nimelisikia ombi hilo na nasema tu kwa Mheshimiwa Mbunge tutawaagiza wataalam ili waangalie kwa makini namna ambavyo tunaweza tukafanya kazi nzuri na mkandarasi yule kuifanya hii barabara ipitike kipindi cha masika. (*Makofî*)

Na. 52

#### **Tatizo la Mazao ya Biashara na Nafaka**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

- Kwa kuwa soko la mazao ya biashara na nafaka ni muhimu sana kwa wananchi.
- (a) Je, kwa nini Serikali inazuia wananchi wasiuze mazao yao nje ya nchi, hasa mazao ya nafaka kama vile mahindi?
- (b) Je, kwa kufunga mipaka kwa mazao ya nafaka Serikali haioni kwamba, wananchi wananyonywa na walangazi wa ndani?

#### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Wizara imeandaa mkakati wa Kitaifa wa Kukuza soko la bidhaa za Tanzania nje ya nchi likiwemo soko la mahindi, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi wakiwemo wa Jimbo la Njombe Magharibi kuruhusiwa kuuza mazao yao nje ya nchi.

Hivyo, ni Sera ya Serikali kuruhusu biashara ya mazao ya chakula kwenda nje ya mipaka ya nchi. Hata hivyo, suala la usalama wa chakula kwa nchi yetu pia hupewa kipaumbele.

Nyakati za upungufu wa chakula Serikali imejiwekea utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji wa chakula unakuwepo na vyakula hivyo havipandi bei kiasi cha kuwafanya wananchi wa kawaida kushindwa kujinunulia vyakula katika masoko. Utaratibu huu ni kulingana na Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 381, Toleo lililorekebishwa 2002 (*Export Control Act Cap. 381 of 2002*).

Kwa mujibu wa Sheria hii, zipo Sheria ndogo ndogo zilizotungwa zinazoainisha aina ya bidhaa zinazozuiliwa kusafirishwa nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, usitishwaji wa usafirishaji wa mazao ya chakula nje ya nchi uliopo sasa unatokana na hali halisi ya chakula nchini kwa misimu miwili mfululizo yaani 2006/2007 na 2007/2008 ambapo maeneo mbalimbali ya nchi yamekuwa yakikabiliwa na upungufu wa chakula. Hivyo Serikali huzuia nafaka hasa mahindi kuuzwa nje ya nchi pale tu hali ya usalama wa chakula inapokuwa siyo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa athari zinazoweza kujitokeza kutokana na zuio la kuuza mazao ya chakula nje ya nchi, Serikali kuitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve Agency (NFRA)*) imekuwa ikichukua hatua madhubuti ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mazao ya nafaka kutoka kwa wananchi kutoka kwenye mikoa yenye ziada ya chakula na kutawanya kwenye mikoa yenye upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa mazao makuu ya biashara kuwa na bodi zinazosimamia mwenendo wa zao husika ikiwa ni pamoja na kusimamia bei; Serikali ipo kwenye mchakato wa kuunda bodi ya mazao mchanganyiko ambayo itahusika na mazao yale ambayo kimsingi hayana bodi, yakiwemo mazao ya nafaka ikiwa ni njia mojawapo ya kupunguza unyonyaji unaofanywa na walangazi wa mazao hayo. (*Makofi*)

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini utekelezaji katika Wizara ya Kilimo sio ilivyo. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kuzuia wakulima kuuza nafaka yao kwenye soko la nje ili kupata bei nzuri, kunawakatisha sana tamaa wakulima hapa nchini na hivyo kusababisha upungufu kwa chakula na kuendelea kuwa tatizo sugu. (*Makofi*)

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba huo utaratibu aliokuwa anauzungumzia utekelezwe na Wizara husika kwa maana ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa sababu ni majibu ya Wizara ya Viwanda na Biashara lakini huku kulivyo hawafanyi hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kwa kuwa hivi karibuni nilitembelea Jimbo la Peramiho kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, nikafika katika vijiji vifuatavyo, nikafika kijiji cha Magagula, Mgazini na Madaba. Kule niliona kuna utaratibu mzuri Serikali imeweka wa hifadhi ya chakula wanunuwa wakulima pale wanunuwa, sasa kwa vile na mimi katika vijiji vilivyopo Kata ya Luduga, Igesi, Imalinyi, Illembula, Mdandu, Wangama, Wanging'ombe na Usuka, vina ziada ya uzalishaji kama vijiji vilivyopo Peramiho. Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua vituo kama ilivyo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama? (*Makofi*).

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kevela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru sana kwa kunipongeza kwa jibu zuri, ninaamini ameipongeza Serikali. Na kuhusu swalii lake la kwanza, kwamba kuzuia wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi ili wapate bei nzuri na kwa kuzuiwa wanakatishwa tamaa na hivyo katika miaka inayofuata pengine inawafanya wasilime zaidi; ninakubaliana naye lakini bila ya shaka na yeye anakubaliana kwamba suala la usalama wa chakula ni muhimu. Na hapo awali kuliwa na wananchi kutoka Bukoba wamelalamika kwamba bei ya ndizi imepanda sana kwa sababu ndizi zinauzwa Sudani.

Na mimi nikajibu kupitia vyombo vya habari kwamba jibu ni kulima kwa nguvu zote na kwa maarifa yote kusudi tuwe na chakula cha kutosha na ziada tunaweza kuiiza nje. Lakini kama hatutakuwa na chakula cha kutosha sisi Watanzania hatutaonekana kama tuna busara kukubali kuuza chakula chetu halafu tununue kwa bei ya juu. Kwa hivyo, pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula na Serikali nzima, itaona namna ambavyo itaimarisha kilimo kwa nia ya kuongeza uzalishaji wa chakula na kupitia KILIMO KWANZA. Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukiwemo na sisi wote, wametuonesha umuhimu wa Watanzania kutumia ardhi yao nzuri kuzalisha mazao ya kilimo kwa wingi ikiwemo chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ninashukuru sana kusikia kwamba kuna utaratibu mzuri sana wa hifadhi ya chakula kule Peramiho, nampongeza Mheshimiwa Jenista, Mbunge na wananchi wa Peramiho na ninampongeza vilevile Mheshimiwa Kevela kwa kutaka kuanzisha utaratibu huo mzuri katika jimbo lake na katika vijiji alivyovitaja. Serikali itakuwa nyuma ya wale wote ambao watakuwa na utaratibu mzuri kwanza wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na hasa chakula na sisi tutakuwa nyuma yenu kuona kwamba utaratibu huo mzuri unajikita na nchi yetu kujitosheleza kwa chakula na kuweza kuuza ziada nchi za nje na wakulima wetu kupata bei nzuri na ili waweze kulima zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umeisha maswali yamekwisha na yamechukua muda wa dakika tano nyingine. Tulicho jifunza ni kwamba sasa hivi Mawaziri majibu yao ni *page* moja tu. Kwa hiyo, mimi ninaomba niwapongeze hivyo. Wanaandika majibu yao, ni mafupi kama inavyotakiwa, mimi hapo ninaomba niwapongeze sana. Tatizo liko kwenye maswali ya nyongeza, ziko hotuba kabisa. Kwa hiyo, unafika mahali huwezi kuwa uliza maswali ya nyongeza zaidi ya mawili, huwezi inakuwa muda hautoshi; maana mimi bahati nzuri ninafanya kila swali tumetumia dakika ngapi. Kuna *the longest* swali letu tumetumia dakika 12. Kwa hiyo, nikamu-*offend* Kiongozi wa Shughuli za Wapinzani, aliposimama sikumpa nafasi kwa sababu tayari ilikuwa zimeshazidi dakika 12. Kwa kawaida kila swali ni dakika 5 tu. Kwa hiyo, mimi ninawapongeza Mawaziri, ninaomba Wabunge, na nyie muanze kufanya vizuri. (*Makofi*).

Sasa tuna wageni. Kuna wageni wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Dr. Batilda Buriani, ambao ni Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira, Bwana Richard Muyungi. Sijui aliko ni wapi? Kuna Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa mazingira Bwana Stephen Mkondo Kaya, kuna Profesa Kinabo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Mimi sijui hawa wako wapi? Kuna Ndugu Majili kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, kuna Dr. Israel Kagege kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, kuna Ndugu Denis Mahimbo, kutoka Chuo cha Cha Mipango Dodoma. Kuna Ndugu Julius Manyerere, kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, kuna Ndugu Makari Moshi kutoka Chuo Cha Miapango Dodoma, kuna George Sayula kutoka Chuo Cha Mipango Dodoma. Sijui kama hawa wote wamekosa nafasi, nadhani!

Sasa nina wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata, ambao ni *Mr. and Mrs. Jackson Betty*, sijui wako wapi hawa? H awa Ndugu nasikia wameoana Jumapili iliyopita. Kwa hiyo, wako kwenye *honeymoon* hivyo; si vibaya ukafanya *honeymoon* katika Bunge ukasikiliza busara mbalimbali. Ninaomba tuwapongeze sana kwa uamuzi wao huo. Lakini wao wote wawili ni waimbaji wa nyimbo za injili. (*Makofi*)

Halafu tuna mgeni mwagine anaitwa Elias Exaveri, mfanyakazi wa Umoja wa mataifa kutoka Viena, Australia; yuko wapi? Karibu sana, ahsante sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr Raphael Chegeni, ambao ni viongozi wa Chama na serikali katika Jimbo la Busega, ambao naomba wote wasimame waliko huko.

Hawa ndio wageni wa Mheshimiwa Dr. Chegeni, kwa majina yao yupo Joseph Msome, yupo Peter Mangushi, yupo Charles Chongela, yupo Limbu Mhulu, yupo Joseph Mabeyo, yupo Malangu Bulengela na yupo John Mzala. Kule Busega akina mama hawapo bila ya shaka! Ahsante sana wageni wa Mheshimiwa Mbunge, karibuni sana. (*Makofi*).

Tunao wageni wa Wabunge, Wabunge hawa ni Profesa Mark Mwандосya, Waziri na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum. Ni wanachuo wa Chuo Kikuu Dodoma, mwaka wa kwanza na ndio wanafunzi wa *Tukuyu Day Secondary* ambao yupo Baraka Edmo, yupo Regina Kansapa, yupo Devi Sarufu, yupo

Alexander Mtweve, yupo Fredrick Melkion na yupo Aletauwa Davis. Asanteni sana hongera kwa kuwa wakwanza huko Tukuyu, nadhani mutavuta na wengine zaidi. (*Makofi*)

Halafu tuna wageni 25 kutoka *Mshike Mshike Art Group, Dodoma*, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Hawa Ndugu wa Mshike Mshike wako wapi sasa? Wasimame wote waliko, ahsante. Karibuni sana wageni wetu. Tunao wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, naomba wasimame hao wote 30 waliko, ahsante sana ninyi ndio majirani zetu wakati wote Bunge linapokuwepo hapa mnakaribishwa; hamhitaji mwaliko rasmi, mnakaribishwa wote kabisa na mu-take advantage ya kuweko Bunge hapa na Ofisi zake, karibuni sana. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo matangazo ya wageni na wengine ambao hatukuwasoma hapa naomba wote wajisikie ndani ya Bunge hili wanakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, mukiangalia kitu cha Waziri Mkuu, hayupo leo yuko safari nje ya Dodoma na kwa hiyo Profesa Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji ndiye anayeshikilia shughuli za Serikali hapa Bungeni. Na mnajua utaratibu unakwenda according to the most senior minister, ndio hivyo. (*Makofi*).

Waheshimiwa sasa tuna matangazo ya kazi; Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana, katika ukumbi utakaoelekezwa na Sekretarieti, watakuwa na kikao. Kwa hiyo sasa Sekretarieti nadhani itawaeleza, mimi sijui ukumbi gani, lakini mutakuwa na kikao saa 07.00. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora.

Mheshimwia Omar Kwang'w, yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anaomba kibali changu kwamba leo tarehe 29/1/2010, Kamati yake ikutane kujadiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuhusu Sera ya Elimu. Na hawa wanaomba kibali kwa sababu watakutana saa 5.00 asubuhi hii.

Kwa hiyo, saa 5.00 asubuhi Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii itakutana katika chumba cha Msekwa, Ukumbi wa Msekwa B. Kwa hiyo, ninadhani baada ya kipindi hiki mnakutana kule, nadhani pale mmealika watu wengi zaidi kuwasikiliza.

Mwenyekiti, wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kuwa watakutana saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kujadili Muswada wa Archtec na *Quantity Surveyors Registration Act, 2009*. Sasa kama mutakuwa mumegongana huko, nadhani mutajua wenyewe, kwa sababu kuna kumbi mbili huko; mwingine mkubwa ule na mwingine uko kule juu, mutafahamiana huko.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu pia, anaomba anapenda kuwataarifu kuwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu imekamilisha kazi, hii ilikuwa inapelekwa kwa

Spika hii, nadhani imeletwa kwa makosa. Wamekamilisha ile shughuli yao. Kwa hiyo, ndio hoja inayokuja baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yamekwisha, tunaendelea na hatua inayofuata.

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema jambo ninalotaka kusema kuhusu utaratibu, kwanza ninakupongeza kwa kazi nzuri uliyofanya na unayofanya kila mara kuhakikisha majibu ya Wabunge yote yanajibiwa. Ninataka kusemea kuhusu Kanuni Namba 40 (e).

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni inasema, “*Swali lolote la Mbunge, halitaruhusiwa kuulizwa Bungeni kama,*” ninasoma kifungu kinachohusika (e), “*lina maelezo ya dhihaka, uwongo, sifa zisizolazimu na au linatokana na habari za kubabaisha.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipouliza swalii kuhusu Komoro na nilipouliza swalii la nyongeza, nilitumia neon rushwa. Neno hili sikuwa na maana ya kulitumia, nilikuwa na maana ya kusema kwamba kumekuwa na ushawishi wa kiuchumi na kisiasa wakati kampeni zinapofanywa za wananchi wa kule kupiga kura, Kwa hiyo, neno rushwa naomba kulifuta.

**NAIBU SPIKA:** Haya, tunashukuru sana kwa, tunaweza kuita nini?, Ni dalili nzuri ya unyeyekevu tu ni unyenyekevu. Kwa sababu swalii lilikuwa jana na sisi tulishangaa kwa sababu unaweza kusababisha ugomvi kati ya nchi na nchi na usiweze kuthibitisha vitu vingine.

Kwa hiyo, tunashukuru kwamba hilo limeondoka na watakaokuwa wanaandika wajue kwamba Mbunge amesahihisha usemi wake wa jana. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Mzindakaya. (*Kicheko*).

Tunaendelea, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

## **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa naibu Spika, maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge.

Maelezo haya yanatolewa chini ya Kanuni ya 150 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Vikao vya Bunge hufanyika siku zote za wiki isipokuwa siku za Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko.

Na kwa kuwa, Mkutano huu wa 18 wa Bunge unaoendelea hapa Dodoma, umepangwa kufanyika kwa siku 14 tu, ambapo mionganoni mwa shughuli zinazohitaji kufanyiwa kazi ni Bunge kujadili na kupitisha Miswada 9 ya Sheria ya Serikali, kupokea na kujadili taarifa 6 za Kamati mbalimbali za kudumu za Bunge, Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango, Bunge kujadili na kuridhia maazimio 6 na pia kupokea na kujadili hoja binafsi 2 za Wabunge na kufanya chaguzi za wajumbe wa Vyuo mbalimbali Vikuu hapa nchini.

Na kwa kuwa, siku za Mkutano huu wa 18 wa Bunge unaoendelea sasa haziwezi kuongezwa kutokana na ukweli kuwa muda ulibakia unahitajika kwa Wabunge kurudi kwenye Majimbo yao kabla ya kurudi na kuendelea na shughuli za Kamati kwa maandalizi ya Mkutano ujao wa 19.

Kwa hiyo basi, Bunge sasa linaazimia kwamba kwa madhumuni ya kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa 18 wa Bunge. Kanuni ya 28 (15) inayoelekeza kwamba vikao vya Bunge vitafanyika siku zote za wiki isipokuwa Jumamosi, Jumapili au Siku za Mapumziko, sasa itenguliwe na badala yake utaratibu ufuataao utumike, na ninaomba kunukuu.

*“Iwapo shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Kikao hazijamalizika, Spika atalihoji Bunge kuhusu hoja ya kuhirisha Kikao cha Bunge na baada ya hoja hiyo kuafikiwa atakiahirisha Kikao hicho hadi siku inayofuata hata kama siku hiyo itakuwa ni Jumamosi. Isipokuwa kwamba siku ya Jumamosi hakutakuwa na kipindi cha maswali.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Bunge liliafiki Kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa*)

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta wa Mwaka  
2009. (*The Electronic and Postal Communication Bill, 2009*)**

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehema, na ulinzi wake uliotuwezesha kufikia mwaka 2010. Naomba nichukue fursa hii kuwatachia Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na wapiga kura wangu kheri ya Mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuungana na wabunge, Ndugu jamaa na marafiki kuwafariji na kuwapa salaam za rambirambi familia ya mzee wetu na mlezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ambaye alikuwa ni mmoja wa waasisi wa Taifa letu Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefariki dunia tarehe 31 Desemba, 2009 tunaomba Mwenyezi Mungu awajalie moyo wa ustahimilivu wanafamilia katika kipindi hiki kigumu cha kupotelewa na mpandwa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kutumia fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliofikwa na majanga ya asili yakiwemo maporoko ya ardhi huko Same, mafuriko huko Kilosa ambayo yamesababisha kupotelewa na wapendwa wao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uwenyekiti na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini (CCM) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mbunge wa Same (CCM) ambao wameshiriki kikamilifu katika kujadili Muswada huu.

Pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati (CHADEMA) ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya upinzani kuhusu Wizara yangu na Waziri Kivuli kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuboresha pendekezo la kutungwa kwa Sheria ya Mawasiliano ya Kielectroniki na Posta (*The Electronic and Postal Communications Act, 2009*). Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote walioshirikiri katika kuchangia maoni na kukubaliana na Serikali kuhusu pendekezo la kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kubwa kuwa mbele yenu kutoa Maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielectroniki na Posta, yaani *The Electronic and Postal Communications Act, 2009*.

Kupitisha sheria hii ni moja ya utekelezaji wa maagizo ya Serikali pamoja na majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayasi na Teknolojia kwa ujumla. Ushauri wenu ambao mmekuwa mkiutoa wakati wote umetokana na uzalendo mlionao kwa nchi yetu na hii imechangia sana katika kuhakisha kwamba teknolojia ya habari na mawasiliano inachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lengo la Muswada. Muswada ulioambatishwa katika Hati hii unakusudia kutungwa kwa Sheria ambayo itashughulikia masuala yanayohusu Mawasiliano ya Elektroniki na Posta ambayo yatarahisisha, kuboresha na kuimarishe huduma za mawasiliano nchini na pia kuwezesha wadau kushiriki kwenye utoaji wa huduma ya mawasiliano kwa biashara ya ushindani kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukua kwa haraka kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kumejitokeza mwingiliano wa teknolojia (*Convergence of Technology*) na hivyo kuathiri usimamizi na utekelezaji wa Sheria za Mawasiliano zilizopo kwa sasa; hivyo kusababisha migongano ya mara kwa mara ya vyombo vya usimamizi.

Hali hii imepelekea kuzorota kwa huduma za mawasiliano ya simu sanjari na Serikali kukosa mapato yatokanayo na uendeshaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada. Madhumuni ya Muswada huu ni kuboresha matumizi ya simu, kusimamia matumizi mabaya ya simu za vinganjani, kuthibiti uchafuzi wa mazingira na ongezeko la gharama za huduma za simu, kuzuia matumizi mabaya ya mitandao.

Kutambua mfumo mpya wa watangazaji wa digitali, kutambua uwepo wa rejesta ya utaratibu wa utambuzi wa vifaa vya mawasiliano, kuwezesha kila mtumiaji wa huduma kupata anuani itakayomwezesha kutambulika na kutambua umuhimu wa *International Mobile Equipment Identity (IMEI)* ili kuzuia wizi wa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo Muhimu Katika Muswada. Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria inayopendekezwa inakusudia kuweka utaratibu wa Kanuni za Kisheria za kuwepo ulazima wa kusajili kadi za simu na kuanzisha masjala ya watumiaji wa simu za viganjani ili kudhibiti matumizi mabaya na wizi wa simu za viganjani;
- (ii) Kuwa na Sheria moja inayozingatia mwingiliano wa teknolojia badala ya sheria mbili za sasa zinazotenganisha Mawasiliano ya Simu na Utangazaji;
- (iii) Kuweka utaratibu wa kisheria kwa watoa huduma za Mawasiliano kushirikiana katika umiliki wa miundombinu hasa minara na hivyo

kupunguza athari za msongamano wa minara na hivyo kupunguza gharama za uwekezaji na hatimaye kufikisha huduma kwa mtumiaji kwa bei nafuu; na

- (iv) Kuweka utaratibu wa matumizi ya mitandao nchini na kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu Tisa. Sehemu ya kwanza inatoa masharti ya utangulizi wa Muswada pamoja na jina la Muswada husika na ufanuzi wa baadhi ya maeneo au misamiati iliyotumika katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza maelezo ya jumla, sehemu hii inahusu mawasiliano ya ki-elektroniki ambayo yanajumuisha masuala ya leseni katika mfumo mpya wa mwingiliano wa teknolojia, matumizi ya mitandao ya maunganisho ya mawasiliano sambamba na miundombinu ya mawasiliano kwa ujumla wake. Sehemu hii inaruhusu mamlaka kuingilia kati pale ambapo watoa huduma wanashindwa kukubaliana katika matumizi ya pamoja ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inahusu masuala ya posta pamoja na taratibu zake zote ikijumuisha barua, vifurushi na vipeto (*small packets*) na vile vile masuala posta na anuani za makazi.

Sehemu ya nne, inahusu masuala ya ushindani wa kibiashara pamoja na taratibu zake katika Sekta ya Mawasiliano na masharti au miiko yake, sambamba na adhabu pindi watoa huduma wanapokiuka taratibu au kuvunja miiko ya ushindani iliyoinishwa. Pia sehemu hii inaongelea management ya masafa, Kamati ya Masuala ya Masafa, ugawaji wa namba na viwango vya kiufundi vya vifaa vinavyotumika kwenye mitandao ya mawasiliano na uhalali wake. Inajumuisha pia uanzishwaji wa masjala ya watumiaji wa simu za viganjani na taratibu zake, sambamba na usajili wa kadi za simu na vifaa husika. Vile vile inaongelea majukumu ya watoa huduma za mawasiliano, mawakala pamoja na watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa ujumla wake.

Sehemu ya tano, inaongelea suala la ufuatiliaji na utekelezaji wa sheria hii. Sehemu hii pia inabainisha jukumu na uwezo wa mamlaka ya mawasiliano wa kufuatilia na kukagua kama watoa huduma za mawasiliano wanazingatia sheria, kanuni na taratibu za Sekta ya Mawasiliano kwa ujumla wake.

Sehemu ya sita, inaelezea makosa yote yanayohusiana na masuala ya mawasiliano ya kieletroniki na posta, ikiwa ni pamoja na makosa yatokanayo na matumizi mabaya ya simu za viganjani, usajili wa simu, masuala ya posta, matumizi mabaya ya masafa, mwingiliano wa makusudi wa masafa na makosa mengine ya nyongeza ambayo yamejitokeza katika sekta ya mawasiliano kwa ujumla na mapana yake. Pia sehemu hii inaainisha adhabu mbalimbali zitakazotolewa kulingana na makosa hayo.

Sehemu ya saba, inapendekeza vifungu vinavyohusiana na namna ya kupata ardhi kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mawasiliano. Sehemu hii pia inatoa mamlaka ya kupekua na kukamata vifaa visivyoruhusiwa katika shughuli za mawasiliano. Pia inaweka masharti ya kupokelewa kwa hati mbalimbali zinazotolewa na mamlaka kama uthibitisho. Sehemu hii pia inaweka masharti yanayohitajika kurahisisha utekelezaji wa sheria hii na jinsi ya kusajili watumiaji wa simu za mawasiliano ya electronic kabla sheria hii haijaanza kutumika.

Sehemu ya nane, inapendekeza vifungu vya mpito na mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni.

Mwisho ni sehemu ya tisa, inayofanya marekebisho katika sheria nyingine ili kuleta uwiano katika matumizi ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako makosa madogo madogo ya kiuandishi na kiuchapaji katika Muswada huu, ambayo yatafanyiwa kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa kukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufanuzi zaidi, tumeambatanisha Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Electronic na Posta wa Mwaka 2009 (*The Electronic and Postal Communication Act, 2009*) kwa ajili ya rejea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. ANNE K. MALECELÀ (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2010 (*The Electronic And Postal Communication Act, 2009*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kwa heshima na taadhima, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Muswada huu mpya wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (*The Electronic and Postal Communication Act, 2009*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nasimama hapa kuwasilisha Maoni ya Kamati tangu kuondokewa na Mbunge mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, aliyesariki tarehe 2 Novemba, 2009; na kwa kuwa Marehemu Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng'itu alikuwa ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa niaba ya wenzangu naomba nitoe pole kwa mjane, watoto wake na familia nzima ya Marehemu; pamoja na Wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuondokewa na Mbunge wao. Marehemu atakumbukwa kwa ushirikiano na mchango wake katika kuiwezesha Kamati ya Miundombinu kutekeleza majukumu yake.

“Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng’itu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii pia kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa (Mb), pamoja na familia nzima kwa msiba mkubwa wa Mzee wetu na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, aliyefariki tarehe 31 Desemba, 2009. Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mzee wetu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba, uliipelekea Kamati hii kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (*The Electronic and Postal Communication Act, 2009*). Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilitekeleza kazi hiyo kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati hii ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaji Mohammed Hamisi Missanga; pamoja na Wajumbe wote wa Kamati, kwa kushiriki kwao katika hatua zote za kuupitia na kuujadili kwa ufasaha Muswada huu. Nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwani ushiriki wao na michango yao ndio imesaidia kuboresha Muswada huu ikiwa ni pamoja na maoni ya Wadau walioshiriki kikamilifu katika Mjadala (*Public Hearing*). Kazi kubwa iliyofanyika kuuboresha Muswada inajidhihirisha katika Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendment*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaji Mohammed Hamisi Missanga -Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela –Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Pascal Constatine Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Dkt. Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Alhaji Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeletwa kwa madhumuni ya kufutwa kwa Sheria za Mawasiliano, Sura ya 302 na Sheria ya Utangazaji, Sura ya 306 na kutunga Sheria mpya ya sekta itakayokidhi mahitaji kufuatana na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia. Aidha, Muswada huu una lengo la kuimarisha huduma ya mawasiliano nchini kulingana na mazingira ya wakati huu, kuingia kwenye mfumo wa soko huria la ushindani wa kibiashara na kutoa huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tukiusubiri Muswada huu muhimu. Kamati inaipongeza Serikali kwa dhati kwa kuleta Muswada, ambao utawezesha Sheria itakayotungwa humu Bungeni kukidhi mahitaji ya sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii mpya inatarajiwa kuwa suluhisho katika baadhi ya Sheria zinazotumika sasa, ambazo zilikuwa na upungufu katika kudhibiti matumizi mabaya ya huduma za simu, kulinda maadili ya taifa, kudhibiti wizi wa simu za mikononi na kudhibiti mwingiliano wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007; Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau husika wa Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta wa Mwaka 2010 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya Wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 14 na 15 Januari, 2010 katika vikao vilivyofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza kwa dhati Wadau wote walioshiriki kikamilifu katika kuuboresha Muswada huu, ambao ni kutoka Mashirika, Makampuni, Taasisi na Sekta mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Soko la Hisa Dar Es Salaam (*Dar Es Salaam Stock Exchange*), *Capital Markets and Security Authority*, Mamlaka ya Usajili wa Makampuni (BRELA), Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), *Courier Association, Tanzania Internet Service Providers Association (TISPA)*, Dovetel (T) Limited, Six Telecom Company Limited, Seacom Tanzania Limited, Afsat Communication (T) Limited, Alldean Satelite Network (T) Limited, Simbanet (T) Limited, Zanzibar Telecommunication Limited (ZANTEL), VODACOM Tanzania Limited, ZAIN Tanzania Limited, MIC Tanzania Limited (TIGO), Benson Information Limited, Shirika la Msaada wa Sheria Tanzania (NOLA) na wengineo wengi ambao sitawezza kuwataja wote lakini wameshiriki kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ilifanikiwa pia kushirikiana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais (Ikulu), Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mawasiliano Zanzibar pamoja na Wizara nyingine katika kuujadili na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Sheria hii imecheleweshwa kutungwa kwani kwa muda mrefu Wadau wa huduma ya mawasiliano wamekuwa wakiitumia huduma hii bila kuwa na sheria. Muswada huu utaziwezesha mamlaka husika kusimamia, kulinda na kuboresha huduma za sekta ya mawasiliano kwa pande zote mbili; yaani kwa mtoa huduma na mtumiaji wa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu kwa wakati tulionao, ambapo kumekuwa na ongezeko la ukuaji wa kasi wa matumizi ya mawasiliano ya kielektroniki.

Kukua kwa teknolojia hii kunahitaji Sera, Kanuni na Sheria zitakazosimamia na kudhibiti matumizi ya teknolojia hii. Kamati inashauri Serikali kupitia upya Sheria nyinginezo zinazohusu sekta ya fedha, biashara na uwekezaji ili kuondoa migongano inayoweza kujitokeza wakati wa matumizi ya sheria hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuboresha na kulinda miundombinu ya mawasiliano nchini. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuwa na mawasiliano ya uhakika, kupunguza gharama kwa watumiaji wa huduma hii ya mawasiliano na kuongeza Pato la Taifa. Sheria hii itaiingiza Tanzania katika ulimwengu wa kisasa katika matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na hivyo kuchangia kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Sheria hii itakapoanza kutumika itaweka uwiano ulio sawa kwa watoa huduma na watumiaji wa huduma hii, kuhamasisha ushindani halali katika soko la biashara na kumpunguzia gharama mtumiaji/mlaji wa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata huduma za mawasiliano kwa ufanisi na kwa wakati, Kamati inashauri Serikali kuharakisha zoezi la uchapishaji wa anwani na simbo za Posta. Zoezi ambalo linaenda taratibu ikilinganishwa na umuhimu wa mpango huo na kasi ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono zoezi la usajili wa kadi za simu, kwani imekuwa ni kero kwa baadhi ya watu kutumia vibaya simu zao za mikononi kuwadhalilisha na kuwatukana watu wengine. Sheria hii itadhibiti tatizo hilo pamoja na kudumisha ulinzi, amani na utulivu katika jamii. Kamati inashauri uwekwe utaratibu mzuri wa kuzuia wizi wa simu za mikononi. Mamlaka zinazohusika zidhibiti uingizaji holela wa simu za mikononi nchini, ambazo baadhi huwa hazina ubora na viwango vinavyotakiwa. Simu nyingi zinapoibiwa inakuwa vigumu kuzipata kwa kuwa hazikusajiliwa, kuhakikiwa na hazina teknolojia ya IMEI inayoruhusu utambuzi wa simu iliyoibiwa kufungwa au kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 71(1) cha Muswada huu kinazungumzia udhibiti wa masafa kwa watoa huduma ya mawasiliano. Pamoja na kuwa sheria imeweka utaratibu wa kumtaarifu mhusika kabla ya kumnyang'anya masafa hayo; Kamati inashauri utaratibu wa kumnyang'anya mto huduma masafa ufanyike kwa umakini kwa kuwashirikisha wahusika watoe maelezo kwa nini masafa yanyang'anywe au yasinyang'anywe. Ushirikishwaji huu utasaidia kuweka mazingira bora kati ya mto huduma na msimamizi wa huduma hii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 75(1) cha Muswada huu kinazungumzia kuweka dhamana kabla ya hukumu (*Deposit Before Conviction*); Kamati inashauri Serikali pamoja na nia nzuri ya utaratibu huo, ni vema ikajiridhisha na kujifunza kutoka

nchi zilizofanikiwa kwa kuwa na utaratibu huo. Hii itasaidia kujua changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa matumizi ya sheria hii inapotakiwa kutoa dhamana kabla ya hukumu, kwani ni utaratibu mpya na haujazoeleka kwa nchi zinazozingatia utawala bora. Aidha, Mamlaka husika izingatie dhana nzima ya ushirikishwaji wa Wadau kabla ya kuanzisha mipango yoyote mipy ya maendeleo ya sekta au teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 78(7) cha Muswada huu kinazungumzia mfumo wa zabuni (*Spectrum Allocation and Assignment*); utaratibu huu ni mpya pamoja na kwamba huko nyuma uliwahi kutumika katika Sheria ya Mawasiliano ya Mwaka 2001. Kamati inaishauri Serikali kabla ya kutunga Kanuni za kuwezesha kutekelezwa kwa sheria hii, ni vema ukafanyika utafiti wa kutosha kubaini faida na hasara zake, kasoro zilizojitokeza na utaratibu huo kuachwa na sababu zipi sasa zinaweza kushawishi utaratibu huo wa zabuni kurudishwa na kutumika bila kuleta usumbufu kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 26 cha Muswada huu kinazungumzia *Requirement on Shareholders*. Kwamba, sheria hii inayataka Makampuni ya Simu za Mikononi kuingiza hisa zao *Dar Es Salaam Stock Exchange*; utaratibu ambao ni mpya kwa watoa huduma za mawasiliano Tanzania. Kamati ilijulishwa kuwa, pamoja na kwamba utaratibu huu ni mpya, una manufaa kwa taifa na kusaidia kuzuia mianya ya uhamishaji wa fedha za Kitanzania nje ya nchi. Kwamba, utaratibu huu umekuwa ukitumika kwa baadhi ya Makampuni ya hapa nchini kama vile *Tanzania Oxygen, Tanzania Breweries Limited, Tanzania Cigarette Company, Simba Plastic, Swissport Tanzania, Twiga Cement, NICOL* na wengineo. Aidha, kuna Makampuni ya Kitanzania ambayo yamejiandikisha katika *Stock Exchange* za nje ya nchi, kwa mfano, *VODACOM Tanzania* wameingia *JSE Securities Exchange* ya Afrika ya Kusini, *ZAIN (MTC)* wameingia *Stock Exchange* ya Kuwait, *TIGO (MIC)* wameingia *Stock Exchange* ya Marekani na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inayashauri Makampuni ya Tanzania, hasa Makampuni ya Simu za Mikononi, yasiogope kujisajili *Dar es Salaam Stock Exchange*, kwani maendeleo na uchumi wa Tanzania utajengwa na Watanzania wenyewe. Wawekezaji wa Kitanzania wawe na uzalendo wa kuwekeza nchini ili kutoa fursa kwa Watanzania wenzao kufaidika na biashara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa, kuna baadhi ya Makampuni ya nje, ambayo yameingiza hisa zao *Dar Es Salaam Stock Exchange*. Makampuni hayo ni kama vile *Kenya Airways, East African Breweries Limited, Jubilee Holdings Limited* na *Kenya Commercial Bank*. Kuingia kwa Makampuni haya *Dar es Salaam Stock Exchange* kunatoa fursa kwa Watanzania kumiliki hisa pamoja na Wawekezaji hawa, ambapo hilo ni jambo jema. Kamati inaishauri Serikali na Mamlaka husika, kufanya jitihada za makusudi za kuboresha mazingira ya Sekta ya Mawasiliano ili kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokutana na Wadau wakati wa *Public Hearing*, wengi wao walionesha wasiwasi wao kuhusu sheria hii mpya na namna

itakavyoweza kutumika bila kuleta mgongano na sheria nyingine zilizopo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira mazuri kuiwezesha Sheria hii kutumika kwa faida ya wote na hii itasaidia kuyarudisha Makampuni ya Kitanzania yaliyojiandikisha katika *Stock Exchange* za nje ya nchi kujiandikisha *Dar es Salaam Stock Exchange*. Serikali ijizatiti kukabiliana na changamoto zitakazotokana na utaratibu huu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa kuingiza hisa *Dar es Salaam Stock Exchange* bado haujazoleka; na kwa kuwa utaratibu huu pia si mgeni katika dunia ya utandawazi na soko huria (kwa mfano, Malaysia wameandikisha Makampuni zaidi ya 500 katika *Stock Exchange* yao); na kwa kuwa Tanzania inahitaji kukua kiuchumi, kuongeza uwazi, kukuza soko la mtaji na kuwa na utamaduni wa kwenda na mabadiliko ya wakati, elimu ya kutosha bado inahitajika. Kamati inaishauri Serikali iendelee kufanya stadi kutoka nchi zinazotumia mfumo huu, kuzijua changamoto, mafanikio, kasoro, faida na hasara za matumizi ya sheria kama hii. Jambo la msingi ni kuwahakikishia Wawekezaji wa ndani na nje usalama wa fedha zao kwa kuweka mazingira mazuri ya matumizi ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sekta ya Mawasiliano ni huduma muhimu na yenye changamoto (*Sensitive and Complicated*), ikilinganishwa na Makampuni mengine ya biashara za bidhaa, unahitajika umakinna katika uendeshaji wa kila siku ili kuepusha mfumko wa bei. Kamati inaishauri Serikali kujizatiti na kuweka utaratibu mzuri wa utunzaji na uhakiki wa fedha ili kuwafanya Wawekezaji, Watumiaji wa huduma ya mawasiliano, pamoja na taifa zima, kufaidika na kupata haki sawa katika huduma hii. Aidha, Serikali iwatumie Wataalam wake waliobobea katika masuala ya sheria za Makampuni, ambao watasaidia katika kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya sheria na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu. Aidha, nimshukuru pia Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Florens Turuka, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Wataalamu na Watendaji wote wa Wizara walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina wakati wote wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu Serikali, pamoja na Wataalam wake, kwa kutoa ufanuzi wa vipengele mbalimbali vyta kisheria mbele ya Kamati pale ilipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru Wadau wote waliotajwa hapo awali kwa ushiriki wao katika *Public Hearing* na kutoa maoni yao, ambayo kwa namna moja au nyingine, yamesaidia na kurahisisha kazi ya Kamati katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha na kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii; Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana Abdallah Hancha, kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu na kujadiliwa Bungeni. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mawasiliiano ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2010 (*The Electronic And Postal Communication Act, 2009*). Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa mzima wa afya ili kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nachukua fursa hii kutoa pongezi na salamu za mwaka mpya kwa Watanzania wote, kwako wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, kwa kuwezesherwa kuuona mwaka huu wakiwa wenye afya njema. Sambamba na hilo, natoa salamu za mwaka mpya na niwapongeze na kuwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Rukwa hasa wa Jimbo la Mpanda Kati, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipatia katika kutimiza majukumu yangu kama Mbunge. Nichukue fursa hii kuwaomba waendeleze imani yao kwangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi, wakazi na wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Kati, natoa pole kwa familia, ndugu na Wananchi wa Jimbo la Ruangwa, kwa kufiwa na Mwakilishi wao Bungeni; Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, ambaye tulikuwa tukishirikiana naye katika kutekeleza majukumu yetu katika Kamati. Natoa pole pia kwa Wananchi wa Same, Mpwapwa na Kilosa, ambao wamepatwa na maafa ya mafuriko. Vile vile Wananchi wa Wilaya ya Ukerewe ambao waliuawa na majambazi. Wote, Mwenyezi Mungu awape moyo wa ustahimilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa naomba kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa viangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6(2)(e) katika maombi ya leseni, kinaweka sharti la uzoefu wa nyuma katika utoaji wa huduma inayoombewa leseni. Kambi ya Upinzani inaona kifungu hiki kinamnyima haki mwekezaji mzalendo ambaye ana mtaji wa kutosha na wataalam lakini hajawahi kufanya biashara hiyo huko nyuma.

Aidha, kigezo hiki kinalazimisha kuwa mwombaji awe na uzoefu wa nyuma katika kutoa huduma inayoombewa leseni. Kigezo hiki cha uzoefu wa nyuma katika kazi hiyo kinamnyima mwekezaji haki ya msingi ya kufanya biashara na kufunga mlango kwa Watanzania ambao hawana huo uzoefu wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 17 cha Muswada kinasema kuwa matakwa ya leseni ya mtu mmoja mmoja yatahusisha masharti yatakayowekwa na mamlaka. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kinaweza kutumiwa vibaya na Mamlaka, kwani masharti ambayo tayari yamewekwa katika Muswada yanatosha, kama hayatoshi ni bora yawekwe wazi kwenye Kanuni badala ya kutoa nafasi kwa mamlaka kuweka masharti mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18(3) vifungu vidogo nya (a),(g),(h),(i) na (j), Kambi ya Upinzani inaona vinatakiwa viwekwe sawa kwani vimeandikwa kirahisi mno na kupelekea kupotosha maana halisi iliyokusudiwa na kuwa na maana tofauti kabisa. Ili kupata maana iliyokusudiwa ni bora kuongeza maneno *line* katika vifungu hivyo, vingine tafsiri inaweza kuwa makampuni hayo yatoe huduma kama vile gari la zimamoto, gari la kubebea wagonjwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona Kifungu cha 21(c) kinatakiwa kuwekwa wazi zaidi kwani kipindi cha siku 30 ni kwa eneo lote kama leseni ya mtoa huduma inavyotaka au ni katika baadhi ya maeneo tu ama ni jumuisho la ukosefu wa huduma katika baadhi ya maeneo? Hivyo, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri aliweke vizuri suala hili ili wadau na watumiaji nao walielewe.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21(j) kinachosema mwanahisa kuuza hisa zake, kuhamisha hisa au mwanahisa mkubwa kuwa mdogo kulingana na hisa anazomiliki bila ya kupata baraka za mamlaka ni kosa na inaweza kupelekea kunyang'anywa leseni.

Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa umiliki wa hisa ni sawa kabisa na umiliki wa nyumba, mashamba au umiliki wa mifugo na kadhalika. Hii inamfanya mwenye mali hiyo kuwa na uwezo wa kuuza pale anapodhani ni muafaka kwake. Je, ni kwa nini inakuwa kwenye hisa katika tasnia ya mawasiliano tu au inatumika pia kwenye makampuni mengine kama yale yanayozalisha umeme, gesi na kadhalika? Kama kifungu hiki ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, Kambi ya Upinzani inashauri kiwekwe kwenye Sheria ya Usajili wa Makampuni ili wanaotaka kusajili makampuni wafahamu sharti hili mapema kabla ya kuingia katika biashara.

Mheshimiwa Spika, Vifungu nya 26(3) na (4) vinawataka wale wote wenyewe leseni kwa mujibu wa Muswada huu kuwa baada ya miaka mitatu ya kufanya biashara inawalazimisha wajandikishe kwenye Soko la Hisa. Kambi ya Upinzani baada ya kuviangalia kwa undani vifungu hivi inaonesha kuwa sheria inawagawa wawekezaji; kwa nini wawekezaji wa Sekta ya Mawasiliano tu baada ya miaka mitatu ya biashara ndio walazimishwe kusajili hisa katika soko? Kambi ya Upinzani inapendekeza sheria zinazotawala Soko la Hisa lazima zizingatiwe na muda usiwe kigezo.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji wapo katika sekta nyingi, mojawapo ni wale waliomo katika Sekta ya Madini; kwa nini nao wasilazimishwe kujiorodhesha katika Soko la Hisa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa makini katika utungaji wa Miswada, isiwe ni kwa ajili ya kulibana kundi fulani kwa sababu wanazozijua wao; haya ni makosa, hivyo basi kama ni lazima vifungu hivyo viwepo basi viwepo kwa wawekezaji wa sekta zote za uchumi.

Kambi ya Upinzani haifurahishwi kuwa na sheria za ubaguzi. Aidha, tumeshindwa kujua dhamira ya kuondoka katika umiliki binafsi na kutaka kuwa wa umma kwa sababu tu ya kushindwa kusimamia ipasavyo sekta binafsi na kupoteza fedha nyingi kama kodi. Tunashauri ni vyema tukajipanga vizuri, sera nzuri na utekelezaji wake kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, vifungu vya 25 na 26 vya Muswada huu vinakinzana na matakwa ya Katiba yetu; Katiba inazuia kutungwa kwa sheria ambazo zinaonesha au kwa kuweka sharti lolote la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake. Naomba kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), Ibara ya 13(2): “Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.”

Kwa msingi huu basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutazama upya sheria inayounda DSE ili iweke vigezo wazi kwa makampuni yanayotakiwa kujisajili na *Dar Es Salaam Stock Exchange* na kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo ili kuepuka mgongano wa kibaguzi unaoweza kujitokeza kutokana na matakwa hayo ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 40(1) kinaongelea kuhusu mamlaka, kusimamisha au kufutwa kwa matumizi ya leseni ya posta, wakati kifungu cha 40(2) kinatoa nafasi ya rufaa kwenye Tume ya Ushindani (*Fair Competition Tribunal*). Kambi ya Upinzani inauliza inakuwaje kwa wenyewe leseni za *electronic communications* nafasi yao ya rufani ni Mahakama Kuu na kwa kutumia utaratibu wa kimahakama? Tunahitaji kupata maelezo ya kutosha juu ya taratibu za rufaa kuwa tafauti na haki kutolewa Posta na kunyang’anywa kwa mawasiliano ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 75(1), (2) na (3) vinamtaka mwenye leseni za matumizi ya masafa kuweka amana, yaani *deposit* ya zaidi shilingi ya bilioni moja au hatifungani za mali zake kwa hasara inayokisiwa kusababishwa kwa mamlaka au kwa mtu mwagine yeyote. Kushindwa kuweka *deposit* hiyo ni kosa.

Kambi ya Upinzani inaelewa umuhimu wa leseni ya matumizi ya masafa kwa taifa, lakini sheria hii isitungwe kwa misingi ya kukomoana bali itoe haki. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuwa, kifungu hiki kinakwenda kinyume na Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nanukuu: “Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.”

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 78(7) kinasema kuwa, masafa yatatolewa kwa njia ya zabuni au kwa bei maalum itakayowekwa na mamlaka. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, itakuwa si haki kutoa masafa kwa njia ya zabuni kwani ni wazi kuwa *principles* za zabuni ni kwamba, mwenye bei kubwa (*Highest Bidder*) ndiye atakayepata. Hili linaweza kusababisha wafanyabiashara kuanzisha ulangizi wa masafa baada ya kujilimbikizia masafa bila wao kuyatumia. Hivyo basi, jukumu la kutoa masafa liwe ni kwa mamlaka ambayo itaweka bei maalum.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 126 kinachosema kuwa mtu yejote anatakayeingia kwenye mfumo wa *computer* na kusababisha madhara yoyote atakuwa ametenda kosa; Kambi ya Upinzani inataka maelelezo kwani kila kampuni au asasi ina mfumo wake wa *computer* inaouelewa; sasa hapa itakuwaje kwa Mamlaka kuweza kudhibiti au mpaka wapewe taarifa kuwa asasi fulani mfumo wao wa *computer* umeingiliwa? Tunaomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 133 cha Muswada kinachosema kuwa mtu yejote atakayetumia *Sim Card* ambayo anajua kuwa haikusajiliwa baada ya muda wa kusajili kumalizika, basi ametenda kosa na adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi milioni 1.5. Kambi ya Upinzani inaona hapa tunaanza kuwadhalilisha Watanzania, kwani mathalani Mkulima wa Tumbaku kule Inyonga au Urambo Vijijini, ambapo mapato yake baada kuuza tumbaku kwa msimu hata hayafiki shilingi milioni moja; hapa kweli tunataka kumsaidia Mtanzania kwa kumrahisishia maisha yake? Kifungu hiki kifutwe kwani kitaleta usumbufu kwa Watanzania maskini, makampuni yasimamishe *sim card* zote ambazo zitakuwa hazikusajiliwa na wala zisitumike ili watu waweze kupata hizo *fine*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwapongeza ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuun pamoja na timu nzima ya Wataalam wa Wizara na asasi zake, pia wadau wote walioota michango yao kwa Muswada huu. Kambi ya Upinzani inaamini Muswada huu utakuwa na manufaa kwa taifa na tunaunga mkono hatua ya kuwanyang'anya masafa yaliyohodhiwa kwa malengo ya kujinufaisha ili yaweze kutumika sasa kwa kuongeza huduma na ushindani wa biashara kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Ukikaa hapa Mezani basi unafurahi kweli, unaweza ukasikiliza maneno *conclusion* haifanani na maneno ya katikati, basi sisi ni wa kusikiliza tu.

Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada ni wa siku nzima lakini mpaka sasa walioomba kuchangia ni wawili tu, kwa hiyo, kwanza nitamwita Mheshimiwa Godfrey Zambi na atakayefuata ni Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta ya Mwaka 2009 (*The Electronic and Postal Communication Bill, 2009*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama kwa mwaka huu wa 2010, naomba nichukue nafasi hii, nitoe kheri kwa Watanzania wote na hususan Wananchi wa Mbozi Mashariki, ambao mimi nawawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nichukue nafasi hii nilete salamu za Wana-Mbozi kwa Serikali kwa ujumla hususan Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo, kwa kukubali ombi lao la kutokuwapelekea mbolea ya Minjingu. Walinipa salamu niwaletee kwa sababu mwaka huu baada ya kupata mbolea ya DADP wamezalisha vizuri na mahindi yao yanaendelea vizuri sana mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Naibu Waziri Dkt. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Dkt. Florens Turuka, Wataalamu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, ambao walihusika katika maandalizi ya Muswada huu na kisha kuufikisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kama tulivyoambiwa, kwanza, naomba *ni-declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ambayo imehusika katika kuupitisha Muswada huu na ninaomba niseme kwamba, nakubaliana kwa asilimia mia moja na maoni yaliyotolewa na Kamati kama yalivyosomwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada huu kama alivyosema Waziri na sisi kwenye Kamati kwamba, Sheria hii inalenga kudhibiti matumizi mabaya ya simu, wizi wa simu, utunzaji wa maadili, pamoja na mambo mengine mengi ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Waziri. Kwa ujumla, mimi naiona Sheria hii kwamba ni nzuri na sisemi kwamba pengine imekuja wakati muafaka, nadhani imekuja kwa kuchelewa, kwa sababu hizi kampuni zimeanza zaidi ya miaka 10 iliyopita lakini leo Sheria kuja siwezi kusema kwamba zimekuja wakati muafaka, lakini tuishukuru pia Serikali kwa kuliona hilo na kuleta Sheria hii sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo moja kwa sehemu kubwa kwa sababu maeneo mengine yanaelewaka na hayana utata kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu ambalo linaonekana limekuwa na utata na mwenzangu wa Kambi ya Upinzani ambaye pia ni Mjumbe mwenzetu kwenye Kamati ya Miundombinu, ndugu yangu Arfi amelisemea sana ni fungu la 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tumekuwa na uwoga, tunatunga Sheria hii kwa mara ya kwanza na kifungu hiki cha kutaka makampuni *ya-list shares* zao kwenye

*Dar es Salaam Stock Exchange* ni jambo ambalo linafanywa kwa mara ya kwanza, kwa hiyo, watu hawakosi kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka tuwe na utamaduni wa kutaka mali za Watanzania ziwafaidishe Watanzania wenyewe. Sioni hofu tunaposema kwamba, makampuni yote yaorodheshe *shares* kwenye soko la hisa, makampuni mengine tayari *yalisha-list shares* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* hata kabla ya kulazimishwa na Sheria yoyote; kwa nini watu wengine au makampuni mengine yawe na wasiwasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tumekuwa na wasiwasi na wakati mwingine tukizungumzia hali hii watu wanaona kama tunalenga kampuni moja au Taasisi moja, jambo ambalo si kweli, tuna makampuni mengi ya simu katika nchi hii, makampuni yote haya yanaambiwa *yaji-list* kwenye soko la hisa na faida za makampuni haya kujiorodhesha kwenye soko la hisa tunazijua.

Moja, Watanzania wengi pia watafaidika kwa maana ya *shares* hizo, lakini pia Serikali itapata kodi sahihi kwa maana ya kwamba kutakuwa na *scrutiny* ya kutosha wakati makampuni haya *yanapo-list shares* zao kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*, kuliko huko nyuma; na faida hiyo kubwa inayafanya makampuni haya sasa yakaguliwe kwa kufuata Kanuni za Kimataifa zinazokagua makampuni haya. Sasa yanakuwa na wasiwasi kwa sababu faida yao itajulikana moja kwa moja; mapato yao yatajulikana moja kwa moja, jambo ambalo wasingepeenda wao lijulikane na mimi sioni shaka kwa nini tufanye biashara ya kifichoficho. Hela hizi zinazalishwa Tanzania, lazima tuone Serikali inafaidika na kupata kodi sahihi ili Watanzania pia tuweze kufaidika. Hii pia ndiyo hofu yao kubwa. Moja ya faida ya makampuni haya *ku-list shares* zao kwenye *Dar Es Salaam Stock of Exchange*, kupata punguzo la *corporate tax* kutoka 30% kwenda 25%; wanapata faida hiyo lakini wanaona faida hiyo ni ndogo ukilinganisha na fedha wanazozalisha bila kupitia kwenye Soko la Hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema, kama makampuni haya haya ambayo yanaonekana kutaka kugoma *ku-list shares* zao kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* *yame-list* kwenye *Ex-Stock Exchange* za nchi nytingine; kwa nini yaogope *ku-list* hapa Tanzania? (*Makofi*)

Kwa hiyo, Tanzania inaonekana ndiyo shamba la bibi la makampuni kuvuna lakini wakalie sehemu nytingine! Jambo hili mimi nadhani kama Watanzania tusilikubali, tusimame na Sheria kwamba lazima *wa-list* ili Serikali iweze kupata kodi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hili ninaomba nisisitize kwamba, tusikubali na twende na maoni ya Kamati na Wabunge wenzangu wenyewe kuitakia nchi yetu mema wasimame na ushauri wa Kamati kwamba, Sheria hii ipite ili Serikali iweze kufaidika na makampuni haya kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Tuliambiwa na Wataalamu tulipokaa kama Kamati kwamba, Serikali haikukurupuka kuja na Sheria hii au kuja na Muswada huu; ilifanya utafiti mahali pengine na kama Kamati tuliambiwa bayana; kwa mfano, nchi kama ya Malaysia *ime-list*

makampuni zaidi ya 500 kwenye soko la hisa la nchi yao ambalo linaitwa BURSA; lakini sisi Tanzania tume-*list* makampuni ya Kitanzania 11 na 4 kutoka nje ya nchi na mimi nikawa najiuliza tumechelewa tulikuwa wapi? Sidhani kama Sheria hii au Muswada huu unakuwa wa ubaguzi kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani alivyosema; Sheria hii inahusu Mawasiliano ya Elektroniki na Posta, kwa hiyo utazungumzia makampuni ambayo yapo chini ya Wizara ya Sekta hii.

Makampuni mengine yatahusu Sheria zitakazotungwa kwenye sekta husika, sidhani kama Sheria hii ingeweza kuzungumzia makampuni mengine ambayo hayako chini ya sekta hii.

Kwa hiyo, nadhani tungeishauri Serikali, jambo ambalo pia kwenye Kamati tuliridhishwa kwamba, Sheria nyingine zinazohusu uwekezaji, kwa mfano, Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya Makampuni na Sheria yenyewe ya Soko la Hisa, ziliangaliwa vizuri kuhakikisha kwamba, makampuni yote mengine yanayohusu kujisajili kwenye Soko la Hisa basi yanafanya hivyo. Kwa hiyo, sitaki kumsemea Waziri, lakini nina hakika asingeweza kusemea makampuni mengine, ila makampuni ambayo yako chini ya Wizara hii, jambo ambalo Mheshimiwa Waziri nadhani amelifanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nisemee kifungu hicho ambacho wenzangu wameonekana kuwa na wasiwasi, kama nilivyosema naomba tuutoe tupitishe Sheria hii ili iweze kufanya kazi. Kwa kumalizia nasititiza kwamba, Wabunge wote tukubali Muswada upite iwe Sheria ili makampuni ya-*list shares* zao kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ili sasa kuwe na uwazi zaidi kwenye mapato yanayotokana na makampuni haya ili Serikali iweze kupata pesa zinazostahili zaidi.

Mheshimiwa Arfi anaposema kwamba, tunalazimisha makampuni ku-*list shares* kwa sababu tumeshindwa udhibiti, mimi sidhani kama hilo ni sahihi sana; kama kuna njia ya wazi zaidi ya kufanya makampuni hayo ya-*list* kwa nini tuwe na wasiwasi wa kwamba Sheria hii inakuwa ni ya ubaguzi; sioni kama Sheria hii inakuwa na ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niliona nisimame kama Mjumbe wa Kamati kusositiza yale ambayo tumekubaliana kwenye Kamati na imekuwa jadi tu kwamba, tunakubaliana kwenye Kamati lakini kwa sababu kaka yangu Mheshimiwa Arfi yuko Kambi ya Upinzani, inabidi aseme yale ambayo ameyasema, ingawa tulipokuwa kwenye Kamati hakuyasema hayo aliyoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Ukitsema mbwa kauma mtu mbona siyo tatizo, lakini mtu kauma mbwa ni hoja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ponsiano Nyami ndiye msemaji wetu anayefuata.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili nami nichangie kidogo katika baadhi ya maeneo ambayo nadhani ni muhimu kuyachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nitoe pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ya kuuleta Muswada huu na pia kuziunganisha hizi Sheria za Mawasiliano na Posta kuwa pamoja. Napenda pia kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote walioshiriki katika mchakato huu bila kusahau Kamati iliyohusika na mchakato mzima wa kuufanya Muswada huu uwe mzuri na baadaye uwe Sheria; ndiyo maana umekosa wachangiaji kwa sababu naona umeboreshwa vizuri. Kwa hiyo, natoa pongezi za dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Serikali ijitahidi kwa njia ya pekee kabisa kuisaidia Posta ili iweze kujiimarisha yenewe na kusimamia yenewe utendaji wake wa kazi kwa sababu Posta ni muhimu popote duniani. Katika Taasisi ambazo ni muhimu duniani Posta huwa inawekwa, lakini kwa upande wa Tanzania naona kama Serikali imeisahau, wakati ule ilipokuwa imeungana na TTCL ndipo ilionekana angalau kuna ahueni lakini kwa wakati huu ambapo TTCL iko peke yake na Posta iko peke yake, Posta inaonekana ni kama haina kazi na hata Serikali hajajali kuipatia mikopo au fedha ili iweze kusimamia vizuri zaidi. Kwa maana hiyo, unakuta tegemeo lao la kusafirisha vifurushi au kutegemea masanduku ya barua ambayo ni machache nchini, hatuendani sambamba na idadi kubwa ya mamilioni ya Watanzania tuliopo. Hali hii inawafanya wasiwe na uwezo mkubwa wa kupata pesa za kujiendesha na vilevile kutoa gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba katika Sheria hii wawawezeshe zaidi ili kwa kushirikiana pengine na makampuni mengine, waweze kuweka anuani za utambuzi katika maeneo yote ya miji, vijiji ili wananchi wote waweze kupata huduma ya mawasiliano kwa urahisi zaidi. Vile vile isisahau kuhakikisha kwamba, watumishi wake wanapewa mafunzo ili waendane na wakati wa Sayansi na Teknolojia tulionao.

Nikienda upande wa mawasiliano, ninaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wa kutaka makampuni haya yaweze kujirodhesha katika soko la hisa. Nami pia naomba nitofautiane na ndugu yangu Mheshimiwa Arfi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ambaye anasema kwamba, Serikali au Sheria inataka kutungwa kwa maana ya kukiuka katiba eti kwa kuwalazimisha hawa wawekezaji katika kujiunga kwenye soko la hisa; haibagui!

Sheria isingeweza kuweka hivyo ingekuwa inawabagua Watanzania amba kwa mujibu wa Sheria tulizoweka, tunataka Watanzania wafaidi. Kwa hiyo, tunapoweka Sheria halafu tunasema kwamba, ni vizuri makampuni yajiingize katika soko la hisa, mwenzetu unasema kwamba Sheria inataka kuwalazimisha na hivyo inavunja Katiba siyo kweli. Kutokufanya hivyo ni kuvunja Katiba, kwa sababu Watanzania amba ndiyo wenye nchi na ndiyo watumiaji wakubwa na ndiyo wachangiaji wakubwa, wao hawafaidi zaidi na kwa hiyo huko ni kuwanyanyasa na kuwabagua Watanzania siyo kubagua makampuni.

Kwa hiyo, mimi natofautiana kabisa na ye ye alipojaribu kutaja vifungu ambavyo vinahusika kama vile kifungu cha 26(3) na (4) na vilevile kifungu cha 13(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si kweli.

Watanzania wameanza kuelimika katika kuweka hisa na Elimu ambayo inatolewa kila siku ndiyo inayowafanya wengi waingie katika uwekaji wa hisa zao kwenye soko. Kwa taarifa tu makampuni haya ya simu katika eneo ambalo wanakusanya pesa nyingi sana ni katika eneo la mawasiliano yenye. Pesa ni nyingi mno, achana na huku wanakouza hizi *air time* au *voucher* au simu zenye.

Eneo ambalo hawalipii kodi ni hilo la mawasiliano yenye tunaloongea na ndiyo maana utaona makamapuni mengi siku hizi yanatudanganya; mara wakuwekee *messages* kwamba umepewa *messages* zinafika mpaka 300 au 400 lakini zitakwisha baada ya siku mbili, hii ni danganya toto! Pia wanakupa ofa tunajirusharusha kwa 500, sijui cheka time. Zain wana jirushe kwa 2000 utaongea siku nzima au 200 mwisho saa 12 au saa 11; hii ni kudanganya tu lakini katika eneo hilo wanapata *billions and billions of money* ambayo hawalipii kodi na ndiyo maana wanakuwa wakali. Mimi sisiti kusema kwamba, walijitahidi sana hawa wenye makampuni, kuhakikisha kwamba wanajaribu hata kuwazengea (*lobbying*), baadhi ya Wabunge ili wawatetee katika azma yao ya kukataa kujiunga katika soko au pia katika kujiandikisha huko, wengine wametoa hata pesa; sasa watakuzengea bila kukupa pesa bwana? Wanajua kwamba, katika eneo hilo Watanzania watafaidi na kwa Tanzania Watanzania wengi wanatumia simu za mkononi.

Ukienda vijijini; wakulima na wafugaji wana simu za mkononi; ukienda mashulenzi wanafunzi hasa wa sekondari na vyuo mbalimbali takriban kila mmoja ana simu ya mkononi. Kama vile haitoshi, ukienda katika maeneo mbalimbali ya huduma kwenye baa na maeneo mengine ya kawaida tu kwa kina mama lishe na kwingineko wanatumia simu za mkononi. Simu hizi zinatoa faida kubwa mno kwa hawa wawekezaji na kwa hiyo kitendo cha wao kujiunga katika soko la hisa kama alivyosema Mbunge aliyetangulia, maana yake ni kwamba mapato yao yataanza kujulikana na kwa maana hiyo watalipa ushuru mzuri tu kwa Serikali amba leo hawalipi wanaona mapato yao yatakuwa ya chini wanaona bado waendelee kumnyonya Mtanzania.

Kuna Kiswahili kinasema “tumgidie bwege”, yaani wamlie huyu mtu asiyejua. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na kifungu ambacho kinasema ni lazima hawa watu kwanza waandikishwe lakini pia ni lazima wajilingize katika hilo wala hatuna haja ya kuogopa.

Kuhusu simu za mkononi kwa wananchi wote amba wanansikiliza hapa; ni muhimu sana kwenda kuzisajili hizo simu za mkononi. Kuisajili simu yako ya mkononi ni faida kwako, zipo faida nyingi lakini angalau mbili, tatu ninaweza nikazisema; kwa mataifa yaliyoendelea yote unapokwenda kule ni lazima *line* yako uisajili tena huchukua siku mbili au tatu ndipo wanakusajili. Watakuuliza eneo unalokaa na kila kitu, lakini faida yake ni kwamba, endapo simu yako itaibiwa, simu hiyo itasitishwa; na kama mtu mwingine ataamua kuchukua *line* yake na kuiingiza kwenye simu yako iliyoibiwa,

itajifunga lakini pia itajionesha kwenye mitambo kwamba simu ile ilioibiwa, ile line ilioingizwa ilikuwa ni ya nani. Pia ni vizuri ukaitunza simu yako hiyo na usiwe na mazoea ya kuwapatia watu kwa sababu kama simu yako itatumika kwa ajili ya matusi au meseji mbaya ambazo zitarekodiwa katika mtambo kule, itaonekana wewe ndiye umetenda makosa hayo na kwa maana hiyo ni lazima kuwa makini na utunzaji wa simu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia watu wanaweza wakatumia simu yako kufanya shughuli za ujambazi, utahusishwa kwamba wewe ndiye uliyeshiriki katika mipango hiyo ya kuwafikisha watu wafanye uhalifu huo. Vile vile endapo utatukanwa itajulikana ni nani na yuko wapi aliyefanya hujuma hiyo ya kukutukana, kwa hiyo, utakuwa na uwezo pia wa kuweza kushtaki na kupata haki yako, kwa sababu utakuwa umekwisha *register* na kila kitu kitakuwa kimekwishaonekana ni nani aliyekufanya hujuma hiyo. Kwa hiyo, wananchi ambao wanaogopa kwenda kusajili hizo simu wakazisajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utoaji wa adhabu, nilikuwa nadhani adhabu ni kubwa sana ingepunguzwa na kwa hiyo uwepo utaratibu wa kwamba, endapo mtu ataamua kutumia *line (chip)* kwenye simu ambayo si yake labda imeibiwa na kadhalika, simu hiyo ijifunge mara moja na ikatae kutoa muunganisho wa mawasiliano; ijikate yenewe utaalamu huo upo na unatumika nchi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia adhabu hiyo itolewe na sioni sababu kwa nini itolewe! Unaposema atakayekuwa amechelewa kujandikisha kwa sababu wengine watajiunga wakati huo ambao hawajanunua simu, leo Sheria itakapokuwa imepita na hata baada ya miaka kuendelea, wengine wataendelea kununua simu; sasa unampa adhabu ya nini? Kwa hiyo, sioni sababu kwa nini apewe adhabu, wengine watapoteza simu na watakaa muda mrefu pengine kutegemeana na mazingira ya pale alipo halafu atakapokuja kutaka ku-*register* simu yake iliishapotea zamani; unampa adhabu ya nini?

**NAIBU SPIKA:** Tayari umemaliza dakika zako.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nilikuwa sijasikia kengele, naomba msamaha. Naunga mkono hoja hiyo, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Okay. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Charles Kajege atafuatia; bahati nzuri wako wengi hawa sasa hivi tutafika mpaka saa saba. Tafadhalii Mheshimiwa Mnyaa, atafuata Mheshimiwa Charles Kajege, halafu Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa akifuatiwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie mada iliyopo mbele yetu. Jambo la kwanza, ningependa kutumia dakika chache kwa ajili ya ufanuzi mdogo. Vile vile

napenda kuipongeza Hotuba ya Maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa jinsi ilivyofafanua vifungu vyote ambavyo vinaleta utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, katika kufafanua hilo, katika hili suala la usajili wa DSE, haya makampuni ambapo Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisisitiza kwamba, Ibara za 25 na 26 za Muswada huu zinakinzana na ukiangalia vizuri kweli zinakinzana. Lengo siyo kwamba, hatuhitaji haya makampuni kujisajili kwenye DSE, tunapenda sana na tunajua kuna faida kubwa ya mapato; lakini alichokusudia Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni kwamba, hii Sheria isiwe ya kibaguzi na hiyo ni kwa mujibu wa Katiba yetu. Halafu tuangalie ile *conclusion* yetu ni kwamba, ni kupata *harmonization* ya hizi sheria; *idea* siyo kupinga ni kwamba, *harmonization* ya Sheria zetu iwepo kwanza na pasiwepo na Sheria ya kibaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika Muswada huu ambao napenda kupongeza ni katika kifungu cha 106 kinachohusiana na *Code of Conducts*. Kwa kweli nimefurahishwa sana na kifungu hiki hasa kutokana na udhibiti wa matangazo; ni jambo la msingi kufuata maadili na tukawa na udhibiti wa matangazo na yale matangazo ambayo yanakinzana na maadili yetu ni vyema yadhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kuweka angalizo, isije kikatumika kifungu hiki na kanuni ziwekwe vizuri, tuweke matangazo ambayo yanatoa elimu kwa mfano, matangazo ya Haki Elimu. Kwa hiyo, kifungu hiki kisije kikatumika kuzuia matangazo ya namna hiyo. Yazuwe yale matangazo ambayo yanaleta maadili machafu kwa jamii ya Kitanzania, maadili ya kigeni ambayo hayaendani na silka na mila zetu, hicho kitumike kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo sikufurahishwa kwamba, katika Muswada huu hazijaelezwa athari za simu za mkononi kwa watoto wadogo. Tuna matatizo katika jamii zetu hasa kwa watu wenye kipato, ambapo tayari mtoto wa miaka tisa, miaka minane au miaka kumi anapewa simu ya mkononi, akiwa na matatizo shule ampigie Baba au Mama; kuhusiana na hili Muswada huu haujaonesha na hili ni tatizo, ni lazima uwepo udhibiti wa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa sote tunashuhudia na maelezo mengi yanatolewa mpaka ndani ya Bunge letu kuhusu viwango vya elimu hasa masomo ya Sayansi na Hisabati, watoto kudondoka kimasomo, tunapoteza taifa na mambo mengine yanayochangia, mojawapo ni hizi simu za mkononi. Leo unampa mtoto simu ya mkononi, katika umri mdogo atawezu kushughulikia mambo mengi yaliyomo na simu nyingine ni kubwa, zina mambo mengi sana ya kidunia, mtoto yule anashughulika na yale sana kuliko akili yake kuipeleka katika masomo na mambo mengine. Kwa hiyo, Muswada huu pia ultakiwa ueleze vitu kama hivi na pawe na udhibiti kama huo na siyo udhibiti wa matangazo tu, lakini na udhibiti kwa watoto wadogo kupewa simu ambapo wanapoteza kumbukumbu za mambo mengine na kuwa *interested* na mambo ambayo hayafai. Kwa hiyo, hilo ni la pili ambalo nilitaka kulizungumzia na ambalo nimeona kama ni kasoro kwamba, halimo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu na lazima niupongeze Muswada huu ni katika miundombinu ya minara kuleta ushirikiano na udhibiti wa miundombinu ya minara. Kusema kweli ni lazima nipongeze kwa sababu inaonekana sasa ile hasara au matatizo ya uzuri wa nchi yetu, ile *Flora and Fauna* inavyopotea kwa kukuta minara sita, saba, kila baada ya maeneo na tuwapongeze vilevile kampuni za Zantel na Vodacom, ambao wameonesha mfano huo mwanzoni kabisa kabla Sheria hii haijakuwepo. Sasa kuwepo kwa Sheria hii ni vizuri haya makampuni mengine mambo ya minara kuchomoza kila mahali yadhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kule mijini hasa katika mawasiliano ya TV, lazima tuwapongeze wanaoleta hizi *cables* kwa kuondoa *butterflies* kila wakati; kila nyumba kuna hizi *butterfly antenna* pia inaondo *Flora and Fauna* ya mji. Kwa hiyo, kwa Sheria hii sasa nafikiri makampuni yanayotaka kuingia ni vyema washirikiane minara na makampuni mengine katika miundombinu hiyo ili kupunguza ucharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo alilizungumzia Mheshimiwa Nyami hapa linahusiana na matangazo katika simu na hizi *offers* zinazotolewa mara kwa mara. Matangazo haya, huu ushindani umekuwa mkubwa, inasikitisha kuona TICRA bado wanashindwa kudhibiti kwa sababu *offers* zinazotolewa na *time* inayotumika na wewe ukiwa unafuatilia *uta-set* ile simu yako, basi utakuta kuna udanganyifu mwangi mno na hili ni tatizo la TICRA kwamba, hakuna udhibiti wa masuala haya. Kwa Sheria hii, nafikiri sasa hivi itasaidia kwa sababu wanajua kabisa watumiaji wa simu walio wengi hawawezi kufuatilia muda walotumia, japo muda unaji-*record* kwenye simu, lakini ukifuatilia matangazo yao na ukija ku-*check* ule muda haviendani. Kwa maana hiyo, kwa Sheria hii tunaomba TICRA iwe inadhibiti vizuri ili wananchi wasidanganywe, ikiwa wao watajaribu ku-*maximize profit* iwe ni *profit* halali siyo katika kuwanyang'anya na kuwadhulumu wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu mdogo, nashukuru sana. Ahsante. (*Makofit*)

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu hapa. *It is a timely intervention* ambayo ni nzuri. Mimi nina yafuatayo katika Ibara zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Ibara ya 12, ukurasa wa 12; Ibara hii inazungumzia *grant of licence*. Nilikuwa nafikiri kwamba, vilevile ni vyema tukaweka *time frame*, yaani muda wa kupokea maombi hadi muda wa kutoa leseni kwa sababu inaonekana hapa iko *open ended*. Kwa hiyo, ni vyema tutaweka huo muda ili tuweze kuwa *more efficient*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu katika Ibara ya 19, ukurasa wa 25 - *Renewal of an Individual Licence* hapa wanasema: “The Authority shall renew an individual licence

*for a term to be agreed between the Authority and the licensee concerned.”* Mimi naona kuna tatizo hapa. Nafikiri ni vyema tukakubaliana kwamba, muda wa kuongezwa uwe ni kiasi gani badala ya kutegemea maongezi baina ya *authority* na *licensee*. Hii itasaidia sana kuepusha upendeleo na matatizo mengine madogo madogo yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika Ibara ya 26(3) inasema: “*Every licensee shall, within three years from the commencement of this Act, and in accordance with requirements of the Capital Stock Market and Securities Act, be required to list local shares with the stock market.*” Mimi nashauri kwamba, kuji-list kwenye *Stock Markets* kusiwe Sheria isipokuwa Shirika lenyewe likishatimiza masharti ya *Capital Stock Market* na likiona kwamba, kuna faida ya kufanya hivyo, lijiunge lenyewe bila ya kulazimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Ibara hiyo hiyo ya 26(4) inasema: “*In disposing of local shares listed or registered with the stock market, the licensee shall sell the local shares to the Tanzanians in accordance with procedures prescribed in the Regulations.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naona tunakwenda kinyume na mikataba mengine ambayo tumeisaini. Kwa mfano, Mkataba wa *East African Common Market*, ambao unaruhusu Wananchi wote wa Afrika Mashariki kuweza ku-trade na ku-cross list makampuni. Sasa tukisema katika hili ni Watanzania pekee ndiyo waweze kununua, nafikiri tutakuwa tunakwenda kinyume na mikataba mengine ambayo tumesaini, hilo naomba nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika Ibara ya 31(2)(b) inasema: “*Not contain discount that unreasonably prejudice the competitive opportunities of other licensees providing applications services and content applications services to the public.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata tatizo hapa, katika biashara *competition* iko ya aina nyingi. *Competition* katika *prices* ni mojawapo. Bei za bidhaa, pamoja na mambo mengine, hutegemeana na teknolojia ambayo unatumia na mambo mengine; sasa tukisema kwamba kama kuna *price war* tuweke Sheria ili bei zisipungue, tutakuwa hatuwatendei haki hata walaji wenyewe. Pamoja na mambo mengine, kazi ya Bunge ni kutunga Sheria ambayo itasaidia walaji wapate *products* au *services* katika bei ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sisi tungeangalia uwezekano wa kuondoa *cartels*. Kwa mfano, kama kuna *cartels* ambazo zinataka ku-tilt *business playing field in their favor* tuweke sheria, lakini kama ni *normal price competition* nafikiri tusiweke Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia tena katika Ibara ya 92(2)(a) inasema: “*A consumer whose mobile telephone has been stolen, lost or damaged shall report to the Network Service Licensee.*” Hapa kama imekuwa *stolen* sina tatizo, kama imepotea sina tatizo lakini kama iko *damaged*, kwa mfano, imeharibika kiasi kwamba, imesambaratika kabisa na hakuna uwezekano wa kufanya tena kazi au mtu akai-assemble tena, sioni umuhimu wa mwenye hii simu alazimishwe kwenda kuripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Part VI, Ibara ya 118 inashughulikia *Offences relating to electronic communications*. Kwanza, niseme tu kwamba, *penalties* hazilingani na *offences* zenyewe; kwa hiyo, nilikuwa nafikiri katika Ibara ya 118(1), hii *fine ya three thousand dollars* ni ndogo sana. Huyu ni mtu ambaye ana- *install*, *ana-operate*, *ana-construct*, *ana-maintain*, *ana-own* na *ana-make available networks facility*. *Network facility* maana yake anahudumia wateja wengi, faini ya dola elfu tatu naona kwamba ni ndogo sana, nafikiri tungeweka hata *five hundred thousand dollars* kwa sababu nia ya faini siyo kwamba, hawa watu wapigwe faini, nia ya faini ni kuondoa zile *incentives* ambazo wahusika wanaziona mle ndani. Nina hakika kwamba, mhusika akiona kwamba, faini ni kubwa kuliko mapato ambayo angepata hawesi kujihusisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, ni vyema tukaweka hapa faini kubwa ambayo itamfanya huyu mtu aogope hata kuanza. Hiyo ni pamoja na 118(2) mpaka Ibara ya 119(1) na nafikiri na sehemu nyingine mbele huku kuna sehemu za *penalties*, wangeweza ku-review waone kama *penalties* zinazowekwa zinalingana na makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 120(a) inasema: “*By means of any network facilities, network services, applications services or content services, knowingly ...*” Tukiishaweka *knowingly* litaleta matatizo sana, anaweza kusema sikufahamu lakini Wanasheria wanasema *ignorance of the law is not a defense in the court of law*. Sasa na sisi tusiweke vitu vingine ambavyo vinapingana na Sheria ambazo zinafahamika. Nafikiri hili neno *knowingly* liondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ni Ibara ya 128, hapa naona kidogo hii faini inakuwa kubwa sana; inasema: “*Any person who is found in possession of any mobile telephone or SIM - card in regard ...*” ukiangalia sasa hapa ndiyo nimesema kwamba, *penalties* hazioani na *offenses* ambazo zimefanywa. Hapa katika maeneo mengine hasa vijijini, mtu anaweza akajikuta anaingia katika tatizo kama hili, lakini tuangalie na *value* ya simu yenyewe, huwezi ukai-*value* katika *five thousand dollars*, simu nyingi ambazo tunatumia hapa Tanzania haiwezi ikaenda mpaka kwenye *five thousand dollars*. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, watu wengi watakuwa *victimized* hapa na watalipa gharama kubwa sana kwa kitu ambacho ni kidogo sana. Nilikuwa nafikiri kwamba, ingeweza kushushwa hata ikawa *a thousand dollar* au *even two thousand dollars*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika Ibara ya 137, ukurasa wa 79; “*Tempering with blacklisted phones*” anasema; “*Any person who physically electronically tempers with any blacklisted mobile telephones, commits an offense and shall be liable on conviction to a fine o one thousand US dollars*. Hii *one thousand dollar* naona ni ndogo sana; nafikiri iongezwe ifikie hata *even ten thousand dollars* na hiyo ni pamoja na ukurasa wa 80, Ibara ya 141 nayo nafikiri kwamba ile *three thousand dollars* ni kidogo ingeongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuchangia, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipatia nafasi angalau na mimi nichangie machache na kwa sababu ya kuheshimu Kanuni za Bunge, sitarudiarudia yale ambayo yamekwishazungumzwa maana mengi yamezungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono sana hoja ya Muswada huu na ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali. Mimi nasema kwamba, Muswada huu umeletwa hapa kwa wakati muafaka, kwa sababu kwanza tulipuruliwa, tunaangalia nini tunachoendelea nacho na makampuni yanaendelea na nini, lakini matokeo yake Serikali imetumia busara kuuleta Muswada huu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwapongeza Mawaziri wawili; Waziri na Naibu wake, utakumbuka mwaka juzi niliuliza swalii hapa Bungeni kuhusu *interruption* tunayoipata kwa kuletewa *messages* za mapenzi na watu ambaao hatujui; na nikailiza kwamba, je, ndoa zetu zikiharibika nani atakuwa na dhamana ya kuyatatua matatizo ambayo yanatukuta nyumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani utakubaliana na mimi kwamba, simu za Wabunge na Mawaziri, hazina siri, nambari zetu siyo siri kabisa. Sasa hivi watu wanaangalia kwenye TV tunaposimama kuzungumza na si ajabu baadae nikaletewa *message*; wakituona wanaangalia ndani ya kitabu nambari zetu za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewahi kuletewa *message* tele hapa na watu ambaao hatujawaona wala hatuwatambui anakuletea “*sweet I love you*”, “*tuonane*”! Sasa *message* kama hizo unaletewa anaziona mkeo, hawezi kuamini kabisa kama yule mtu humjui. Humu ndani zaidi ya asilimia hasmini tumeshatelewa *message* za namna hiyo. Mheshimiwa Waziri aliposikia kilio nilichokitoa hapa na nikamwambia mimi yalishanikuta nusura ndoa yangu iharibike, akajibu vizuri sana kwamba, Serikali inafanya matayarisho ambayo mtakuwa salama ninyi nyote. Simu zetu zimo ndani ya vitabu hatari tupu lakini sasa ole wao na mimi nasema kweli nikiletewa *message* leo hii hapa nakuletea Mheshimiwa Waziri, nakwambia nitafutie huyu aliyeniletea *message*. Mke wangu nampenda, siwezi nikagombana naye kwa *message* za watu ambaao siwajui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hakuna Mbunge asiyempenda mke wake au mwanamke asiyempenda mumewe; sasa atuharibie mtu ambaye anakuona tu sura yako ndani ya TV? Hili haliwezekani kabisa. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hawa kwa kutekeleza jibu walilolitoa la kwamba, ndoa zenu hazitoharibika. Ninaamini watu watajirekebisha na ninapenda elimu itolewe kuwaambia hao wabaya kwamba, sasa watanaswa na watashtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna penye zuri na baya likakosekana; hivi karibuni Zantel walikuwa na mtindo; simu yako unaiweka hela mwenyewe hujaomba kwa mtu, wanakuungizia pesa wanakwambia tunakukopesha. Mtindo huu ulilinga ukawa ni kero

kwa jamii, kwa sababu baadae wanakata pesa bila wewe mwenyewe kujua; ukiweka vocha tu wanakata pesa! Mtindo huu ulikuwa unatukera kweli kweli, hivi sasa ni kiasi cha kama wiki mbili au tatu hivi umesita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliangalie nalo hili, kwa sababu kila siku makampuni haya yanaleta utaratibu mwingine ambaao wanautaka wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ambalo linatupoteza pesa zetu, unaweza kuona mimi nimekaa hapa na Mheshimiwa Blandes yuko pale, simu yake iko wazi nikampigia utashangaa kuna mwanamke anakujibu mteja unayempigia kwa sasa hapatikani; simu yeke iko wazi na yangu iko wazi! Haya ni maudhi makubwa ambayo hayavumiliki, simu yake iko wazi na ya kwangu iko wazi maana yake unajaribu tu kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inatokea sana na mimi ningelikuomba utakapotoka hapo nje ya Bunge, ujaribu kunipigia simu yangu utaambiwa hivyo hivyo na simu zangu ziko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo hili ni kero ni la jimboni kwangu; nakumbuka kiasi cha miaka saba, wakati ule tulikuwa hatujawa wastaarabu wa kutafuta simu za mkononi, nilikuwa na simu ya TTCL ya *prepaid* kila siku ikawa sipati mawasiliano vizuri nikamwambia Dkt. Maua Daftari akaja Mwera *physically* akaangalia tatizo akalijua, akalitatu na nashukuru mpaka leo inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo liko kwa Zantel, Tigo na Vodacom. Vodacom niliishatupa *line* yangu zamani. Mwera ni kilomita kumi kutoka mjini, Dkt. Maua anapajua vizuri mpaka ndani kwangu kilomita kumi kutoka mjini na mnara uko kilomita mbili kutoka nyumbani kwangu ukitokea mjini hupati mawasiliano yoyote ndani, kama unataka kupiga simu utoke nje utafute mahali penye jiwe ukae. Zantel na Tigo sasa unapigwa simu, mimi niliwahi kupigiwa simu na Makatibu wa Kamati wiki mbili hawanipati kwa sababu ninapokuwa ndani hawawezi kunipata kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, mnara mwingine wa Zantel umejengwa kilomita moja na nusu kutoka pale. Dkt. Maua anajua. Ninamtaja sana kwa sababu yeye ni mzoefu wa njia ile. Kilomita moja na nusu, tena juu ya kilima, basi ndiyo imezidi *ku-collapse* pale kwangu, mnara wa kilomita tano kule mbili huku moja na nusu hupati kabisa simu.

Minara hii kama ilivyosemwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kero na wala siamini kama inafanya kazi. Wakati mwingine unapiga simu husikii *ina-ring* kumbe mtu ameshapokea huna habari fedha zako zinakwenda. Sasa haya hayavumiliki. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie haya kwa manufaa yetu sote.

Kubwa ninaloliahidi hapa leo, naziangalia *message* zangu zote nilizoletewa, kesho nikijaliwa nikiletewa *message* mbaya kama hizi sikubali; mimi simpendi mtu mwingine bwana. Nilisema hapa Bungeni sisi wazee tunaheshimu ndoa zetu, hata kama

mtu anataka kumpiga mkewe, atampiga kwa ncha ya khanga sasa hatutaki mtu atuharibie ndoa bure. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia na namtakia kheri Waziri na Naibu wake, lakini haya yangu niliyoyazungumza tafadhali naomba sana wayazingatie. Nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofifi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Sasa namwita Dkt. Juma Ngasongwa, katika orodha yangu ni mchangiaji wa mwisho.

**MHE. DKT. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya Sheria ya Elektoroniki na Posta. Kwanza, naomba nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari na Katibu Mkuu, ambaye namfahamu tangu alipokuwa anasoma kule Chuo Kikuu cha Sokoine, maana nilikuwa mwalimu wake, kwa kazi hii nzuri ambayo wameifanya na wanafunzi wapo wengi hapa ndani niliowafundisha. (*Makofifi*)

Kwa hiyo, nasema sheria hii imekuja wakati muafaka kabisa katika suala zima la uchumi wa kisasa. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia mambo makubwa mawili. Moja ni lile la kujenga uchumi wa kisasa na TEKNOHAMA ni jambo la kisasa, hili jambo ni zuri sana na ndiyo maana nataka kuunga mkono wale wanaosema lazima Makampuni haya yajiandikishe katika *Dar es Salaam Stock Exchange* kwa sababu kwanza tunauwezesha uchumi wetu kuutawala wenyewe. Katika upande wa pili wa Ilani ya chama chetu unazungumzia uwezeshaji wananchi kiuchumi. Maana hii ndio inayowawezesha wananchi kiuchumi na lazima washiriki katika uchumi wao na Taifa lao. Hili ni jambo jema.

Kwa kuwa ninachangia kwa mara ya kwanza; naomba niseme mambo mawili ya utangulizi. Kwanza, natoa rambirambi zangu kwa niaba ya Wapiga kura wa Ulanga Magharibi, kwa Mjane wa Mbunge mwenzetu Ng'itu; lakini pili nitoe rambirambi kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na familia yake, kwa kuondokewa na mzazi wao ambaye alikuwa Kiongozi Shupavu wa Taifa letu, maarufu kwa jina la "Simba wa Vita". Kwa hiyo, nawapa pole na naomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amina.*

Vile vile naomba kutambua maafa yaliyotokea Same, Kilosa na wote ambao wameathirika naomba Mwenyezi Mungu awape subira na uwezo wa kuelewa na kuvumilia ili wasisononeke sana na majonzi hayo. Baada ya kutoa pongezi, sasa nataka kurudia kwenye hoja. Kwanza, naomba niseme suala la kuandikisha *SIM card* hili ni suala zuri. Sehemu nyingine ukienda hata hapa Afrika ya Kusini tu au Uarabuni kule Dubai au Abu Dhabi, huwezi kupata simu hapo hapo ya mkononi, lazima upite muda fulani na lazima uoneshe pasipoti yako kama wewe ni mgeni. Sasa hapa unawenza kununua *SIM card* saa yoyote halafu ndio hili tunaloeleza la matusi. Mtu ananunua kadi anawatukana wenzake baadae anaitupa na hawezi kupatikana. Nafikiri hili la kuandikisha *SIM card* ni jambo jema kabisa, lazima tulitilie mkazo na tuliendeleze kwa

ukamilifu. Suala siyo la kuandikisha tu na kufuutilia kama wale wanaofanya uhalifu wanachukuliwa hatua, maana ukiandikisha tu lazima *sanctions* hizi ziwepo ili watu wanaofanya makosa wapate adhabu zinazostahili.

La pili ambalo nimeshalisema mwanzo lakini nataka kulirudia ni hili la kujiandikisha katika *Dar es Salaam Stock Exchange*. Hili ni muhimu na wala sina matatizo kwamba, lina ubaguzi wa Kikatiba halina ubaguzi. Kwa sababu kuna mahali lazima uanze, tunaanza hapa na Makampuni haya ya simu ndio yenyenye fedha nyingi. Makampuni haya yanapata fedha nyingi sana, kwa hiyo, lazima kodi nazozende Serikalini lakini pia wananchi wawezeshwe kiuchumi kwa kununua hisa katika Makampuni haya na hili ni jambo muhimu sana. Hapana kulionea haya na tumeanza na matumaini kwamba, Mawaziri wengine watakapokuja; kwa mfano, itakapokuja Sheria ya Madini tutafanya hivyo hivyo.

Lazima tufanye hivyo kuanzia sasa, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia umefungua njia sasa Mawaziri wenzako watakapokuja wafanye hivyo hivyo na kama hapana budi basi Mwanasheria Mkuu wa Serikali alete Muswada hapa wa Marekebisho ili mambo haya yawe *across different sectors of our economy* ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa Taifa lao. Hili ni jambo jema tu. Mimi naona siyo sahihi Makampuni yanajiandikisha kwenye *Stock Exchange* ya London, Canada, South Africa lakini hawafanyi hivyo hapa; hii maana yake nini? Hiyo siyo sahihi wakati rasilimali kubwa inatoka hapa lazima tukubaliane hili, hili ni suala la uzalendo na lazima tulisimamie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni hili la minara. Mimi nakubali kabisa kwamba, suala la minara lazima lisimamiwe vizuri na lazima kuwe na ushirikiano katika matumizi ya minara. Kwanza, kwa mfano, hawa jamaa wa VODACOM wana tangazo lao pale wanasema wana mtandao mkubwa zaidi katika nchi umeenea sehemu zote; kwangu haupo. Kwangu hakuna ni juzi tu ndio wameanza kufanya juhudu tu ya kuuleta, lakini sehemu kubwa ya jimbo langu mtandao wa VODACOM haupo. Mimi nashukuru, wakati fulani nilipokuwa pale nilikuwa siku nyingine nikiwa jimboni nataka kuangalia mambo yanakwendaje ofisini, basi napanda kwenye mti na ule mti unaitwa jina la Ngasongwa, Mti wa Ngasongwa halafu napiga simu napata. Jamaa hapa wakanicheka ooh wewe Bwana Ngasongwa unakuwaje unapanda kwenye mti, sasa nifanyeje; nataka njue habari za Dar es Salaam ambako ndiko nimepewa majukumu ya kuendesha?

Bahati nzuri watu wa ZAIN wakati huo CELTEL, wakasikia kilio hicho wakajenga mnara Malinyi, wakajenga mwingine Mtimbira, sasa ndio napambana nao wajenge na wa Itete maana huu walishaahidi siku nyingi tangu mwaka juzi wangeujenga kwani Naibu Waziri ameshughulikia sana kuhusu jambo hili, naomba sasa Waziri mwenyewe ulishughulikie mnara mwingine wa Itete ujengwe jaman, i maana mtaniharibia wakati wa uchaguzi. Watu wanafikiri nafanya ubaguzi kumbe mimi sifanyi ubaguzi, ninyi ndio mmeanza mkajenga kwanza Malinyi nyumbani kwangu, mkafuata Mtimbira, sasa jengeni na wa Itete jimbo zima likamilike ili watu waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kujenga minara mingi ndio lenyewe. Hakuna haja ya kujenga minara mingi mahali pamoja, watu watumie minara ile ile; najua msingi wake ni biashara. Wengine wanasema ushindani wa biashara kwamba ukiwa na uwezo ndio utajenga minara mingi, lakini mashindano ya kujenga minara haina maana sana kwa sababu kwanza ni gharama kwa Taifa, lakini pili inaongeza bei kwenye simu. Kwa sababu pia tunalipia minara ile. Tatu, hata ninyi Serikali mnapunjika katika kupata kodi zenu kwa sababu sehemu ya fedha zile zinagharimia minara ile. Minara ile ni gharama vile vile siyo tu kwa kujenga hata kwa kuiendesha, sehemu nyingine hakuna umeme. Kwangu mimi wanatumia sana majenereta, sasa majenereta saa 24 ni gharama kubwa ya mafuta na kadhalika.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na suala hili kwamba, minara ile *tui-rationalise* Makampuni mengi yaweze kuchangia minara ile na kwa kufanya hivyo nchi itakuwa na *access* zaidi ya mawasiliano. Sasa hivi kama tungepiga hesabu ya minara hii, kwa mfano, ule uliojengwa na watu wa VODACOM pale Malinyi wangeujenga Itete au Ilagua, jimbo zima sasa tungakuwa na mawasiliano bila matatizo. Kwa hiyo, naomba suala hili mlitilie mkazo na lifanywe vizuri ili tuweze kuisimamia nchi yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni hili la mapinduzi katika Sekta ya Posta; naunga mkono hilo la matumizi ya *Addresses* na *Postcard*. Hili ni suala zuri kwa sababu huduma zitakuwa karibu zaidi ya wananchi. Kule Ulaya na sehemu nyingi zilizoendelea wanafanya hivyo na utakuta barua inaletwa kabisa nyumbani kwako. Jambo hili ni zuri kuliko kutegemea matumizi tu masanduku. Sijui kama mtayaondoa masanduku, lakini mkianzisha matumizi haya na yakaenea nchi nzima, basi matumizi ya kwenda kutafuta barua sehemu nyingine mbali kutoka nyumbani kwako yataondoka. Kwa hiyo, hili ni jambo zuri kwa maana ya kwamba, tunataka tuliimarishe Shirika la Posta. Lazima tuliimarishe kwa sababu bila ya kuliimisha hili, litaendelea kuwa mzigzo na sidhani kama ni sahihi. Sasa hivi watu wa Scandinavia Bus Service ndio wanasesfirisha sana mzigzo yetu. Sisemi kwamba, kuwe na *monopoly* hapana, ninachosema ni kwamba lazima tuwe na utaratibu ambao unafaa kuimarisha wadau wote katika sekta ile siyo kupendelea baadhi ya wadau. Kwa hiyo, hili ni jambo zuri na naliunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimefurahi sana kwamba, katika sheria hii vifungu vingi sana vimewekwa katika suala la kuwekea utaratibu au ushindani. Nafikiri hili ni jambo zuri sana. Sisi zamani tulipokuwa tunafundisha uchumi tulikuwa tunasema kwamba, soko halitoi haki au rasilimali sawa kwa kila mtu anayeshiriki katika soko. Soko lina tabia ya kupendelea wale wenye uwezo zaidi, hakuna *equality at the market place*; ndicho kinachosemwa pale, mwenye fedha zaidi ndiyo anapata zaidi. Hata ukienda sokoni mjini utakuta wanenanua vitu vitatu au vinne tu wanamaliza, wengine wanenanua vitu vingi pale ndio tabia ya soko. Kwa hiyo, lazima tulisimamie soko.

Kulisimamia soko ni jambo jema na mafunzo ya uchumi wa sasa huu uliotokea wa vurumai mwaka jana umeonesha kwamba, soko bila kulisimamia ndio unawenza kupata vurumai kubwa zaidi. Kwa hiyo, soko hili la *Electronics* na *Postal Services* lazima tulisimamie na tuliwekee kanuni ili jamaa hawa wasitunyonye sana, kwa sababu

pale kwenye soko kuna watu wengine wananyonywa zaidi lakini kuli-control ni vizuri ili kunyonyana kule kuwe na nafuu kidogo. Kwa hiyo, hivi vifungu vyatuhindani hapa vimenifurahisha kweli na kwa mara ya kwanza nadhani Serikali inazingatia suala la kutazama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kukushukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nawashukuru wachangiaji wote mliopata nafasi asubuhi hii, tukirudi mchana tutampa nafasi hoja aweze kuhitimisha mjadala katika Muswada huu na kwa kuwa Muswada wenye una vifungu vingi, basi tutapitia kimoja hadi kingine ili muweze kutoa mapendekezo yenu kama yapo. Kwa sasa sina shughuli nyingine, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 12.43 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, asubuhi tulipoahirisha shughuli za Bunge, wachangiaji wote walikuwa wamepata nafasi; kwa hiyo, ilikuwa zamu ya watoa hoja kuanza kujibu hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupa uzima na kutuwezesha kukutana leo hii. Nakutakia wewe binafsi, Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, kheri ya mwaka mpya, ikiambatana na kuwatachia mafanikio mema katika uchaguzi wa mwaka huu. (*Makofit*)

Pili, napenda nitoe pole kwa familia na ndugu wa Marehemu Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa. Kifo chake ni pengo kubwa kwa chama chetu, nikiri tu Marehemu Mzee Kawawa alinisaidia kujifunza mengi katika siasa. Busara zake katika kufanya maamuzi ya mambo mengi mazito zitakumbukwa milele. Nawapa pole ndugu zangu wa Wilaya ya Namtumbo na naiombea roho ya marehemu iwekwe mahala pemapeponi. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kidogo kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu mia kwa mia. Sekta ya Mawasiliano Nchini inakua kwa haraka na mabadiliko ya teknolojia yanazifanya nchi zote si Tanzania tu, kuchukua hatua muafa ili kwenda na wakati na pia kuzifua tilia nafasi zinazopatikana kutoana na mabadiliko hayo ya haraka yanayoendelea. Sekta ya Mawasiliano inayo nafasi kubwa ya kuboresha uchumi wa nchi yetu iwapo itawekewa mikakati mizuri ya uwekezaji na kutoa huduma zao. Kwa mantiki hiyo hiyo, Watanzania nao ni vema wafaidike na ukuaji wa haraka na fursa zitokanazo na Sekta hiyo. Ndiyo maana katika utekelezaji wa uwezeshaji wa wananchi wetu kiuchumi, Sekta inaweka kwa makusudi kabisa, taratibu za wao kupata nafasi za kuingia ubia na kuwa na *share* katika makumpuni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika Sekta hii hauna hasara iwapo mipango madhubuti, mikakati imara ya uwekezaji, uwezo wa kifedha na uwezo wa kitaaluma utakuwa unafikiwa. Licha ya uzuri wote huo wa Sekta hii, bado kuna madhara kadhaa ambayo tusipoweka mikakati thabiti, basi usalama wa nchi yetu na maadili ya watoto wetu yanaweza kuperomoka. Mawasiliano ya simu za mkononi na *internet* yameboreshwa na kurahisha maisha yetu na wengi wamefaidika na ujio wake. Wapo wanaoyatumia mawasiliano haya kwa kufanya uhalifu uporaji, uhujumu na kuharibu *image* za watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika chache naomba nichangie machache. Kwanza, nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, tulipokuwa naye katika kujadili hoja hii katika Kamati tulikubaliana naye mambo yote na aliunga mkono mambo mengi sana; lakini nadhani alivyokuja hapa akaja na mengine; namwachia Mheshimiwa Waziri ayasemee hayo lakini nasema alisema jambo moja kuhusu posta kusimamisha au kufuta leseni ya posta, leseni za elektroniki ni Mhakama Kuu lakini leseni za posta zinaamuliwa na Mamlaka.

Ukiacha leseni za mtoa huduma za umma, nyingine zote ni zile zilizozidi muda wa miaka mitano, pia uwekezaji wake siyo mkubwa ukilinganisha na ule wa makampuni ambayo yanatoa huduma za kielektroniki, kwa sababu zinasimamiwa. Kusimamishwa au kufutwa kwa leseni hizi kushughulikiwe na Mamlaka ya Utoaji Leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Hili lipo na linafanyika tangu zamani.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela akiwa ni Mwenyekiti wa Kamati, tunamshukuru sana na tunaishukuru sana Kamati kwa kutupa *support* ya kutosha na mengi waliyoyasema ni yale ambayo tumekubaliana sote kwa pamoja. Tunawashukuru nyote. Amesema mengi; kuharakisha zoezi la kuchapisha anuani na *symbol* za Posta, Kamati inapongeza usajili wa Kadi za Simu, kuzuia wizi wa simu, udhibiti wa uingizaji wa simu na utaratibu wa kumnyang'anya mtoa huduma masafa ufanyike kwa umakini. Tunasema haya yote tunamshukuru na maoni ya Kamati tutayafanyia kazi na Sheria hii ikipita, itapunguza masuala mazito ya uharifu.

Vile vile lilizungumzwa suala la *deposit* ya milioni nne. Serikali ijifunze katika nchi nyingine, tunasema sawa. Utaratibu wa kuingia hisa DSE, hili atalisemea sana Mheshimiwa Waziri. Serikali iweke mazingira mazuri ili kusaidia makampuni kujiandikisha DSE na Serikali iendelee kufanya utafiti kujua faida na hasara na kuweka mazingira mazuri ya usalama wa fedha zao. Serikali itumie wataalam kutoa ushauri juu ya masuala haya. Ushauri wa Kamati tunauzingatia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Zambi, yote uliyoyazungumza ni yale ambayo tumekubaliana katika Kamati. Amesema anakubaliana na Sheria hii; ni nzuri, mali za Watanzania zinafaidisha Watanzania wenyewe na wengi watafaidika na Serikali itapata kodi sahihi; na sheria hii haina ubaguzi. Tunasema shukrani Mheshimiwa Zambi, hoja zako ni nzuri na malengo ya Muswada huu tumeyasikia na tunakubaliana na mawazo yako yote. Nirudi tena kwa Mheshimiwa Arfi,

alizungumzia kifungu cha 6(2)(e) kwamba, kifungu hiki kinamnyima haki Mwekezaji mzalendo ambaye anamtaji wa kutosha lakini ambaye hana uzoefu, kinafunga mlango kwa Watanzania wasio na uzoefu wa biashara. Tukitazama hali ilivyo hivi sasa na uzoefu wa nyuma, tunasema ni muhimu kwa ajili ya kampuni yoyote inayotaka kuanza kutoa huduma ya mawasiliano nchini.

Aidha, kampuni isiyokuwa na uzoefu inaweza kuingia makubaliano na kampuni yenye uzoefu au kuajili wataalam wenye uzoefu; Mamlaka ya Mawasiliano imeshatoa leseni kwa makampuni yanayomilikiwa na Watanzania ambayo hayana uzoefu wa nyuma. Kwa mfano, Kampuni ya Dovetel ambayo sasa inaitwa Sasatel, walioomba mwanzoni walikuwa ni Watanzania. Kwa hiyo, hakukuwa na uzoefu lakini wakapata watu ambao wana uzoefu katika fani hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 inazungumzia kuwa Mamlaka itaweka masharti kwa mtu mmoja mmoja anayehitaji leseni. Jambo hili linaweza kutumiwa na Mamlaka kwani masharti yaliyopo katika Muswada yanatosha, vinginevyo ibainishwe wazi kwenye Kanuni. Hii Ibara ilikuwa inazungumzia *terms and conditions and individual licence*.

Tunaposema hivi hatumaanishi *terms* ya mtu mmoja mmoja ila ni aina ya leseni ambayo inafafanuliwa kwenye kifungu cha 15. Naombeni sana Waheshimiwa Wabunge, tumeleta *amendment* nafikiri mkizipitia zitasaidia vizuri. Iwapo Kampuni hajtaridhika, basi ye ye anayo nafasi ya kwenda kwenye *Competition Tribunal* na kama hakuridhika hapo anaweza kwenda Mahakamani.

Vifungu vya 18(g), (h) na (i) vinazungumzia masuala ya *material breach*. Nilisema vifungu hivi au vipengele hivi vinapotisha maana halisi ya maneno *line* yaongezwe. Tunasema ushauri tumeuzingatia na kifungu kimeboreshwa kwa kubadilishwa neno *provide* na kuwa na maneno *facilitate routing*. Maana kuna zile *services* zinazotolewa na makampuni *free of charge*, tumeweka usawa vizuri hapo kwenye mabadiliko. Suala lingine ninalotaka kulizungumzia lilikuwa ni kwa nini wenye leseni za *electronic communication* nafasi yao ya rufaa ni Mahakama Kuu na kutumia utaratibu wa kimahakama. Tunasema utaratibu ni kwamba, kama mtoa huduma hajtaridhika na jambo lolote au na uamuji wa Mamlaka, anaweza kukata rufaa kwenye Tume ya Ushauri na kama hajtaridhika katika Tume anaweza kwenda Mahakama Kuu. Hii inafanya kwa watoa huduma wote wala hakuna ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilizungumzia kifungu cha 78(7), masafa kutolewa kwa njia ya zabuni au bei maalum itakayowekwa na Mamlaka, jambo litakalosababisha wafanyabiashara kufanya ukaguzi wa leseni kwa vile kanuni za zabuni ni kwamba, mwenye bei kubwa ndiye atakayepata na tunapendekeza jukumu la kutoa masafa liwe ni kwa mamlaka kuweka bei maalum. Tunasema utaratibu wa kutumia zabuni si mpya, ulikuwepo toka zamani na utafafanuliwa kwenye Kanuni na vigezo vingi vitatumika na siyo kwamba lazima apewe *the highest bidders*. Unaweza ukawa na *highest bidder*, lakini hawezi ku-*qualify* kufanya lile jambo.

Lingine ni suala lililotoka kifungu cha 126; *unauthorized access au use of computer system* tulisema kwamba, ufanuzi unahitajika kwa kuwa mtu anayetaka kuingia kwenye mfumo wa kompyuta na kusababisha madhara atakuwa amefanya kosa kwa vile kila kampuni ina mfumo wake; itakuwaje kwa Mamlaka kuweza kudhibiti? Hapa ni utaratibu wa matukio haya pamoja na mashirikiano na mataifa mengine katika kupashana taarifa za matukio ya kuingiliwa kompyuta na mitandao yake.

Kipengele cha 126 kimeboreshwa tutakuwa na 126(1); *there shall be established computer emergency response team which shall be responsible for coordinating the response on cyber security and computer related incidents and cooperate with other society in the world.*

Pili, kitakuwa 126(2); *The Minister shall make regulation to the composition, duties and function of CRT* na kutakuwa na kifungu kingine cha tatu kitakacho-take care yale ambayo tumeyaacha. Kifungu cha 133 kinasema kuwa, anayetumia *SIM card* ambayo haikusajiliwa anakosa na adhabu yake ni *fine* isiyozidi shilingi milioni 1.5 za Kitanzania. Akasema kwamba, watu wengi wa majumbani na vijijini hawawezi kumudu adhabu hii. Ukitisoma vizuri ile adhabu ni kwamba, kifungu hiki kinatoa fursa kwa mahakama kuweza kutoa adhabu kulingana na uzito wa kosa lenyewe; *not exceeding*, kwa hiyo siyo lazima atoe milioni 1.5 lakini nia ni udhibiti.

Mheshimiwa Charles Kajege yeye aliomba kifungu cha 92(2) neno *damage* liondolowe maana simu iliyoharibika haiwezi kutumika. Tunasema simu iliyoharibika inaweza kutumika kwenye simu nyingine, kwa hiyo, neno *damage* tunafikiria sisi bado libakie litakuwa na maana yake.

Mheshimiwa Gosbert Blandes anapongeza kitendo cha makampuni katika soko la hisa, kwani makampuni haya yamejisajili nchi za nje, wazawa watashiriki kukuza uchumi wao na kwa utarabibu huu hisa za Kitanzania zitanunuliwa na watu wa kipato cha chini. Pia aliomba asaidiwe mnara wa simu katika Kata yake ya Nyakakika eneo la Kadegesho.

Tunamshukuru Mheshimiwa Blandes kwa kuunga mkono hoja hiyo, hususan kifungu cha 26 ambacho Mheshimiwa Waziri atakitolea ufanuzi zaidi na Serikali itaangalia utaratibu wa kuyaomba makampuni ya simu na suala lako tulishalipeleka kwa makampuni kwa ajili ya kulifanyia kazi. Kulikuwa na suala moja ambalo lililetwa na Mheshimiwa Charles akiomba kwamba, tuwe na muda maalum (*time frame*), tangu kupokea maombi na kutoa leseni. Tunasema hili litashughulikiwa na litaanishwa katika kanuni baada ya kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Msindai alisema ni muhimu sana kujiunga na DSC kuleta uwazi na mapato kuliko kusubiri misaada. Tunakubaliana na hoja yake ila lengo la kusimamia suala hili katika Sekta ya Mawasiliano basi sekta nyingine nazo nadhani wataona umuhimu wa kutufuata sisi tulivyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 19 kinazungumzia *renewal of individual licence* ambacho nilishazungumzia mapema. Anasema muda wa kuongezwa uwe wazi

katika sheria. Tunasema muda umeainishwa katika *regulations* na ukienda kwenye *regulations* utaona zote zimewekewa muda maalum. Tutaomba Mheshimiwa Waziri akitolee maelezo kifungu cha 26.

Mheshimiwa Haroub Masoud, tunakushukuru kwa pongezi zako. Tunakupa pole kwa hizo meseji ambazo zinaweza kukuletea matatizo kwa mdogo wangu. Niseme tu nia yetu ya kuleta Muswada huu ni katika kuondosha haya matatizo ambayo wewe unaona yanakusibu. Nikuombe tu utuunge mkono ili upite Muswada huu tuweze kuwa na udhibiti ambao wewe unauhitaji. Nakubaliana na wewe kwamba, matatizo ya network ni kero na kama ulivyo sema, zinatolewa *promotion* nyingi watu wanajirusha na kwa muda wote watu wanakuwa wamekamata *line* zile wengine hawapati mawasiliano.

Niseme tu kwamba, TCRA itaendelea kudhibiti hili na kuona kwamba, ubora wa huduma inapatikana. Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa alizungumzia matumizi ya anuani ya makazi na *postal codes* ni jambo zuri na ni maendeleo na linaimarisha Shirika la Posta Tanzania. Jambo hili litaimarisha Sekta nzima ya Posta ikiwemo sekta binafsi. Napenda kutoa taarifa kwamba, Serikali imedhamiria kwa dhati kabisa kuweka mazingira mazuri ya kuendesha shughuli hizi za posta nchini kwa kuzingatia sera na miongozo ya mikakati ya posta 2003.

Anuani mpya za kitaifa zimezinduliwa rasmi tarehe 18 Januari, 2010 na Mheshimiwa Makamu wa Rais Mjini Arusha na utekelezaji utaendelea katika sehemu nyingi nchini ikizingatia hali halisi ya fedha itakavyopatikana. Agizo lililotolewa kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kote nchini na sisi wasimamizi wa seka hii, tutahakikisha kwamba hilo linafuata kwa kumwomba mwenzetu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba, tunapata fedha za kutosha kwa utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Manyanya alitaka Wizara iongeze *Tele-centres* hasa vijiji na mashulenii. Tunasema ushauri umezingatiwa na mipango ya utekelezaji inaendelea na vilevile Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ulianzishwa kwa makusudi ya kuzambaza mawasiliano vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huo mdogo niliopewa, nashukuru sana kupata nafasi hii na nawaombeni Waheshimiwa Wabunge kama mnavyonipa ushirikiano nikifanya kazi zenu za mawasiliano, mnipe ushirikiano kwa kupitia Muswada huu tuweze kudhibiti mambo mengi ambayo yanatuletea matatizo katika maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuhitimisha hoja yangu, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuhitimisha hoja hii leo hapa Bungeni. Napenda nichukue nafasi hii vilevile kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na waliochangia kwa maandishi. Wote nawashukuru sana kwa michango yao ambayo nina imani kubwa itatusaidia katika kutekeleza Sheria hii baada ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Wa kwanza ambaye amemaliza sasa hini ni Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Naibu Waziri ambaye kwa kweli amejibu karibu hoja zote ambazo zilitolewa hapa. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Napenda vilevile kumtambua Mheshimiwa Said Amour Arfi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Nawashukuru Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Eng. Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Margreth Sitta, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

Baada ya kuwashukuru Wabunge kwa michango yao, naomba nitoe ufanuzi wa maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge na hususan yale ambayo Naibu Waziri hakuyagusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo limezungumzwa sana leo lilikuwa ni ile ibara ya 26 inayozungumzia juu ya uwekezaji kwenye soko la hisa. Napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano imekuwa kwa kasi sana toka soko hili lilipoanza kufunguliwa mwaka 1994, kwa kuanza kuruhusu wawekezaji binafsi kuingia kwenye soko na kuondoa ukiritimba wa Kampuni ya TTCL, ambayo wakati ule ilikuwa inashughulika na hili. Kwa miaka 16 sasa sekta imekuwa kwa kasi na kufikia watumiaji zaidi ya milioni 14 na pato ghafi kwa mwaka linalozidi shilingi trilioni 1.6 za kitaifa kwa mwaka. Sekta hii imegusa sehemu mbalimbali za uchumi wetu hapa nchini. Ukuaji huu haukutokea kwa bahati mbaya ila ni kwa juhudzi za Serikali, Wawekezaji na Sera mahususi zilizoboresha mazingira ya uwekezaji kama vile misamaha mbalimbali ya kodi na Sera za Ubinafsishaji. Udhibiti wa mirabaha ambayo imepungua kutoka asilimia tano mpaka kufikia asilimia 0.8. Vilevile Serikali kuitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imefungua milango yote ya soko na kuruhusu ushindani kamili. Mwaka huu Serikali kuitia Muswada huu inaelekeza juhudzi zake kwenye kuongeza ushindani, kuboresha mazingira ya kibiashara na kuongeza ushiriki kamili wa Watanzania walio wengi zaidi kwenye Sekta hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada mpya unalenga kuweka kwa vitendo jitihada za makusudi za Serikali ya Awamu ya Nne katika kuawezesha Watanzania katika uwekezaji na umiliki wa uchumi kwa kutenga asilimia mahususi itakayomilikiwa na Watanzania katika Sekta ya Mawasiliano. Sheria hii inaendana na juhudzi mahususi na kaulimbi ya Serikali ya Awamu ya Nne kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Muswada huu ukipitishwa ikawa Sheria, utaleta mabadiliko makubwa kwa kuleta mazingira shirikishi kwa Watanzania katika Sekta ya Habari na Mawasiliano.

Muswada unatimiza kile kilichokuwa kikikosekana katika Sheria ya Mawasiliano iliyopo kwa sasa. Tangu kuanzishwa kwa Tume ya Mawasiliano Mwaka 1993 chini ya Sheria ya Mawasiliano Namba 18 ya Mwaka 1993. Sheria imekuwa na sharti katika leseni inayotaka umiliki wa hisa katika Kampuni za Mawasiliano kuwa si chini ya asilimia 35 kwa Watanzania. Sheria hii haikuweka bayana ni kwa namna gani kwa Watanzania walio wengi wanaweza kushiriki katika umiliki wa hisa hizo za asilimia 35 kwa sababu asilimia 35 inawezekana mtu mmoja mwenye uwezo akanunua hizo zote basi akawa mmoja lakini Watanzania walio wengi hawanufaiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Huduma za Utangazaji Namba 6 ya Mwaka 1993 ina upungufu katika umiliki wa hisa. Sheria hiyo inataja viwango vya asilimia 55 na 51 kuwa mikononi mwa Watanzania lakini haioneshi ni Watanzania wangapi wanatakiwa kumiliki hisa hizo. Ni kutokana na upungufu huo katika Sheria hizo mbili na katika kutekeleza lengo la kutoa fursa kwa Watanzania kushiriki katika kumiliki Sekta ya Uchumi, ndiyo chimbuko la mapendekezo la kuweka katika Muswada.

Suala la makampuni kujirodhesha katika soko la hisa ili asilimia za umiliki zijumuise Watanzania waliowengi zaidi. Katika hili tunatarajia kuwa makampuni haya yatafuata utaratibu wote uliowekwa na Sheria ili kuhakikisha kuwa yanatimiza masharti ya kuruhusiwa kuuza hisa hizo zao katika soko la hisa. Uzoefu katika nchi nyingine unaonesha kuwa makampuni mengi yaliyo katika Sekta ya Mawasiliano zimejirodhesha katika masoko ya hisa nje ya Tanzania. Haya yalielezwa asubuhi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na nirudie kutoa mfano. Kwa mfano, Tigo imejjirodhesha kwenye Stokhom Stock Exchange Sweden na Nasdaq Stock Market ambayo ni New York Marekani. Vodacom South Africa imejjirodhesha Johannesburg Stock Exchange. Zain imejjirodhesha Kuwait Stock Exchange, lakini zote hizo hazijajirodhesha katika soko letu hapa nyumbani.

Aidha, uzoefu unaonesha kuwa hata baadhi ya kampuni zilizoko nchini ambazo zinawashirikisha wenyе hisa katika nchi nyingine, kampuni hizo zimejirodhesha katika soko la hisa hapa nchini. Kwa mfano, Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), imenorodheshwa katika soko la hisa nchini lakini vilevile Submiller ambayo ina asilimia 52.83, imenorodheshwa katika London Stock Exchange na Johannesburg Exchange. Aidha, Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), ambayo imenorodheshwa katika soko la hisa na wakati huo Kampuni ya Ushirika Japan Tobacco Incorporated yenye asilimia 75 imenorodheshwa katika soko la hisa la Tokyo.

Benki yetu ya NMB ambayo inashirikiana na Rabo Bank yenye asilimia 34.9 imenorodheshwa katika soko la hisa nchini na Rabo Bank inahusisha Benki za Ushirika 152 za Netherlands. Mbali na kushirikisha Watanzania wengi kumiliki hisa, maendeleo na utendaji wa makampuni katika soko la hisa hudhihirishwa na bei ya hisa za soko za kampuni katika soko. Udhihirishwaji huo pamoja na wazo ambalo linatakiwa kuwepo katika uendeshaji wa kampuni na mahesabu ya kampuni, hufanya makampuni hayo kuwa na viwango vilivyo bora vya utendaji. Hivyo basi, pendekezo la uanzishwaji wa hisa kwa Watanzania wengi kwa kupitia soko la hisa utaongeza ufanisi. Tutaendeleza juhudi za

kuhakikisha Watanzania walio wengi wanashiriki katika shughuli za kiuchumi hususan katika Sekta hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuleta pendekeso hilo katika vipengele vinavyohusika inasema watawekeza, vile vile *in accordance with Capital Market and Securities Act*. Kwa hiyo, bado taratibu zitafuatwa kama zilivyowekwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimalizie majibu machache ambayo Naibu Waziri alikuwa ameyaacha. Nianze na swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Margret Sitta, ambapo alisema kwamba, tuhakikishe bei za simu zinapungua. Ninachosema ni kwamba, bei za simu toka zilivyoanza zimeendelea kupungua kila wakati na kwa sasa hivi zitazidi kupungua kwa sababu huduma hizo baada ya ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa na vile vile baada ya kuanzisha Mfuko unaoitwa *Universal Communication Access Fund (UCAF)*. Ni kwamba, huo ndio utakaopeleka mawasiliano mpaka kufikia kwenye ngazi ya vijijini, kwa hiyo, gharama za mawasiliano zitapungua kwa sehemu kubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa na swali la Mheshimiwa Charles Mguta Kajege, ambaye alisema neno “*knowingly*” litoke, kwani mtu akifanya kosa hata bila kujua bado ni kosa. Tunasema neno hili tunaona bado libaki kwani mantiki ya kuwepo kwake ni kwa ajili ya kumwajibisha mhusika ambaye anakiuka miiko ya kazi yake, hivyo kuliiondoa linaleta mwanya wa watoa huduma kutowajibika katika makosa yaliyo bayana katika utendaji wao wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na swali ambalo liliulizwa na Kambi ya Upinzani, ambalo kwa kweli nimekwishalijibu kuhusu Ibara za 26(3) na (4) na 25 na 26 kwa ujumla. Ambalo linasema sheria inawagawa wawekezaji; kwa nini wawekezaji wa Sekta ya Mawasiliano tu baada ya miaka mitatu ya biashara ndio walazimishwe kusajili hisa katika soko?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema sheria hii inahusu Sekta ya Mawasiliano na posta tu. Sasa zile zitakazokuja nyingine, nao wataona umuhimu wa kuweza kuingiza vigezo vya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwepo na kifungu cha 75 ambacho kinamtaka mshtakiwa aweke *deposit* ya zaidi ya bilioni mbili. Tunasema jambo hili siyo geni, kwani kuweka dhamana ni suala muhimu katika shauri lolote lile na sisi wenyewe hapa ni mashahidi; kesi za EPA zinazoendelea wanatakiwa kuweka hiyo dhamana na ndio maana wengine wamelazimika kukaa ndani mpaka watakapopata dhamana ambayo imetajwa. Jambo la masafa na mambo mengine haya, kusema kweli ni mambo ambayo ni *very sensitive*; hii ni rasilimali ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi alisema, wanaotumia simu na huduma za mtandao vibaya kwa kuchafua watu wengine, sheria hii iwabane.

Akasema makampuni ya simu yasambaze huduma sehemu nyingi zaidi ili kuwafikia wananchi walio wengi zaidi na akasema gharama za huduma za simu bado ziko juu. Sasa hili la kufikia sehemu mbali zaidi, nimeshatoa maelezo nilipokuwa najibu swali la Mheshimiwa Margret Sitta pamoja na gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunaeleza kwamba, sheria imezingatia matumizi mabaya na kuweka vifungu vya adhabu. Soko letu bado linakua, hata hivyo sheria inatoa fursa ya soko kukua na kufikisha mawasiliano sehemu nyingi zaidi na maeneo yasiyo na mvuto wa kibashara yatakayosaidiwa kwa kuwepo kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Kwa upande wa mambo ya *promotion*, Naibu Waziri ameshatoa maelezo, kwa hiyo hayo yamekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa alizungumzia juu ya kifungu cha 106. Kifungu hiki kisingetumika kuzuia matangazo mazuri ya kielimu na ya kimaendeleo kama ya Haki Elimu. Ni vema kifungu hiki kikatumika kudhibiti matangazo yenye maadili potofu kwa jamii na kwamba, adhabu ni kubwa mno ifutwe.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kifungu hiki kina lengo la kudhibiti matangazo yenye maadili potofu na mabaya kwa jamii. Pia kifungu hiki hakitumiki kuzuia matangazo na vipindi vyenye lengo la kutoa elimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu zote zimetoa kima cha chini (*not less than*) na pia kiwango cha juu (*not exceeding*) kutokana na kosa na kuipa uhuru mahakama kufanya maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejibu hoja zote ambazo zilitolewa asubuhi hii. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (The Electronic and Postal Communication Act, 2009)**

Ibara ya 1

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 2

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 13

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, nimehusika sana katika Muswada huu, lakini ninapoona pana makosa ni vizuri wenzetu wakatufafanulia.

Ibara ya 13(3) inayoanza na “*The Authority shall define each content service license in relating to.*” Tulisema yale maneno “*in relating to*” yasomeke “*in relation to*”. Sasa bahati mbaya wenzangu tulikubaliana lakini naona hawakuyaona yale. Pia

ukienda subsection 4 inasema “*Every content service licensee shall be required to enter*”. Sasa neno *enter* limeandikwa vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja, nadhani umemuelewa?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, 13 anayosoma sielewi iko wapi.

**MWENYEKITI:** Anasoma kwenye marekebisho, si 13 ina marekebisho?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Kwenye marekebisho!

**MWENYEKITI:** Eeh, maana 13 pamoja na marekebisho yake, kwa hiyo iko kwenye marekebisho.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:**  
Tumeizingatia.

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia hoja katika kifungu hiki hasa Ibara ya 26(3) na (4); katika ya (3), ningependa nipaye maelezo ya...

**MWENYEKITI:** Naomba nikuongezee kwamba nimesema kifungu hicho kina marekebisho, sasa si utakwenda kwenye marekebisho?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho sijaona kwa sababu ile *schedule of amendment* imetolewa kabla ya mchango wangu, kwa hiyo, sidhani kama itakuwa *ime-capture*.

**MWENYEKITI:** Ilitolewa asubuhi hukuiona? Sema hoja yako, halafu watasema kadiri ilivyorekebishwa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika ibara ya 26(3) anasema: “*Every licensee shall, within three years from the commencement of this Act...*” Sasa labda tuseme kwamba, *in case* akishindwa kutimiza haya masharti kwa sababu hatuoni kutatokea nini hapa. Hiyo ya kwanza.

Katika ibara ya nne, mstari wa pili anasema: “*The licensee shall sell the local shares to the Tanzanians.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia makampuni ya simu, kwa mfano; kampuni kama ya ZAIN ina-operate Tanzania na Uganda; na hivi karibuni tulisaini Mkataba wa Common Market ambao unaruhusu kila mkazi wa *East Africa* aweze kufanya biashara, aweze kununua *shares* katika kila nchi. Sasa kama tutaiacha *provision* iwepo hapa, tutakuwa tunapingana na mkataba ambao tumemaliza kuusaini juzi. Labda ningependa kupata maelezo hapo. Ahsante.

**MWENYKITI:** Lakini, hicho cha nne kilirekebishwa. Mwanasheria Mkuu tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Mheshimiwa Charles Kajege ni sahihi. *Capital Stock Market* na *Securities Act* siyo jambo ambalo sasa hivi linatekelezwa kwenye Common Market ya Afrika Mashariki. Kama anavyofahamu, *process* hiyo itakuja kwenye *Monetary Union* baada ya *process* ya Common Market kumalizika. Hii ni *process* ambayo ni ndefu na ikifika wakati huo kama kutakuwa na mabadiliko ya sheria basi itabadilishwa lakini ilivyo sasa ni sawa sawa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake kwamba ni nini kifanyike kwenye ibara ndogo ya (3) kama makampuni haya yatashindwa, nafikiri hilo suala liko wazi kwamba, kama hayatakuwa yametimiza masharti ya *Capital Stock Market and Securities Act*, hayata-list shares kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*.

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 37

Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 43

Ibara ya 44

Ibara ya 45

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 46

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 47

Ibara ya 48

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 49

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 50

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 51

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 52

Ibara ya 53

Ibara ya 54

Ibara ya 55

Ibara ya 56

Ibara ya 57

Ibara ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 59  
Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaona  
marekebisho yamefanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Ibara ya 63

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 64  
Ibara ya 65

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 67  
Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 70

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 71

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 72

Ibara ya 73

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 74

Ibara ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 76

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 77

Ibara ya 78

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim, lakini na marekebisho yapo soma pamoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ningependa kupata ufanuzi kuhusu kifungu hiki katika suala la masafa. Katika Muswada huu, imeelezwa kwamba, masafa yatauzwa kwa njia ya zabuni. Nafahamu kwamba, kwenye zabuni yule ambaye atakuwa na bei ya juu ndiye anayepata zabuni hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa na wasiwasi hapa kwamba, wale walio na uwezo mkubwa, wanawenza kununua masafa bila kuyatumia na hivyo kuleta...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim, naomba ukae kidogo. Tupo kwenye *stage* ya kutunga Muswada, siyo *argument* kama inazidi ama nini. Sasa hapo ukiniambia maneno fulani hapa yanaathiri kitu fulani, nitakuelewa. Kama ni hoja tu kwamba ni mnada au nini, hiyo tulishamaliza. Sasa endelea kama ni hivyo basi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufanuzi tu, kama muda wake umepita basi.

**MWENYEKITI:** Alishatolea maelezo, sasa tunatunga sheria, maana tukianza kuelezana hapa, tutarudi kule kule kwenye mjadala.

Ibara ya 79

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 80

Ibara ya 81

Ibara ya 82

Ibara ya 83

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 84

Ibara ya 85

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 86

Ibara ya 87

Ibara ya 88

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 89

Ibara ya 90

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 91

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 92

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Wakati akifanya majumuisho, Naibu Waziri alisema kwamba, hakukubaliana na hoja yangu kuhusiana na *damaged mobile telephones* kwamba, bado inaweza kuwa inatuma au wakatumia *e-mail*. Sasa labda hapa wangeweza kufafanua vizuri kwamba, itakuwa *damaged* kiasi gani kwa sababu kama iko *damaged* na itaendelea kutuma *e-mail*, maana yake ni kwamba *ina-function*. Sasa kama inafanya kazi na mimi ndiye mwenye simu, sijui kama nitakuwa nawajibika tena kwamba imeumia tu, lakini inafanya kazi kwa hiyo nikaripoti tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *e-mail* itakuwa inafanya kazi inavyotakiwa, kwa sababu tumesema hapa kwamba itakuwa *damaged*, kwa hiyo lazima kwa vyovoyote vile Mheshimiwa Mbunge aripoti kwamba simu yake iko *damaged* na ikiwa *damaged* siku nyingine, *e-mail* bado itakuwa inaendelea kufanya kazi, lazima aripoti.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya ziada kuhusiana na *e-mail*; *e-mail* siyo namba ya simu ambayo kama simu imekuwa *damaged* ile *SIM card* ambayo ilikuwa inatumika kwenye ile simu ikitumika kwenye simu nyingine watajua kwamba ilikuwa ni ya simu ile iliyokuwa *damaged*. Kwa hiyo, ndio maana tuna *obligation* ya kuripoti kutokana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa maelezo ya ziada.

Ibara ya 93  
Ibara ya 94  
Ibara ya 95  
Ibara ya 96

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 97  
Ibara ya 98

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 99

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 100  
Ibara ya 101

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102  
Ibara ya 103

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 104  
Ibara ya 105  
Ibara ya 106  
Ibara ya 107  
Ibara ya 108  
Ibara ya 109

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 110  
Ibara ya 111

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 112  
Ibara ya 113  
Ibara ya 114  
Ibara ya 115

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 116  
Ibara ya 117  
Ibara ya 118  
Ibara ya 119

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 120

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 121

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 122

Ibara ya 123

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 124

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 125

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 126

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na marekebisho kwa maana ya ile *fine*, lakini sasa tumefanya marekebisho mengine ili iwe na vifungu vitatu; 126(1), 126(2) na hiyo inayosomeka hapo ilipo itakuwa 126(3). Nawea nikaisoma: 126(1) isomeke *there shall be established a National Computer Emergency Response Team (CERT), shall be responsible for coordinating irrespective of cyber security and computer related incidents and corporate with other CERT's in the World.* Hiyo ndiyo itakuwa 126(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, 126(2) inasema: “*The Minister shall make regulations by the ... as a composition, duties and functions of CERT* ili yokuwepo inakuwa 126(3).

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 127

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 128  
Ibara ya 129

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 130  
Ibara ya 131

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 132

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 132 imefanyiwa marekebisho lakini marekebisho yaliyofanywa yanahusiana na *2000 dolars* kuwa ni 3 milioni. Sasa hiki kifungu ulivyo sema, tunatunga Sheria katika hii adhabu iliyotolewa hapa, ukweli wa mambo ni mkubwa mno kwa kutilia maanani hawa watu wanaohusika katika kifungu hiki ni mawakala wadogowadogo wanaouza simu; kufanya hivi ni kwamba huondoa hii ajira wasiweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, *three million fine* ndiyo mtaji wa hawa mawakala wanaouza simu na pengine haufiki. Kwa hiyo, tukiweka adhabu ya milioni tatu ni sawasawa na kuwa tunaondoajira kwa hawa watu wadogowadogo. Mimi naona hapa adhabu ni kubwa na ingeweza kuwa hata 50,000 shillings tu na ndiyo maana nilitaka Wanasheria watusaidie lakini hawakuwepo. Nilitaka ushauri wako kwenye suala hili wakati ule, sasa naomba ufanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ningeomba Mheshimiwa Waziri ujibu hili.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mhshemiwa Naibu Spika, kosa hili siyo dogo na Sheria hii inatungwa kwa ajili ya kurekodi simu ili ajulikane nani aliyenayo na hata akifanya kosa aweze kuadhhibiwa. Sasa ukisema hili siyo kosa kubwa, kwa kweli itakuwa inakwenda kinyume na tunayoyazungumzia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Uzuri ni kwamba, usipokosa hudaiwi kulipa; sasa amezungumza kuhusu wanasheria wanaokaa pale, alikuwa ameniandikia *ki-note* anasema wale wanasheria hawapo ye ye aliwa anataka kupata *consultations*. Mimi nikamjibu fanya makosa hapa nitakusahihisha hapa hapa.

Sasa kama Wanasheria wangekuwepo na masahihisho ni hayo, isingewezekana kufuatana na Kanuni kufanya marekebisho, *process* yake ni ndefu, lazima upeleke kwa maandiko saa 24 kabla ya mabadiliko yenyewe, halafu na wale wanaohusika kubadilisha wanatakiwa wapewe nakala hiyo; kwa hiyo, wasingeweza kusaidia marekebisho kwa hapa. Labda sana sana wangekusaidia maelezo. Sasa natoa maelezo siyo ya kifungu, natoa yale uliyoniambia ndiyo maana nikauliza hawa wanatoa ushauri humu ndani lakini kwa maana ya marekebisho wala wasingekusaidia.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninakubali ushauri wako, lakini Kamati hii tunaweza tukakubaliana kwa sababu adhadu ya milioni tatu kwa watu kama hawa kwa kweli ni kubwa mno, kiwango cha adhabu kimezidi kosa lenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, adhabu lazima ziwe *promotional* na kosa na kosa hili linalofanywa hapo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri siyo dogo. Kwa sababu kama huyu mtu ana-*temper* ina maana kwamba, anafanya hivyo akiwa anafahamu kwa makusudi na kama anafanya kwa makusudi, ina maana kuwa ana kitu kibaya anataka akitende, kama hatafanya hivyo hatapata hiyo adhabu kama unavyosema. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, kifungu hicho kiko sawasawa kabisa na ni moja ya njia ya kuwafanya watu kuwa watii wa sheria na kuwa na adabu vilevile. (*Makofi*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 133

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahu muu ambaye haja-rejista simu bila kujua lakini sasa *registration* ya simu kwanza inatakikana iwe ni *continuous process*. Kwa hiyo, kama muu haja-*register* ukampa adhabu ya milioni moja na laki tano na wakati Naibu Waziri anatoa ufanuzi alisema itakuwa kiwango cha mwisho *up to*, lakini kwenye *schedule of amendment* hamna; na hapa imeeleza wazi kwamba, *a fine of 1000 US Dolar*. Sasa kwenye hizi *dollars* zote itakuwa ni milioni moja laki tano kwa hiyo bado hii adhabu pia ni kubwa, haiendani kama alivyosema Mwanasheria Mkuu; uzito wa kosa lenyewe na *fine* yenyewe haviendani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni Ibara ya 133.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyoleza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwamba, adhabu hizi ni *propotional* na uzito wa kosa. Sasa *exercise* yote hii tunayoifanya na muu mmoja abakie na simu ambayo haijawa-*registerd* hilo ni kosa kwa sababu *it is a continuous process* na kwamba, tunapokwenda baada ya mwezi wa sita hata *registration*

zitakuwa zinafanyika kule kule anakonunulia simu. Kwa hiyo, ye ye akifanya hivyo kwa makusudi aendelee kutumia namna hiyo ni kosa kubwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hili hatubishani ni kwamba, Mbunge kawahamasishe itakapofika mwezi wa sita, wale wenye simu za leo wawe wame-*register* ili wasiingie kwenye matatizo haya.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mnyaa kwamba, kuna tatizo la uandishi hapa. Nafikiri maneno ambayo tungetumia ni *not exceeding* kusudi wale watakaoamua basi iwe ni kikomo kwenye *1000 US Dolars*, nafikiri haitakuwa na matatizo yoyote tuweke iwe *maximum*.

**MWENYEKITI:** Naomba usome kama inavyotakiwa kusomeka sasa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba isomeke: “*Any person who knowingly uses or causes to be used unregistered SIM card, commit an offence and shall be liable on conviction to a fine not exceeding 1,000 US Dollars or its equivalent in Tanzanian Shillings or to imprisonment for a term of six months or to both.*”

**MWENYEKITI:** Tuna-note kwamba katika Muswada mzima mliondoa habari ya *Dollar*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni sawaswa na mabadiliko yale pia yatafanyika hapa; ni suala la uandishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, nilikuona kabla Mwanasheria Mkuu hajasimama.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika sasa kwa ufanunuvi ukitoa *not exceeding* kwa sababu ndiyo itakubaliana na ufanunuvi wa Naibu Waziri.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 134

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 135

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 136  
Ibara ya 137  
Ibara ya 138  
Ibara ya 139

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 140

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 141  
Ibara ya 142  
Ibara ya 143  
Ibara ya 144  
Ibara ya 145  
Ibara ya 146  
Ibara ya 147

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 148

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 149  
Ibara ya 150  
Ibara ya 151

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 152

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 153  
Ibara ya 154  
Ibara ya 155

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 156  
Ibara ya 157  
Ibara ya 158  
Ibara ya 159

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 160

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 161  
Ibara ya 162  
Ibara ya 163  
Ibara ya 164  
Ibara ya 165

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 166

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, Ibara ya 166.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 166(1)(c), mstari wa tatu kisomeke: “*Any statement of a person relating to the affairs of any person that is made to any Officer of...*” Maneno yale yanayofuata *Tanzania Communications Regulatory* yafutwe kwa sababu yamejirudia.

**MWENYEKITI:** Utasomaje *any officer of the ...* malizia basi ukisharekebisha hivyo maana yake inakuwa *in accordance* sasa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** *An officer of the Authority in accordance with provisions of this Act.*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunafuta *Tanzania Communication Regulatory* basi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Ambayo ndiyo Authority yenyewe.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunasema Authority that is; kwa hiyo tupo wote.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 167

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 167 ile (1) iondoke kwa sabau hakuna kipengele kingine.

**MWENYEKITI:** Marekebisho ni kuondoa ile (1).

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 168

Ibara ya 169

Ibara ya 170

Ibara ya 171

Ibara ya 172

Ibara ya 173

Ibara ya 174

Ibara ya 175

Ibara ya 176

Ibara ya 177

Ibara ya 178

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 179

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 180

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 181

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 181, kwenye *numbering* iko A halafu inafuta herufi nyingine badala ya B isahihishwe.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kifungu cha 181 kina A na B, pale ilipokuwa C ifanywe B.

(*Ibara iliyoatajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 182  
Ibara ya 183  
Ibara ya 184  
Ibara ya 185  
Ibara ya 186  
Ibara ya 187  
Ibara ya 188

Jedwali la Pili

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilirudia*)

**Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (The  
Electronic and Postal Communication Act, 2009)**

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (*The Electronic Act, 2009*), kifungu kwa kifungu na imeukubali, pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huu sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara  
ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umepita njia zote, kwa upande wetu tumemaliza safari. Sasa marekebisho yaliyofanywa hapa, baada ya kundikwa yatapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili uweze kupata *sign* yake uanze kutumika kama Sheria. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Wizara na Wataalamu wake, kwa kuleta Muswada wa namna hii. Nadhani ulikuwa umechelewa.

Naomba pia niwashukuru Kamati ya Kudumu inayohusika na Muswada, imefanya kazi kubwa sana; tumewaona jana walikaa mpaka usiku wakiendelea kuuboresha Muswada huu, lakini bila wadau pia Muswada huu usingeboreka. Kwa hiyo, tunawashukuru sana wadau kwa kutoa mawazo yao ambayo yameheshimiwa na kuwekewa misingi ya kisheria. Kikubwa tunachosema, kila mmoja akiweza kutimiza wajibu katika eneo lake, tutakuwa tumejenga Tanzania yenye amani na maendeleo. Kwa hiyo, naomba niwashukuru wote na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa wiki nzima tuliyofanya kazi pamoja, haikuwa wiki nyepesi lakini tumeifanyia kazi vizuri. *(Makofisi)*

Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya sana asubuhi tumepitisha hoja wenyewe kwamba, hata Jumamosi tuko tayari kufanya kazi kwa mujibu wa Kanuni ya 151(1). Kwa hiyo, natoa taarifa kwamba, kesho tutakuwa na Bunge saa tatu asubuhi, tutauangalia Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa kwa Mwaka 2009. Kwa hiyo, Mwenyekiti na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watakuwa wamejiandaa vizuri.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine, naomba nahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.49 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 30 Januari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*

